

## KIRINYAGA WEST

102/1

### KISWAHILI

#### KARATASI 1

#### INSHA

##### 1. Insha ya lazima.

Ukiwa gavana wa kaunti mojawapo hapa nchini, umeandaa kikao na mbunge na afisa wa masuala ya kiusalama jimboni ili kujadili mikakati ya kupambana na visa vyatya ukosefu wa usalama.

Andika mazungumzo yenu.

##### 2. Uhuru unaopewa vijana leo katika nchi yetu una madhara zaidi kuliko faida.

Jadili.

##### 3. Andika insha itakayodhihirisha maana ya methali:-

Mtaka cha mvunguni sharti ainame.

##### 4. Andika insha itakayokamilika kwa manano haya:-

... Mstakiwa alimwangalia hakimu kwa macho ya huruma kisha akamwangalia mkewe na wanawe akatamani kuwaomba msamaha lakini hukumu ilikuwa imetolewa.

102/2

### KISWAHILI

#### KARATASI 2

#### (Ufahamu, Ufupisho, Sarufi na Isimujamii)

##### 1. UFAHAMU (alamu 15)

##### Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Joto kuhusu kashfa mbalimbali katika Hospitali ya Rufaa ya Kenyatta huenda limetulia kufuatia kisa cha upasuaji wa kimakosa uliofanyika majuzi. Hata hivyo, hatuwezi kuepuka ukweli kuwa, Kenyatta bado ni hospitali kubwa na muhimu sana katika nchi yetu na nje ya mipaka yetu. Kwa sababu hiyo inastahili kuboreshwa kwa kila namna. Kwa sababu hiyo inastahili kuboreshwa kwa kila namna ili iweze kutumikia idadi kubwa ya watu ambaa hububujika huko kupokea matibabu ya kitaalamu.

Kwanza, ni muhimu kutambua kuwa Hospitali ya Rufaa ya Kenyatta ni mojawapo ya hospitali kubwa nchini na katika ukanda wa Afrika Mashariki ambayo inajivunia wataalamu katika nyanja zote za utabibu. Hospitali hiyo inajivunia wataalamu wa moyo, figo, upasuaji, ngozi mionganoni mwa wataalamu wengine wanaohusika katika kusuluhisha magonjwa ya wanadamu. Kwa sababu hiyo, inatumwa katika mafunzo ya wanafunzi wanaosomea vyuo vikuu vilivypopo Nairobi na hata cha Kenyatta. Wanafunzi wazamifu pia hufanya mazoezi yao katika hospitali hii. Wengi wao huwa wanafunzi wa kimataifa waliovutiwa na ubora wa hospitali hiyo. Mashine muhimu za kupiga picha za ubongo na viungo vyatya mwili, za kusafisha mkojo, za kufanya upasuaji na za kupima magonjwa kama vile saratani zinapatikana katika hospitali hii. Kwa hakika, hivyo ndivyo vigezo vyatya hospitali bora.

Nionavyo, washikadau wanafaa kuanza mjadala kuhusu jinsi ya kuboresha huduma katika hospitali hiyo ili iweze kukidhi mahitaji ya wateja wengi wanaoitiegemea. Hii ni kwa sababu katika siku za hivi majuzi, hospitali hiyo imekuwa ikihusishwa na maovu. Awali kulikuwa na shtuma kwamba wahudumu wa mochari walikuwa wakijaribu kuwanajisi akina mama ambaa walikuwa wamejifungulia kwenye hospitali hiyo. Bila shaka shtuma kama hizo lazima zichafue jina kubwa la hospitali hiyo hata kama waliohusika walikuwa wachache tu. Lakini kisa cha upasuaji wa makosa ndicho kilichodhihirisha wazi kuwa hospitali hii inahitaji kupigwa msasa kadiri ya kina na uketo wake ili kubaini chanzo cha shida iliyopo kuna uwezekano wafanyakazi wa hospitali hii wana matatizo fulani yaliyowazonga japo hawajapata njia mfuti ya kuyawasilisha. Kwa hivyo, wanaweza kutumia mbinu mbadala ama kulipiza kisasi au kuichafulia jina hospitali hiyo.

Kumekuwa na malalamishi kuwa hospitali hii haina dawa za kutosha kwamba wagonjwa wanaotumwa kwenye hospitali hiyo hulazimika kununua dawa zao wenyewe na hivyo kupandisha gharama za matibabu. Huenda hali hiyo

ikawatamausha baadhi ya wagonjwa walalahoi ambao wanalindwa na katiba kupokea matibabu bora na ya lazima. Hospitali hii inafaa pia kutafuta mbinu za kuzuia msongamano wa wagonjwa. Msongamano huenda ni ishara ya kuwepo kwa wafanyakazi wachache au kutolewa kwa huduma duni kugatuliwa kwa huduma za afya kulinuiwa kumaliza tatizo hilo ingawaje hospitali nyingi za rufaa kwenye majimbo mbalimbali bado zinajengwa na zilizojengwa tayari hazina dawa na vifaa. Hapo ndipo serikali inafaa kuingilia kati ili Kenyatta itoe huduma bila shinikizo nyingi.

### **Maswali**

- |  |           |
|--|-----------|
| (a) Hospitali ya Rufaa ya Kenyatta ina umaarufu wa kipekee. Thibitisha.  | (alama 2) |
| (b) Bali na utabibu ni huduma nyingine gani hutolewa katika hospitali hii.   | (alama 2) |
| (c) Hospitali ya Rufaa ya Kenyataa imefikia kiwango cha hospitali bora. Fafanua.                                   | (alama 3) |
| (d) Taja kashfa mbalimbali zilizozua joto katika hospitali hii ya Kenyatta.  | (alama 3) |
| (e) Washikadau katika hospitali ya Rufaa ya Kenyatta wana wajibu upi katika kuboresha huduma katika hospitali hii? | (alama 3) |
| (f) Eleza maana za maneno yafuatayo kama yaliviyotumika katika kifungu.  | (alama 2) |
| (i) Utatibu  |           |
| (ii) Hospitali ya Rufaa  |           |

### **2. UFUPISHO (alama 15)**

#### **Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.**

Katika dunia ya leo, ni muhali siku kupita bila kupokea habari kwenye vyombo vya habari kama vile redio, runinga, gazeti ama mtandao, kuhusu maafa yanayoifanya dunia kuvuja usaha. Hiini kutokana na ongezeko la visa vya utovu wa usalama na ugaidi ambavyo kufikia sasa vimekuwa donda sugu kwa sababu ya idadi kubwa ya watu ambao huangamizwa katika vitendo vya ugaidi. Miongoni mwao, wapo ambao hufariki katika uvamizi ama mashambulizi, aidha ya moja kwa moja kwa kutumia bunduki, bastola, mizinga na mabomu au kupitia walipuaji wa kujitoa mhanga wanaotumia vilipuzi vya kujitengenezea.

Katika nchi ya Somalia, tangu kupinduliwa kwa aliyekuwa rais wa nchi hiyo Mohamed Siad Barre mnamo tarehe 26 Januari 1991, taifa hilo limeshuhudia msambaratiko, utovu wa usalama na vita. utovu huu wa usalama ukawa mwanzo wa uharamia wa kutekwa nyara kwa meli katika ghuba la Edeni, kisha maharamia kuitisha kikombozi kutoka kwa wamiliki wa meli hizo. Ingawa takwimu za hivi karibuni zaonyesha kuwa idadi ya meli zinazotekwa nyara kila mwaka katika ghuba la Edeni zimepungua, hali ingali tete. Hali hii ilifanya nchi mbalimbali zinazotumia Bahari ya Hindi kuweka mikakati kadha, ikiwemo kuwatuma wanajeshi wao kushika doria baharini ili kuwadhibiti maharamia, pamoja na kubuniwa kwa mahakama maalum nchini Kenya kusikiza kesi za maharamia hao.

Eneo la Afrika Mashariki, Kenya na Tanzania zimewahi kushuhudia milipuko ya mabomu katika balozi za Marekani mnamo mwaka wa 1998 huku Kenya ikiathirika zaidi wakati hoteli ya Kikambala mjini Mombasa ilipolipuliwa mnamo mwaka wa 2002. Hivi karibuni, Kenya imeshuhudia misururu ya mashambulizi mabaya zaidi yakiwa yale ya duka la Westgate na eneo la Mpeketoni katika kaunti ya Lamu. Naijeria pia ilishambuliwa mwaka wa 2014 wakati mashabiki wa kabumbu wakishuhudia mchuano wa kombe la Dunia.

Kutokea kwa mashambulizi hayo huwaacha watu na taathira mbalimbali. Wapo watu wanaoachwa wajane na mayatima kwa kuuawa kwa jamaa zao na wale ambao hupatwa na ulemavu wa maisha kama vile kuvunjika viungo vya mwili kama miguu na mikono au uti wa mgongo. Isitoshe, kuna wale ambao hupoteza kabisa uwezo wa kuona au kusikia. Wapo pia wanaopoteza mali ya thamani ya pesa nyingi kutokana na kuteketea kwa majengo yaliyoshambuliwa na hivyo kusababisha hasara ya kiuchumi sio tu kwa wananchi bali pia kwa serikali. Aidha, serekali na mashirika ya kiserikali na yale yasiyo ya kiserikali, hospitali, mabalozi na asasi nyingine za umma aghalabu hupoteza kiasi kikubwa cha pesa na raslimali katika kuwashudumia wahanga wa mashambulizi ya aina hii na hivyo kudumaza ustawi wao.

Kutokana na hasara za kiwango cha juu, mataifa mengi yamezidisha ari na chadi za kuangamiza ugaidi na jinai duniani ili kuhakikisha tunaishi katika dunia iliyo salama. Kinachobaki kwa raia wa nchi mbalimbali ni kuona ufanisi utakaotokana na hatua hizi.

### **Maswali.**

- (a) Fupisha aya mbili za kwanza kwa maneno (60 - 65) (alama 8, 1 utiririko)  
(b) Kwa kutumia maneno (45 - 50) eleza madhara ya ugaidi. (alama 5, 1 utiririko)
- 3. Matumizi ya lugha. (alama 40)**
- (a) **Andika sauti zenyne sifa zifuatazo.** (alama 2)  
(i) Kiyeusho cha mdomo  
(ii) Irabu ya mbele juu  
(iii) Kipasuo ghuna cha kaakaa laini  
(iv) Kikwamizo sighuna cha menoni
- (b) **Onyesha muundo wa silabi katika maneno yafuatayo.** (alama 2)  
(i) igwa  
(ii) mchwa
- (c) Ainisha viungo vya kisarufi katika sentensi hii. (alama 2)  
Alani
- (d) **Weka vitenzi katika hali ya kuamrisha kwa wingi.** (alama 2)  
(i) -nywa  
(ii) Tubu
- (e) **Geuza sentensi hii katika usemi wa taarifa.** (alama 3)  
-Sitakuja shuleni kesho," mwalimu mkuu akasema, -Nitaenda kuhudhuria mukutano Mombasa."
- (f) **Kanusha bila kutumia \_amba'** (alama 2)  
Nitavaa viatu ambavyo ni safi.
- (g) **Tunga sentensi ukitumia kiwakilishi cha pekee katika ngeli ya:- U - U** (alama 2)
- (h) **Andika kwa udogo.** (alama 2)  
Ng'ombe hao walichinjiwa karibu na mji ule.
- (i) **Bainisha miundo miwili ya kirai kivumishi.** (alama 2)
- (j) **Andika upya sentensi zifuatazo ukitumia visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari.** (alama 2)  
(i) Babangu hapendi kunywa pombe  
(ii) Mgeni alipofika ukumbini, sherehe zilikuwa zimeanza tayari.
- (k) **Andika sentensi ifuatayo upya kwa kufuata maagizo.** (alama 2)  
Yaya alimpikia mtoto chakula kitamu. (Anza kwa: Chakula ...)
- (l) **Tumia neno \_jana' kutungia sentensi kama.** (alama 2)  
(i) Nomino  
(ii) Kielezi
- (m) **Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi tofauti ya alama ya kinyota.** (alama 2)
- (n) **Onyesha yambwa katika sentensi ifuatayo.** (alama 3)  
Mwajuma alitumia ufunguo kumfungulia Amina mlango.
- (o) **Tunga sentensi katika wakati uliopo hali isiyothihirika.** (alama 2)
- (p) **Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha matawi.** (alama 4)  
Mama alimtembelea mwanawе aliyekuwa mgonjwa.
- (q) **Tunga sentensi kuonyesha jinsi kiambishi -ndi- kinavyoweza kutumiwa pamoja na nomino ifuatayo.** (alama 2)  
mapambo
- (r) **Fafanua maana mbili zinazojitokeza katika sentensi hii:-** (alama 2)  
Alitukimbilia sana
- 4. Isimu Jamii. (alama 10)**
- (a) Eleza sababu **tano** zinazomfanya mtu kufanya makosa ya matamshi na sarufi katika mazungumzo

- yake. (alama 5)
- (b) Eleza sababu **tano** zinazowafanya vijana kupenda kutumia misimu katika mawasiliano yao. (alama 5)

**102/3**

**KISWAHILI  
KARATASI 3  
FASIHI**

**SEHEMU A: HADITHI FUPI  
SHIBE INATUMALIZA - Salma Omar Hamad.**

1. **Lazima.** (alama 20)  
 —Hatwezi kumaliza kula, kila leo tunakula”  
 (a) Eleza mukadha wa dondo hili. (alama 4)  
 (b) Fafanua tamathali ya usemi iliyotumika. (alama 2)  
 (c) Eleza umuhimu wa mnenaji. (alama 4)  
 (d) —Eakini nakwambia tena, kula kunatumaliza” Kwa kudokeza hoja kumi, jadili ukweli wa kauli hii. (alama 10)

**SEHEMU B: RIWAYA  
K. WALIBORA. KIDAGAA KIMEMWOZEA.**

**Jibu swali la 2 au 3.**

2. — ... kirejea tena na kumpasulia mbarika ... Ndugu usinifikirie mwendawazimu wala mlevi ...”  
 (a) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)  
 (b) Eleza tamathali ya usemi uliyotumika. (alama 2)  
 (c) —Ardhidicho kichocheo kikubwa cha unyama wa binadamu: Kwa kudondo hoja kumi na nne, thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 14)
3. —Ndoto **g**uhuru barani Afrika imegeuka kuwa jinamizi, jinamizi inayowafanya wazalendo kulia” Kwa kudokeza hoja ishirini, eleza jinamizi hili linalowafanya wazalendo kulia. (alama 20)

**SEHEMU C : TAMTHILIA**

**Pauline Kea: Kigogo**

**Jibu swali la 4 au 5.**

4. —Ski hamsini zako wewe ... Hatutaki kufanya nira na mtu ...”  
 (a) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)  
 (b) Eleza tamathali ya usemi iliyotumika. (alama 2)  
 (c) Uongozi wa Majoka umesheheni sumu ya nyoka. Thibitisha kwa kudokeza hoja kumi na nne. (alama 14)
5. Utawala mbaya ni tatizo sugu linalozikumba nchi nyingi za kiafrika. Jadili, kwa kurejelea matukio ishirini katika tamthilia ya Kigogo. (alama 20)

**SEHEMU D : USHAIRI**

**Jibu swali la 6 au 7.**

6. **Soma shairi hii kisha ujibu maswali.**

Naingia ukumbini, nyote kuwakariria,  
Ushairi niwapeni, hoja nitawaachia,

Mnipe masikioni, shike nachoelezea,  
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Naanza kwa usalendo, nchi yetu tuipende,  
Yadhihirishe matendo, nchi yetu tulinde,  
Wa kila mtu muwendo, usije kawa mpinde,  
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Wote tuwe na umoja, tuuache ukabila,  
Kabila lisiwe hoja, mwenza kumnyima hela,  
Taifa letu ni moja, Mkenya ndilo kabla,  
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Linda demokrasia, uongozi tushiriki,  
Haki kujielezea, wachotaka na hutaki,  
Changu naweza tetea, demokrasia haki,  
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Tena adili usawa, mgao rasilimali,  
Bajeti inapogawa, isawazishe ratili,  
Idara zilizoundwa, faidi kila mahali,  
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Tuwe na uadilifu, twache tamaa ya hongo,  
Tusiwe na udhaifu, wa kuwa watu waongo,  
Tukomeshe uhalifu, kisha tuache maringo,  
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Ubinafsi si adili, ila ni kusaidiya,  
Ukiwa nayo maali, asiyenacho patiya,  
Kama mtu mswahili, ubinafsi achiya,  
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Na inavyoelezea, katiba ni kielezi,  
Tutii kwa mazoea, hadi kijacho kizazi,  
Kwa hayo nitawachia, hiyo ya ziada kazi,  
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

### **Maswali.**

- (a) Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu. (alamu 2)
- (b) (i) Onyesha aina mbili za uhuru wa kishairi uliotumiwa katika shairi hili.  
(ii) Bainisha umuhimu wa uhuru wa kishairi uliotaja hapo juu. (i) (alamu 2)
- (c) Bainisha kipengele kifuatacho cha kimtindo katika shairi hili.  
Usambamba (alamu1)
- (d) Eleza toni ya shairi hili. (alamu 1)
- (e) Bainisha nafsineni katika shairi hili. (alamu 1)
- (f) Ainisha shairi hili kulingana na:-  
(i) Mpangilio wa vina.  
(ii) Idadi ya vipande katika ubeti. (alamu 2)
- (g) Changanua muundo wa ubeti wa nne. (alamu 3)
- (h) Eleza aina mbili za urudiaji katika shairi hili. (alamu 2)
- (i) Andika ubeti wa pili kwa lugha nathari. (alamu 4)

### **7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Hukuja hapa kwa wingi,  
Vitimbi nya kila namna,  
Kunambia nikuruzuku,  
Kimwana awe mwenzio,  
Hukumtwaa mwanangu,  
Kisema mno walavu,  
Vipi wangeuza ngoma,  
Mapepo wampigia?

Siwe uloandaa,  
Harusi ya kukata na shoka,  
Masafu ya magari, yakilalama juu kali,  
Hadi kanisani kungia, mimbari wa kusimama,  
Kasema utamuezi, hadi yenu mauko?  
Vipi jicho lageukia, mitaani vipaa mwitu?

Hukunabia we fidhuli,  
Mwanangu utamtunza?  
Taandamana naye daima,  
Ja chanda na pete?  
Hukumwonjesha tamu, ya ulaghai huyuno?  
Midisko wampleka, kizingizia mapenzi,  
Vipi wamtezea shere, mwanangu kumliza?

Lini taacha dhuluma hizino humfanyiazo,  
Tuchukua lini majukumu,  
Ya kumlea na vifaranga?  
Huachi kulia u waya.  
Wanao kitelekeza  
Nadhiri zako za nitakipu promisi,  
Zi wapi mwana balaa?

Lini tafumbua maozi, uone huyu nduli,  
Alotwala wengi wapendi,  
Kwa jicho la nje kuwangia,  
Imeanguka miamba mingapi, nayo ngangania kufia dodani,  
Zinduka mwana zinduka,  
Ailayo waangamiza.

### **Maswali.**

- |   |           |
|---|-----------|
| (a) Hili ni shairi huru. Thibitisha.  | (alamu 2) |
| (b) Mwandishi anaibusha masuala kadhaa ya kijamii. Yadokeze.                  | (alamu 2) |
| (c) Bainisha nafsineni katika shairi hili.                                    | (alamu 1) |
| (d) Eleza toni ya utungo huu.   | (alamu 1) |
| (e) Bainisha matumizi ya:-  | (alamu 2) |
| (i) Mistari mishata.  |           |
| (ii) Mistari kifu.  |           |
| (f) Eleza kwa kutoa mifano mbinu za kifasihi zilizotumika katika ushairi huu. | (alamu 3) |
| (g) Eleza vile mshairi alivyotumia idhini ya kishairi katika utungo huu.      | (alamu 3) |
| (h) Bainisha umuhimu wa masuali ya balagha yaliyotumika katika ushairi huu.   | (alamu 2) |
| (i) Andika ubeti wa tatu kwa lugha tutumbi.                                   | (alamu 4) |

### **SEHEMU E FASIHI SIMULIZI**

8. Ewe malaika wangu  
Ulosuka toka mbinguni  
Mbingu kapasua kwa heri  
Siku nipokukopoa  
Ulinitia furaha iliyopasua kifua  
Tabasamu kipajini pako  
Ilinitia tumaini, ikanisahaulisha zingizi  
Ikayayeyusha madhila, ya utasa wa miaka kumi  
Ikapeperusha mbali, cheko la ukewenza.

Sasa napolia, wanitonesha jeraha  
Wanirejesha misri, kwa vitimbi vyta Firauni  
Kwa vitisho vyta muhebi  
Talaka kuahidiwa, hadi mbingu  
Lipofungua milango ya heri.

Silie mwana silie, walimwengu watakusuta,  
Tangu hapo tanabahi  
Vidume humu mwenu  
Kulia havikuumbiwa,  
Machozi na kekevu ni za kike fahamu,  
Jogoo halii daima huwika  
Nikikuona kigugumika hivi wanitia hangaiko  
Tumaini kuzima  
Udhafu kiandama  
Moyo kutia hamaniko,  
Ananipigania nani?  
Watesi king‘ang‘ania  
Changu kujitwalia?

### **Maswali.**

- (a) Thibitisha aina ya utungo huu. (alamu 2)
- (b) (i) Bainisha jinsia inayoongolewa kwenye utungo huu. (alamu 1)  
(ii) Thibitisha jibu lako la hapo juu (i) (alamu 1)
- (c) (i) Elesa nafsineni katika utungo huu. (alamu 1)  
(ii) Toa sababu mbili kuthibitisha jibu lako la hapo juu (i) (alamu 1)
- (d) Eleza sifa **tano** za utungo huu. (alamu 5)
- (e) Huku ukitoa mifano, bainisha vipengele sita vyta kimtindo ambapo nafsineni imetumia kufanikisha uwasilishaji wa utungo huu. (alamu 6)
- (f) Eleza majumumu **tano** ya utungo huu. (alamu 5)

**GATUNDU SOUTH  
102/1 KARATASI YA 1  
INSHA  
KIDATO CHA NNE  
JULAI 2018**

**MAAGIZO**

1. Katika kijiji cha Jikaze pamekuwa na ongezeko la visa vyana walio katika ndoa kujiuu na kuwaua wapenzi wao. Umealikwa na Chifu wa kijiji hiki kuwahutubia vijana kuhusu suala hili. Andika hotuba utakayoitaa ukiangazia vyanzo na suluhu kwa tatizo hili.
2. Pikipiki (bodaboda) zina faida na hasara. Jadili.
3. Tunga kisa kitakachodhahirisha maana ya methali ifuatayo:  
—Aarhiwaye akakataa hujionea mwenyewe. ”
4. Andika insha itakayoanza kwa maneno haya:  
Mshtakiwa alimwangalia hakimu kwa macho ya huruma, kisha akamwangalia mkewe na wanawe akatamani kuwaomba msamaha lakini hukumu ilikuwa imetolowa ...

for free past papers, visit: [www.freekcsepapers.com](http://www.freekcsepapers.com)

### 1. UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Kweli, taarifa zimeonekana katika vyombo vya habari kuwa vijana wetu wanajua mengi kutushinda. Wengi wameshiriki ngono ilhali tukiwa nyumbani sisi wazazi tunawaona malaika.

Kwa kweli taarifa hizo ni sawa na mbiu ya mgambo kuwa tuzungumze na watoto wetu kuhusu suala hili. Ni vyema wajue kutoka kwetu kuliko kufahamu kutoka kwa wengine amba badala ya kuwaelekeza wanawapotosha. Mara nyingi wakiwa katikati ya marika, wao hushinikizana kujaribu na wengi wanaamini kuwa kufanya mara moja sio tatizo. Lakini kile ambacho hawaelewii ni kuwa hiyo mara moja inaweza kuwabebesha mimba ama kuwaambukiza ukimwi na maradhi ya zinaa. Aidha, utu huumbuliwa na hivyo kupotoka kimaadili. Hayo ni masuala ambayo wazazi hawafai kuyaonea haya tena kwa sababu watoto wetu wanayafahamu lakini cha msingi ni kujua ukweli na hatari zilizopo.

Wazazi wengi wamewatelekeza watoto wao. Wengi husema kuwa wanawatimizia kila hitaji. Hii inamaanisha kuwa unalipa karo kwa wakati unaofaa, kuna chakula cha kutosha nyumbani, mavazi wako nayo na pia pesa za mfukoni wanazo. Lakini kile ambacho hawana ni muda wa kuwa na watoto wao. Baadhi ya matatizo tunayokumbana nayo yanaweza kutatuliwa ikiwa wazazi watatenga muda wa kuzungumza ana kwa ana na watoto wao.

Ni kweli wengi wamesingizia kazi kwa sababu wanaamka mapema na kurudi usiku. Lakini hiyo kazi ina maana gani ikiwa kesho utajipata na mjukuu wa kulea bila kutarajia? Kwa hivyo, wazazi lazima waache kuwaachia wafanyakazi wa nyumbai jukumu lao ama kuapeleka katika shule za bweni mapema kwa sababu wanawaona kuwa mzigo. Pia kuna wale ambaa huwachwa hata vilabuni kwa madai kuwa wanakutana tu na marafiki zao.

Baadhi ya mavazi, ingawaje huwafanya watoto wao kuonekana kama wanaoenda na wakati ama ya kisasa, huwa hayafai. Lazima wafunzwe tangu wakiwa wachanga kuhusu suala la kujiheshimu. Haifai kufikiria kwamba kwa sababu ni mtoto anaweza kuvalaa chochote kile. Mtoto anafaa kuvishwa mavazi ya heshima. Pia, wazazi wachunge mavazi yao wenyewe.

Maswali

- a. Eleza dhamira ya mwandishi wa makala haya. (alama 2)
- b. Kushiriki ngono mapema kwa vijana kuna athari gani kulingana na makala haya? (Alama 4)
- c. Wazazi wamechangia vipi shida zinazokumba vijana chipukizi? (Alama 4)
- d. Taja majukumu manne makuu ya wazazi kulingana na makala haya? (Alama 4)
- e. Eleza maana ya maneno haya kimuktadha.
  - a) Madai (alama 1)
  - b) Mbiu ya mgambo (alama 1)

### 2. UFUPISHO

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Katika kipindi cha mwongo mmoja uliopita, tumeshuhudia mabadiliko na maendeleo makubwa kuhusu vyombo vya habari nchini Kenya. Hapo awali, redio ndicho chombo cha habari cha kipekee kilichotamalaki kote nchini. Familia nyingi ziliweza kumiliki chombo hiki. Rusinga ilikua miliki ya wachache, hasa mabwenyenye. Sasa hivi hata akina yahe nchini na mashambani wanamiliki chombo hiki.

Rusinga kama kifaa kingine chochote cha mawasiliano kina manufaa yake. Kwanza kabisa ni nyenzo mwafaka ya kufundisha. Vipindi vinavyopeperushwa katika rusinga huwa na mafunzo kemkem kwa mtu wa kila rika. Hali kadhalika, rusinga huweza kuleta vipindi ambavyo huwafahamisha watu mambo yanayoendelea katika mazingira yao na duniani. Aidha, rusinga ikitumika pamoja na michezo ya video, hasa ya kielimu, huwafanya watu kujenga umakini pamoja na kuchua misuli ya ubongo na kuwafanya watu kuwa macho wanapofanya kazi.

Fauka ya hayo, televisheni ni chemichemi bora ya kutumbuiza na kuchangamsha. Hakuna mtu asiyependa kuchangamshwa na kuburudishwa. Televisheni ni mojawapo ya vyombo mwafaka vya kutekeleza hayo kutokana na vipindi vyake. Uburudishaji huu huwa ni liwazo kutokana na shinikizo na migogoro tunayokabiliana nayo kila siku. Uburudishaji huu hupatikana kwa urahisi majumbani mwetu.

Vivyo hivyo, runinga hutumika kama nyenzo ya kuendeleza utamaduni, kaida na amali za jamii. Vingi vya vipindi vya runinga huwa ni kioo ambacho huakisi mikakati na amali za jamii.

Kwa upande mwingine, hakuna kizuri kisichokuwa na dosari. Licha ya manufaa yake, televisheni imedhihirika kuwa na udhaifu wake. Kwanza, baadhi ya vipindi vya runinga na video hujumuisha ujumbe usio na maadili, kama vile – matumizi ya mabavu, ngono za kiholela, lugha isiyo na adabu, ubaya wa kimavazi na maonevu ya rangi, dini, jinsia, kabilia na utamaduni. Si ajabu kuwa baadhi ya vijana wetu wanaiga baadhi ya mambo haya. Vijana wetu siku hizi wameingilia ulevi wa pombe na afyuni, ngono za mapema kabla ya ndoa na mavazi yanayowaacha takribani uchi wa mnyama. Wengi wamekopa na kuyaiga haya kutoka katika runinga. Ukiwaliza wafanyacho, watakujibu kuwa ni ustaarabu kwani wameupata katika runinga.

Matumizi ya runinga na michezo ya video yasiyodhibitiwa, huweza kuwa kikwazo cha mawasiliano bora mionganoni mwa familia. Matumizi kama haya huwapa wanafamilia fursa ya kujitenga. Imedhihirika kuwa runinga haichangii kujenga uhusiano bora wa kijamii. Ukilinganisha na vyombo vingine vya burudani ambavyo hutoa nafasi ya watu kutangamana na kujenga uhusiano bora, televisheni haichangii haya. Badala yake tajriba ya televisheni huwa ya kibinfsi. Hali hii inapotokea katika kiwango cha familia televisheni inaweza kutenganisha wazazi na watoto wao.

Halikadhalika, runinga na video aghalabu hueneza maadili yasiyofaa. Mathalani baadhi ya vipindi vya televisheni huendeleza hulka ya kuhadaa, ngono za kiholela, kuvunjika kwa ndoa,n.k. hulka hizi zisizoendeleza maadili ya kijamii huchukuliwa kama zinazofaa na zinafuatwa na waliostaraabika. Huu ni upotovu.

Isitoshe, baadhi ya matangazo huhimiza matumizi ya madawa ya kulevyta kama tembo na sigara. Vitu hivi vinapotangazwa, hupambwa kwa kila hali na udanganyifu mwingi ambaa huwavutia vijana na watoto wengi. Si ajabu mtu anapowauliza wanaotumia vimeo hivi walivoanza, watajibu kutokana na athari na matangazo katika runinga na vyombo vingine.

Utafiti umeonyesha kuwa vipindi vya runinga na video ni chanzo cha matumizi ya nguvu za mabavu mionganoni mwa wanafunzi. Wazazi wengi huchukulia vibonzo katika televisheni kuwa vinalenga kuburudisha tu na havina ubaya wowote. Lakini ukweli ni kuwa, vipindi vingi vya vibonzo hushrikisha matumizi ya hila na nguvu za mabavu. Haya huibusha hamu ya vijana na watoto huyaiga.

Kwa hivyo, ni muhimu wazazi na jamii kutambua madhara ya televisheni. Utambuzi huu utawafanya wawaelekeze vijana na watoto jinsi ya kutumia televisheni na video ili kuepukana na madhara yake.

### Maswali

- (a) Kwa kuzingatia habari uliyosoma eleza manufaa ya runinga kama chombo cha mawasiliano. (maneno 50-60) alama 5  
(b) Kwa maneno kati ya 60-70, fupisha taarifa hii kuanzia aya ya tano hadi mwisho. (alama 8)

### 3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

- (a) Silabi ni nini? (alama 2)  
(b) Andika kinyume cha:  
Msichana aliingga darasani kwa haraka. (alama 2)  
(c) Tambua viambishi awali na tamati katika kitenzi:  
Aliyemlia (alama 2)  
(d) Akifisha:  
sikiliza bwana mdogo siku hizi tunaishi katika jamii ambayo imebadilika hayo mawazo yako ya zama kongwe hayatakufikisha popote alifoka abdi (alama 3)  
(e) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia matawi.  
Wote warefu ni wanafunzi. (alama 4)  
(f) Onyesha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi hii:  
Nyumba iliyojengwa jana imebomolewa. (alama 2)  
(g) Tunga sentensi sahihi ukitumia vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizoko kwenye mabano.  
(i) -fa(fanyia) (alama 1)  
(ii) soma (tendesheana) (alama 1)  
(h) Ainisha vielezi katika sentensi ifuatayo:  
Juma alitukumbusha alivyotutembelea mara kadha mwaka jana. (alama 2)

- (i) Onyesha aina ya shamirisho katika sentensi:  
Mzazi alimbebea mtoto vitabu kwa mkoba. (alama 3)
- (j) Tambua aina ya vitenzi katika sentensi:  
Amekuwa akilala kwa vile yu mgonjwa. (alama 3)
- (k) Taja na utofautishe vipasuo vya ufizi. . (alama 2)
- (l) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kutumia visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari.  
Amegura mjini kwa sababu ya mvulana huyo. . (alama 3)
- (m) Yakinisha:  
Hajanivunja mlango wala kuniibia. (alama 2)
- (n) Onyesha aina za nomino katika sentensi ifuatayo na utambue zimo katika ngeli gani.  
Kamati iliushuku werevu wake. (alama 2)
- (o) Toa maana mbili za sentensi:  
Alisimamisha gari njiani. (alama 2)
- (p) Eleza matumizi ya ~~na~~” katika sentensi:  
Njambi na Halima wanaandaliwa chakula na Hamedi. (alama 3)
- (q) Tumia mzizi ~~nye~~” katika sentensi kama kiwakilishi. (alama 1)
- 4. ISIMU JAMII**
- (a) Eleza sababu TANO zinazowafanya watu kuchanganya msimbo. (alama 5)
- (b) Kwa kutolea mifano mwafaka eleza sifa TANO bainifu za sajili ya maabadini. (alama 5)

for free past papers, visit: [www.freekcsepastpapers.com](http://www.freekcsepastpapers.com)

**KISWAHILI  
KARATASI YA 3  
FASIHII**

**SEHEMU A: Hadithi fupi- Tumbo lisiloshiba  
Alifa Chokocho na Damu Kayanda**

SWali la lazima

- Ukitumia hadithi fupi ya Tumbo Lisiloshiba na Shibe Inatumaliza, jadili maudhui ya uongozi mbaya. (alama 20)

**SEHEMU B: Riwaya- Kidagaa Kimemwozea -Ken Walibora**

Jibu swali la 2 au la 3

- ...aliyoyarithi toka kwa bwana wake mzungu yalikuwa mengi, hayahesabiki”  
 (a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)  
 (b) Eleza wasifu wa anayerejelewa. (alama 4)  
 (c) Thibitisha kwa kutoa mifano **kumi na mbili** ukweli wa kauli kuwa —aliyoyarithi kutoka kwa bwana wake mzungu yalikuwa mengi hayahesabiki” (alama 12)
- Kwa kutoa mifano mwafaka, fafanua vile usemi, — **kmbe** kuinamako ndiko kuinukako,” unavyooana na Riwaya ya Kidagaa Kimemwozea huku ukimrejelea mhusika Amani na DJ. (alama 20)

**SEHEMU C: TAMTHILIA- KIGOGO**

**PAULINE KEA**

Jibu swali la 4 au la 5

- udong haubishani na mfinyanzi”  
 (a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)  
 (b) Taja na ueleze wahusika wengine **watatu** kutoka tamthilia hii waliokuwa upande wa msemajii. (alama 6)  
 (c) Thibitisha kwa kutoa **mifano kumi** kuonyesha ukweli wa kauli kuwa udongo haubishani na mfinyanzi. (alama 10)
- Hawkuvunja mguu wa kitamathali...”  
 (a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)  
 (b) Tamko hili linamaanisha nini na ni tamathali ipi ya usemi imetumika. (alama 4)  
 (c) Taja na ueleze sifa **sita** za anayelengwa katika tamko hili. (alama 6)  
 (d) Eleza umuhimu wa anayerejelewa katika tamko hili. (alama 6)

**SEHEMU D: USHAIRI Jibu swali la 6 au la 7**

- Soma shairi hili kisha ujibu maswali

Wana-haramu

Hebu nikuulize Mama Afrika

Kwa nini.....

Mimba change ukajichukulia

Ya haramu sana ilotepetea

Ukazaa wana walojahilia

Wasiojijua, wala yao njia?

Kuzururua ukamalizikia

Bila muruwa, heba kukupotea

Ukawa ganda la kupita njia

Usiye maoni ya kuonelea

Kwa nini.....  
Ukazaa kizazi kilo kiwete  
Kilichopagawa kwa kini kite  
Hata utu wake ukakipotea?

Ah moyo waumia!  
Hupigwa na mshangao  
Niwafikiriapo

Wale barobaro wanao  
Wasaliti wanati walo na vyeo  
Walomdhidi mama mzazi wao  
Kwa muradi wao

Lakini sijali  
Sijali kwani najua  
Siku moja itawadia  
Wana-haramu watajihalalia  
Kila cha haramu kukuondolea  
Na kukutakasa

Mama wasikia?  
Hiyo siku itakapofika  
Kila la dhuluma litajikatika  
Na kila mahali utadhihirika  
Mwisho wa salata na uharamia.  
Mama wasikia?

#### Maswali

- (a) Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu. ( alama 2)
- (b) Andika maudhui manne katika shairi hili. (alama 4)
- (c) Andika ubeti wa nne kwa lugha natharia. (alama 4)
- (d) Eleza tamathali 3 za lugha na utoe mifano kutoka kwenye shairi. (alama 6)
- (e) Eleza maana ya fungu hili la maneno  
—ukazaa kizazi kilo kiwete” (alama 2)
- (f) Eleza maana ya neno hili:  
Jahili ..... (alama 2)

#### 7. KUJITEGEMEA

1. Nchi ni ile ambayo, imekita ardhini  
Sio ile iombayo, ghaibu na majirani  
Taratibu siyo hiyo, wananchi twambizaneni  
Daima hukaa chini, maganja ya mpewaji
2. Chumo lote na mitaji, leo limo maganjani  
Bepari na wanyonyaji, wasalie maguguni  
Shime utekelezaji, vingine havifanani  
Daima hukaa chini, maganja ya mpewaji
3. Twaishije tujihoji, wanachi humu nchini  
Kila tunachohitaji, kupatakwe ugenini  
Hiyo ni tete haviji, tongo tupangusaneni  
Daima hukaa chini, maganja ya mpewaji

4. Kuomba wataalamu, ni mwendo haulingani  
Tupate wa humu humu, wajuzi wa kila fani  
Mbele washike hatamu, kwa mapimo na makini  
Daima hukaa chini, maganja ya mpewaji
5. Tuufuate wongozi, pamwe na nyingi imani  
Tushiriki kila kazi, na mambo yalomkini  
Mikopo ina kinyezi, si kitu cha tumaini  
Daima hukaa chini, maganja ya mpewaji
6. Yote hatuyatimizi, alotimiza ni nani  
Lakini tuwe maizi, tusizurure mijini  
Tukamshabibi kozi, kipanga au kunguni  
Daima hukaa chini, maganja ya mpewaji
7. Shujaa itakiwavyo, aonekane vitani  
Na sisi vita tunavyo, roho kwa roho ugani  
—~~k~~tegemea” vilivyo, kondo tujiamueni  
Daima hukaa chini, maganja ya mpewaji

#### Maswali

- (a) Mtunzi wa shaii hili ana dhamira gani? (alama 2)
- (b) Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu zako. (alama 2)
- (c) Eleza mambo matatu ambayo mshairi anashauri nchi ifanye ili kujitegemea. (alama 3)
- (d) Taja aina moja ya idhini ya kishairi iliyojitekeza kwa wingi zaidi katika shairi na utoe mifano ya matumizi yake. (alama 7)
- (e) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari. (alama 4)
- (f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi. (alama 2)
- (i) Ghaibu
- (ii) Tukamshabibi

#### SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

8. (a) miviga ni nini? (alama 2)  
(b) Eleza sifa zozote **nane** za miviga. (alama 8)  
(c) miviga ina hasara katika jamii. Thibitisha kwa kutoa mifano minne. ( alama 4)  
(d) Miviga haipaswi kuangamizwa katika jamii. Toa sababu sita kutetea hoja hii. (alama 6)

**CEKENA PRE-MOCK****102/1****KIDATO CHA NNE  
KARATASI YA INSHA****MAAGIZO:**

1. Jibu maswali mawili
2. Swalii la kwanza ni la **lazima**
3. Swalii la pili lichaguliwe kutoka kwa maswali matatu yaliyobaki
4. Kila swalii lina alama 20
5. Insha iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
6. Kila insha isipungue maneno mia nne (400)

**Swalii la kwanza ( lazima )**

1. Andika tahariri kwa gazeti la Wajuzi kuhusu mada ifuatayo.  
Polisi kukabiliana na uhalifu (alama 20)
2. Hivi karibuni, serikali imeteua baadhi ya shule za bweni kuwa na kitengo cha wanafunzi wa kutwa. Jadili (alama 20)
3. Andika insha yenye kichwa kifuatacho.  
**(Mchelea mwana kulia hulia mwenyewe)** (alama20)
4. Umweso ulimweka ghafla na kuyakatiza maongezi yetu, radi ya kutisha ilifuatia. Miyo ilitupiga kwa kishindo na kutisha.....(Endeleza kisa hiki) (alama 20)

**1. Ufahamu: ( alama 20)**

**Soma taarifa ifuatayo kasha ujibu maswali.**

Inasemekana kuwa uongozi hutoka kwa Maulana. Siku hizi, kauli hii inaonekana kinyume na inapingwa vikali na mahuluki wengi. Hali hii imetokana na ukweli kuwa viongozi wengi wamekuwa katili. Wengi wao hutekeleza maovu bila kujali wala kubali. Kiongozi ye yote Yule anayedai kuwa mwema hana budi kuwa **mwongofu** na wa kuaminika; anafaa kuwa kielelezo kwa wafuasi wake. Hili lisipotendeka, **vurumai** huzuka mi ongoni mwa watu.

Kiongozi bora sharti awe mnyenyeketu. Mtu mwenye mashau si kiongozi bora. Kiongozi wa aina hii huwahudumia watu kwa moyo wake wote. Jambo hili huwafanya watu waridhike. Watu wengi hawapendi viongozi wanaojipigia debe kila wakati. Viongozi kama hawa huwachosha na hata kuwachusha wafuasi wao. Matokeo ya haya yote huwa ni majuto kwa raia huku wakijiuliza kilichowafanya wawachague.

Maadili ni sifa nyingine inayomtambulisha kiongozi bora. Kiongozi wa aina hii hafai kujihuisha na vitendo vya kikatili kama matumizi ya mabavu, mauaji na hata ufisadi. Anafaa kuwajibika kazini na kuwa tayari kuyasikilza malalmishi ya watu anaohudumia. Inamlazimu kiongozi bora kuwaheshimu wananchi bila kuzingatia vyeo vyao; asidharau maoni yao kuhusu jinsi ya kuuboresha uongozi wake.

Pia, kiongozi bora anastahili kuwa na huruma. Hii inamaanisha kuwa anafaa kuwa tayari kuwaonea **kite** wananchi wanaotatizika maishani. Anafaa kubuni mikakati ya **kuwaumi** watu kama hawa. Hali hii huwafanya watu waongeze imani yao kwa kiongozi kama huyu. Ikiwa kiongozi atajitia hamnazo anapofahamishwa kuhusu **masaibuya** wananchi, watu watatamani siku ya kumtoa mamlakani ama kwa kupiga kura au kumwomba Jalali ahitimishe uongozi wake haraka iwezekanavyo.

Utetezi wa kazi za wanyonge ni sifa nyingine muruwa ya kiongozi bora. Kiongozi kama huyu anapaswa kuwa tayari kuhakikisha kuwa sheria inafuatwa katika himaya yake. Hali hii huwafanya wanajamii kupata haki zao **bilakubughudhiwa**. Wale wasiopata haki wanazostahili wanastahili kuchungiwa maslahi na kiongozi kama huyu.

Hakuna mtu anayestahili kuitwa kiongozi bora kama si mpenda amani. Kiongozi anayepalilia rabsha katika jamii hafauli hata kidogo kuitwa kiongozi bora. Ni wajibu wa viongozi kusuluhisha ugomvi wowote uliomo mi ongoni mwa wanajamii. Jambo hili huifanya kunawiri na kuzagaa kote kote. Wanajamii wakiishi katika mazingira yenye amani huweza kutekeleza shughuli zao bila hofu wala kindubwendubwe.

Kiongozi bora anastahili kujitenga na ubaguzi kama ardhi na mbingu. Ni ukweli usiopingika kuwa baadhi ya viongozi huwabagua wananchi kwa misingi ya kitabaka, kijinsia na kikabila. Ni muhimu kwa kiongozi ye yote yule kuhakikisha kuwa kuna umaja wa wananchi katika jamii. Hii ni kutokana na ukweli kuwa jifya moja haliwezi kuinjika chungu. Astahili kuhubiri umaja katika hatamu ya uongozi wake. Nao wananchi humkumbuka daima dawamu.

Uwajibikaji ni kitambulishi kingine cha kiongozi aali. Kiongozi bora anafaa kuwajibika kazini. Kiongozi anayestahili niyule ambaye anatekeleza majukumu yake kikamilifu. Suala la upigaji zohali ni muhali kwa kiongozi wa aina hii. Ni mtu anayefanya kazi kimhanga ili kuuboresha maisha yake naya wateja wake.

Kiongozi ye yote asiye na hulka tulizozungumzia huishia kuwa hasimu wa watu. Viongozi wote wanastahili kuyapa kipaumbele maslahi ya umma. Hawafai kuwa wabinafsi. Ni watu wenye utu, maarifa, waongofu na wenye bidii. Wananchi wana wajibu wa kuwachagua viongozi wanaofaa bila kupofushwa na ahadi za uongo.

### **Maswali**

- a) Kwa nini kauli kuwa, uongozi hutoka kwa Maulana, yaonekana kinaya na kupingwa na watu wengi? (alama 1)
- b) Eleza kiini cha watu wengi kuchukia viongozi wanaojisifu kila wakti. (alama 2)
- c) Eleza matokeo ya kiongozi kuwasaidia wananchi wanaotatizika maishani. (alama 1)
- d) Taja misingi mitatu inayotumiwa na baadhi ya viongozi kuwabagua wananchi (alama 3)
- e) Eleza maoni ya mwandishi kuhusu jukumu la wananchi kuhakikisha kuwa uongozi bora umedumu (alama 1)
- f) Taja vitambulishi vinne vya kiongozi bora. (alama 4)
- g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yaliviyotumika katika ufahamu.
- (i) Mwongofu
  - (ii) Kuwaani
  - (iii) Kite

### **Ufupisho.**

Swala la nidhamu ni nyeti sana ambalo lafaa kushughulikiwa ipasavyo ili mambo yawe shwari katika ulimwengu. Nidhamu inapodumishwa basi maswala mengine huwa rahisi kutekeleza popote pale. Katika Biblia, ni dhahiri kuwa Bwana Mungu aliumba mwanadamu kamilifu, Adamu, akamweka katika bustani ya Edeni ili atawale viumbe wengine. Mungu alimpa Adamu uhuru wa kula chochote alichotaka katika bustani ya Edeni lakini akamkataza kula matunda kutoka kwa mti uliokuwa katikati ya bustani hiyo. Baadaye Mungu akagundua kuwa Adamu alikuwa na kitwea cha ajabu kasha akaamua kuumba Hawa ili awe msaidizi wake. Bila shaka Adamu alifurahi kwa hatua hii. Hata hivyo, Hawa alindanganywa na shetani aliyejuka kwa mfano wa nyoka, akala tunda walilokatazwa na Mungu na hatimaye akampelekea Adamu naye akala. Matokeo yalikuwa kwamba walijipata uchi kisha Mungu akakasirika nao na kuwafukuza kutoka kwa bustani na kuwapa adhabu.

Mwanamume aliambiwa kuwa angefanya kazi na kutokwa na jasho ili apate chakula. Mke naye aliambiwa kuwa kujifungua kungekuwa nauchungu mwingi. Naye nyoka akaambiwa atakuwa na uadui mkubwa kati yake na mwanadamu na angekuwa akifa kwa kugongwa kwenye kichwa. Hata hivyo Mungu hakuwatekeleza wanadamu kabisa. Bwana Mungu alimtuma Yesu akafa mtini ili kila amwaminiye asiye akaangamia, bali aweze kupata uzima wa milele. Ni dhahiri kuwa Mungu alikosewa sana na wanadamu aliowaumba lakini hakuwatupa kabisa bali aliwajalia nafasi nyingine ya kuwa wana wake. Ikiwa Mungu alifanya haya, sembuse sisi binadamu? Kila mwanadamu hukosea nani vyema njia mwafaka zifuatwe katika kutekeleza adhabu ili anayeadhibiwa aweze kubadilika na kuona makosa yake. Adhabu inapotolewa nivyema kwanza kuchunguza cha kitendo, sababu zinazopelekea kutendeka kwa kitendo hicho, dhamira ya mtendaji na athari za kitendo husika. Baada ya haya, mhusika atakuwa katika hali bora ya kutekeleza adhabu.

Katika nchi yetu kwa mfano, adhabu hutolewa katika asasi mbalimbali kama vile shule, vyuo, ndoa kanisa msikiti mionganoni mwa asasi nyingine. Katika ndoa kwa mfano, mke anapokosea mumewe adhabu lazima iambatane na era za kijamii na kimataifa. Kwa mfano, swala la kuwapiga wanawake au wanaume katika ndoa halifai kabisa katika ndoa yoyote hata kama mtu amefanya kosa gani! Kuna njia mwafaka za kuleta masikilizano katika ndoa kama vile kushauriana, kuomba ushauri, nasaha au pia kwenda kanisani. Pia mambo yamezidi sana ambapo wanawake wakidhulimiwa wanaishia kuwaumiza waume zao sana au hata kuwaua! Swali ni je, ukiua mtu umesuluhisha tatizo lolote? Adhabu yoyote lazima iambatane na uzito wa kosa na pia athari zake kwa mhusika lazima zichunguzwe kabla ya adhabu yenye kutolewa.

### **MASWALI**

- a) Fupisha aya mbili za kwanza. (maneno 60-80) (alama 10, moja ya utiririko)  
 b) Fupisha aya ya tatu (alama 5, Moja ya utiririko)
- 3. Matumizi ya lugha**
- a) Andika sifa zozote mbili za sauti zifuatazo. (alama 2)  
 (i) /u/  
 (ii) /ch/
- b) Andika maneno yenyе miundo ifuatayo. (alama 2)  
 (i) Konsonanti, Konsonanti, irabu, irabu, konsonanti, irabu  
 (ii) Konsonanti, irabu, konsonanti, irabu, konsonanti, konsonanti, irabu
- c) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi tofauti ya kiakifishi yifungo‘ (alama 2)
- d) Tambua ngeli za nomino zifuatazo (alama 2)  
 (i) Kithembe  
 (ii) Pango
- e) Tunga sentensi ukitumia (alama 2)  
 (i) Kihusishi cha ulinganisho  
 (ii) Kihisishi cha hasira
- f) Ainisha virai vivilyopigwa mstari katika sentensi ifuatayo (alama 2)  
Mwalimu mrefu mwembamba atawatuza wanafunzi kesho asubuhi
- g) Ainisha mofimu katika neno \_awaye‘ (alama 2)
- h) Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa.  
 —Rjelea maelezo katika kitabu ili kuhakiki majibu yako, mwalimu alimwambia mwanafunzi (alama 3)  
 i) Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo. (alama 2)  
 (i) Thibiti  
 (ii) Dhoofisha
- j) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mtindo wa matawi (alama 4)  
 Ambao walipewa zawadi walicheza vizuri sana
- k) Kwa kutunga sentensi mbili, onyesha matumizi mawili ya kiambishi ku‘ (alama 2)
- l) Tunga sentensi moja yenyе kivumishi cha idadi jumla na kielezi cha idadi jumla (alama 2)
- m) Andika sentensi ifuatayo kwa kufuata maagizo. (alama 2)  
 Nyanya alifurahia matokeo ya mjukuu wake  
 Anza: Matokeo.....
- n) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo (alama 2)  
 Anita alisema kuwa angeenda kwao
- o) Kanusha sentensi ifuatayo katika hali ya udogo wingi (alama 2)  
 Mbwa wake ana meno makali
- p) Andika visawe vya maneno haya (alama 2)  
 (i) Cheki  
 (ii) Ndoa
- q) Tunga sentensi kwa kuzingatia kauli zifuatazo (alama 2)  
 (i) Kauli ya kutendeshea  
 (ii) Kauli ya kutendua
- r) Andika maana ya nahau zifuatazo (alama 2)  
 (i) Bugia chumvi  
 (ii) Meza mrututu
- s) Andika methali inayoafiki maelezo yafuatayo (alama 1)  
 Heri kidogo ulichonacho kuliko kingi unachoahidiwa
- 4. Isimujamii**
- (i) Eleza maana ya Lafudhi (alama 2)  
 (ii) Eleza sababu nane zinazosababisha Lafudhi (alama 8)

**102/3**

**KIDATO CHA NNE  
FASIHI**

**SEHEMU A: USHAIRI**

**LAZIMA**

**Soma mashairi haya kasha ujibu maswali**

**SHAIRI: A  
MWANAMKE**

1. Namwona yu nyumbani  
Na jembe mikononi,  
Analima,  
Mwanamama,  
Mavuno si yake  
Ni ya mume wake
2. Namwona viwandani,  
Pia maofisini,  
Yu kazini,  
Hamkani,  
Anabaguliwa,  
Na anaonewa.
3. Namwona yu nyumbani,  
Mpishi wa jikoni,  
Yaya yeye,  
Dobi yeye,  
Hakuna malipo,  
Likizo haipo.
4. Namwona kitandani,  
Yu uchi maungoni,  
Ni mrembo,  
Kama chombo  
Chenye ushawishi,  
Mzima utashi.
5. Namwona mkekani,  
Yuwamo uzazini,  
Apumua,  
Augua,  
Kilio cha kite,  
Chapa mpiga pute.
6. Kwa nini mwanamke,

**SHAIRI B  
WANAWAKE**

1. Wanawake ni wavyazi  
Na wao ndio walezi,  
Kwetu sisi wapumbavu,  
Kutupumbaza pumbaa.
2. Ndio wao waadhamu  
Watutowao hamumu  
Tunaposhidwa na ghamu  
Ya mambo yakinuva.
3. Hakika Ukiwatunda  
Huna budi kuwapenda  
Na wendapo kuwadanda  
Lazima utawavaa.
4. Kwa hakika mwanamke  
Ni kiumbe kilo pweke  
Na waume mupulike  
Wana mengi manufaa.
5. Kwa ufupi nakueleza  
Haya basi nisikiza  
La kwanza hututuliza  
Wapo nyumbani mwakaa.
6. Chakula ukikileta  
Mcheleo au nyata  
Hupika pasi matata  
Vikaiva kwa hawaa.
7. Au tuseme muhogo  
Na vijisamaki ngogo  
Utuwapo mzigo  
Kama huo kwa jamaa.
8. Huyo hufanya haraka

for free past papers, visit: [www.freecesepapers.com](http://www.freecesepapers.com)

- Ni yeye peke yake,  
Anyimwaye,  
Heshimaye,  
Haki anakosa,  
Kwa kweli ni kosa.
9. Ikawa tahangaika  
Kushughulika kupika  
Chakula kukiandaa.
10. Atafazaika sana  
Kukupikia kimwana  
Kwa sababu yako bwana  
Kwa kujuwa yako njaa.
11. Unapotoka kazini  
Au mwanaawe shulenii  
Ajuwa wa taabani  
Kwa tumbo kukamaa.
12. Pili ndiye mkombozi  
Wa kuteteza uzazi  
Wa kuongeza mizizi  
Udugu na ujamaa.
13. pindi unapouguwa  
Kwakowe hujisumbuwa  
Kukutafutia dawa  
Hana dakika kukaa
14. Huituza nyumba yako  
Hunadhifu nguo zako  
Na zaidi viro vyako  
Ambavo nya manufaa.
15. Yataka tuwahesimu  
Mno sana tufahamu  
Yafaa tuwakarimu  
Kamba nipa wee twaa.

- (i) Yalinganue na kulinganisha mashairi A na B kimuundo (alama 4)  
(ii) Kwa kurejelea kigezo cha mishororo eleza bahari za mashairi A na B (alama 2)  
(iii) Eleza madhumuni ya mtunzi wa shairi A (alama 2)  
(iv) Tofautisha toni katika mashairi haya mawili (alama 2)  
(v) Suala la ubabedume limeangaziwa kwa kina katika shairi A. fafanua (alama 4)  
(vi) Mwanamke wa shairi A anahitilafiana na wa shairi B. Jadili. (alama 2)  
(vii) Shairi B ni wosia kwa wanajamii. Thibitisha dhana hii. (alama 2)  
(viii) Eleza maana ya kifungu yikawa kwa hawaa‘ katika ubeti wa sita wa shairi B (alama 2)

## SEHEMU YA B: RIWAYA

- 2. Kidagaa kimemwozea (alama 40)**
- (i) Mama alipothubutu kupatana nao, walitaka kupasuka kwa hasira. Hawakutaka suluhu wala kusafianania (alama 4)  
a) Eleza muktadha wa maneno haya (alama 4)  
b) Tambua mbinu mbili zilizotumika katika dondoo (alama 2)

- c) Tambuana ueleze mgogoro unaoangaziwa katika dondoo hili. (alama 2)  
d) Eleza Migogoro mingine sita inayojitokeza katika riwaya hii (alama 12)
3. Matukio mengi ya riwaya kidagaa kimemwozea ni kinaya cha maisha ya binadamu. Jadili (alama 20)

### SEHEMU YA C: TAMTHILIA

#### Kigogo na Pauline Kea

#### Soma swalii lifuatalo kisha ujibu maswali

4. —..... wanadai kitu kikubwa au kitu chote!”  
a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)  
b) Tambua maudhui yanayodokezwa kwenye dondoo hili (alama 2)  
c) Kwa kutumia hoja sita eleza namna maudhui uliyoyataja hapo juuyanavyojitokeza katika tamthilia ya kigogo (alama 6)  
d) Fafanua wasifu wa msemewa (alama 4)  
e) Fafanua umuhimu wa msemaji (alama 4)
5. Tamthilia ya -Kigogo”ni tamthilia ya tanzia. Thibitisha kwa kufafanua mifano kumi (alama 20)

### SEHEMU YA D: HADITHI FUPI

6. Ubadhirifu wa mali ya umma umetamalaki katika hadithi ya shibe itatumaliza. Jadili kwa kutoa mifano mwafaka (alama 20)

#### 7. Tumbo lisiloshiba.

Kwetu tunapigania mikono ielekee vinywani. Mzoea vya sahani, vya kigae haviwezi

- a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)  
b) Taja tamathali moja ya usemi inayojitokeza kwenye dondoo (alama 2)  
c) Fafanua sifa za msemaji (alama 2)  
d) Jadili maudhui ya utabaka ukirejelea hadithi husika (alama 20)

### SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

#### 8. Fasihi simulizi

- a) Taja vipera viwili vya maigizo (alama 2)  
b) Eleza sifa zozote nne za kumuundo za maigizo (alama 4)  
c) Fafanua majukumu yoyote sita ya maigizo katika jamii ya kisasa (alama 12)  
d) Mbinu zifuatazo zina umuhimu gani katika uwasilishaji wa fasihi simulizi  
(i) Uradidi  
(ii) Uigaji sauti (alama 2)

## **MERU CLUSTER**

**102/1**

### **KISWAHILI**

**Karatasi 1**

**(Insha)**

#### **1. LAZIMA**

Wewe ni mkurugenzi wa kampuni ya mzalendo. Kumekuwa na utepetevu na uzembe kazini. Waandikie wafanyakazi memo kuwaonya dhidi ya jambo hili.

2. Andika insha kuhusu jinsi raia wanavyoendeleza matumizi mabaya ya ardhi.
3. Usalama unazidi kuzorota jimbo la Meru. Jadili chanzo chake na jinsi ya kutatua.
4. Andika kisa kitakachomalizikia kwa maneno :  
... kweli binadamu heshi vituko. Niliyemdhania kuwa ndiye kumbe siye.

**102/2**

### **KISWAHILI**

**Karatasi 2**

#### **1. UFAHAMU**

##### **Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yote.**

Muasi mila bila shaka ni mtwana ama kijakazi ijapokuwa mlowezi au mkimbizi. Yakini ni kuwa hata wakirmbizi walowezi hawaghafiliki lugha zao. Basi ni jambo la kutatanisha si haba lukuki za wananchi wanaojidai wazalendo wakibekua kufahamu lugha hii bila kuitumia. Si ajabu wengi wamekuwa safihi katika mazungumzo ya Kiswahili na anayejaribu basi huonekana mbumbumbu mzugu wa reli.

Kiswahili kama somo vile vile lilipuuza na linaendelea kupuuzwa, kwani dalili ya mvua ni mawingu. Jiulize kwa nini huko ufaransa lugha inayotumiwa ni kifaransa, katika vitengo vya elimu ilhali nchini Kiswahili kimeandimika kama theluji ya kukaanga katika viwango fulani vya elimu.

Ilikuwa tu juzi nilipokuwa nikirandaranda afisini humu nchini nikitafuta gange, niliambiwa ajizi ni nyumba ya njaa. Nilipigwa bumbuazi kwani katika orodha ya matakwa ya waajiri, Kiswahili hakitiliwi maanani kabisa na hata kwингine hakitajwi.

Si ajabu kuona kuwa wafanyakazi wengi humu nchini hawawezi kuwasiliana kwa lugha takata.

for free past papers, visit [www.Irreekcsepapers.com](http://www.Irreekcsepapers.com)

Naam, si vizuri kuacha mbachao kwa mswala upitao, lakini hebu tazama maktaba humu nchini zimejaa vitabu vya Kiingereza, Kifaransa.... Lakini hata! Vya Kiswahili ni vichache mithili ya rasharasha mkurungani. Kweli mfinyanzi hulia gaeni na mababu zetu wangerauka kabla ya siku ya kiama hawangeweza kupata pahali pa kujificha kutoona utandu huu wa tahayuri. Ibra vinyinginya wetu kutomaizi tahajia ya Kiswahili.

Ushababi ni fahari ya kila mja na ni haki kwa wote, mgalla muue na haki umpe. Lakini nasikitika kusema kuwa vijana wamefanya tadbiri katika uenezaji wa lajaja iitwayo 'sheng' iliyo kama msumari wa moto juu ya kidonda kwa Kiswahili. Vijana watumia 'sheng' huku wakikiacha Kiswahili katika kaburi la sahau.

Langu ni kuwatahadharisha, uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti na pia mbio za sakafuni hazina budi kuishia ukingtoni.

Nina kiwewe chungu nzima kusema kuwa hata shulenii Kiswahili hakipewi umuhimu. Mfano mwafaka ni idadi ya vipindi vinavyotengwa kwa kila somo, vya Kiswahili ni haba. Si ajabu mtihani wa Kiswahili haufanywi vyema na wengi.

### **Maswali**

- a) Uzalendo wa wananchi ni wa kutiliwa shaka. Thibitisha kauli hii ukirejelea kifungu. (alama 1)
- b) Eleza jinsi Kiswahili kinaweza kupata sura mpya kisera. (alama 4)
- c) Ni jinsi gani washikadau wanadidimiza maendeleo ya Kiswahili nchini. (alama 4)
- d) Ukiwikita katika kifungu, onyesha ukweli wa kuacha mbachao kwa mswala upitao. (alama 2)
- e) Vifungu vifuatavyo vina maana gani kwa mujibu wa kifungu? (alama 2)
  - i) mbumbumbu mzungu wa reli
  - ii) nikikunja jamvi
- e) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyonumiwa katika kifungu. (alama 2)
  - i) hawaghafiliki
  - ii) tadbiri

### **2. MUHTASARI**

#### **Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yote.**

Wengi wetu tunaweka fedha benki. na labda huenda ikawa hiyo ndiyo akiba ya pekee tuliyonayo. Kwa mfano, watumishi wengi waishio katika miji mikubwa hawana nyumba zao wenye wala mavuno (kama yale mavuno ya shamba) ambayo wangeweza kuweka kama akiba yao. Walicho nacho ni mishahara yao tu, basi, ambayo inalipwa kwa fedha zinazopitia benki. Watu wengi wanapoweka fedha benki kusudi lao ni kuondokewa na wasiwasi kwa vile wanafahamu fedha zao ziko mahali pa salama. Watu wanaoweka fedha zao (hasa fedha nyingi) nyumbani mwao, mifukoni, kabatini ndani ya magondoro au kuzichimbia chini - ni watu wajinga. Fedha zao huenda zikapotea au zikaharibiwa na mchwa, au zikatoweza ikiwa nyumba inaharibiwa na moto au mafuriko. Wakati mwengine ikiwa mwenye nyumba amefariki dunia ghafla au kwa bahati mbaya. pasipo kuacha wasia wowote na kabla hajamjulisha mtu kama kuna fedha alizozichimbia chini, basi pesa zake zinaozea mumo humo, mtu "anakufa na pesa zake." Pamoja na hayo ipo hatari kuwa fedha zinazofichwa nyumbani zinaweza kuibwa na wezi au kutumiwa ovyo ovyo kwa sababu zipo. Mtu anapoweka fedha zake benki anaondokewa na mashaka yote haya. Kwani benki ni mahali penye usalama. Fauka ya hayo hazitumiki ovyo ovyo au hatari yoyote ile kuzikabili.

Mtu anapoweka fedha zake benki, anaweza kupata faida ya riba ilipwayo na benki kila mwaka na kwa hivyo fedha yako huongezeka zaidi. Mtu akifungia shilingi elfu kumi ndani ya sanduku (kasha) kwa muda wa miaka kumi au ishirini, akifungua atapata kiasi kile kile. Lakini akiweka benki atakuwa na kiasi zaidi. Mtu mwenye fedha benki anaweza kulipa madeni yake kwa njia ya hundi. Hundi ni hati maalum iliyoandikwa na kutiwa sahihi na mtu

mwenyewe, ambayo inamruhusu mkuu wa kulipa deni Fulani kwa kupunguza akiba ya fedha iliyo chini ya jina la mtu yule. Hii ndiyo njia bora zaidi ya kulipa malipo ya kila aina - mishahara, kodi na madeni yote makubwa. Mwenye deni anaandika tu na kutaja kuwa mtu fulani au kampuni fulani au shirika fulani au serikali ilipwe fedha kiasi fulani halafu benki ndiyo inayomlipa huyo mtu, kampuni au serikali au shirika kwa kupunguza kilichotajwa kutoka kwcnye akiba (ghafla) ya mwekaji katika benki hiyo.

Utumiaji wa hundi unapunguza sana hatari ya wizi na pia unarahisisha malipo kwa watu wanaoshi mbali maana hundi ni kikaratsi ambacho unaweza kukifungia ndani ya bahasha na kukipeleka kwa njia ya posta. Tena ni shida sana mtu kukiiba bila kubainika. Mwekaji fedha hufaidika sana kwani benki inamsaidia kuweka hesabu iliyo kamili ya mapato na matumizi yake. Hii ndiyo maana karibu malipo

yote ya idara za serikali, makampuni, vyama mbalimbali na mashirika hulipwa kwa njia ya hundi na kutofanya hivyo huonekana kama ni kinyume cha sheria.

Kwa kweli, kazi za biashara inayoendeshwa kwa kutumia "fedha" za hundi ni kubwa sana kuliko ile inayoendeshwa kwa fedha taslimu.

- a) Bila kubadilisha maana aliyokusudia mwandishi, fupisha aya mbili za kwanza. (Maneno 60-70)  
(alama 7, 2 za mtiririko)
- b) Eleza mawazo makuu ya mwandishi katika aya mbili za mwisho. (maneno 40-50)  
(alama 5 na 1 ya mtiririko)

### 3. MATUMIZI YA LUGHA : (ALAMA 40)

- a) Tofautisha sauti zifuatazo ukizingatia uzuiliaji wa hewa. (alama 2)  
i) ny .....  
ii) y .....
- b) Andika upya sentensi ifuatayo kwa kubadili maneno yaliyopigiwa mstari kwa nomino. (alama 2)  
Mwanafunzi mwerevu alitafakari
- c) Tunga sentensi ukitumia \_ja' katika kutendewa. (alama 2)
- d) Yakinisha sentensi ifuatayo katika ukubwa wingi.  
Mtoto wa mjini hakunywa maziwa aliyopewa na msichana. (alama 3)
- e) Ainisha viambishi katika neno lifuatalo :  
furahiwa (alama 2)
- f) Andika sentensi ifuatayo katika msemo wa taarifa :  
—Ninjatolea kwangu kuwapokea wageni hawa leo.” Mwenye nyumba alisema. (alama 2)
- g) Tunga sentensi yenye muundo ufuataao : (alama 3)  
i) nafsi  
ii) yambwa  
iii) mzizi  
iv) kutendea  
v) kutenda  
vi) kirejeshi
- h) Eleza uamilifu wa maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo. (alama 2)  
i) Kazi yoyote itafanywa na mafundi hawa.  
ii) Kazi yote itafanywa na mafundi hawa.
- i) Toa mfano wa sauti mwambatano ya kaakaa gumu. (alama 1)
- j) Tunga sentensi yenye muundo ufuataao : (alama 3)  
N + V + V + E + t + N

- k)** Nomino zifuatazo ni za ngeli gani ? (alama 2)  
 i) kiu .....  
 ii) bidhaa .....
- l)** Eleza majukumu mawili ya sentensi ifuatayo : (alama 2)  
 Ondoka hapa na nikikupata tena nitakushtaki!
- m)** Tunga sentensi ukitumia kihusishi cha wingi wa ngeli ya I-ZI. (alama 2)
- n)** Tambua kiarifa na chagizo katika sentensi ifuatayo : (alama 2)  
 Mjomba alijengewa nyumba kubwa kwa mawe msimu uliopita
- o)** Tumia jedwali kuchanganua sentensi ifuatayo: (alama 4)  
 Dereva aliendesha gari ila utingo hakuwa analipwa nauli.
- p)** Tunga sentensi ukitumia wakati ujao hali endelevu. (alama 1)
- q)** Eleza matumizi ya kwa‘ katika sentensi ifuatayo: (alama 1)  
 Mfungwa aliachiliwa kwa kubadili tabia zake.
- r)** Bainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo  
 Nyinyi mtapadiwa mbegu kwa jembe la mtwana huyu. (alama 3)
- s)** Tunga sentensi kudhihirisha matumizi ya kinyota. (alama 1)

#### 4. ISIMUJAMII (ALAMA 10)

—Hay basi. Beba mmoja! Beba mmoja! Dada njoo. Nafasi ni ya mmoja. Ni mbao tu. Bei ya chini Usiachwe, bei ni poa.”

- a)** Taja sajili inayorejelewa na maneno haya. (alama 2)  
**b)** Fafanua sifa nane za sajili hiyo. (alama 8)

for free past papers, visit: [www.freekcsepapers.com](http://www.freekcsepapers.com)

**SEHEMU YA A : TAMTHILIA****Kigogo : Pauline Kea****1. LAZIMA**

—Asant ya punda kweli ni mateke. Sikujua ungekuja kunihangaisha ...”

- a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
- b) Onyesha jinsi msemewa anamwangaisha msemaji. (alama 2)
- c) Kwa kurejelea tamthilia nzima onyesha ukweli wa methali —Asate ya punda ni mateke.” (alama 14)

**SEHEMU B : HADITHI FUPI****Tumbo lisiloshiba na hadithi nyingine****Jibu swalii la 2 au 3**

2. —... mendeleo yanadai mchango wa kila mtu, maskini na tajiri”
  - a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
  - b) Taja na ueleze sifa nne za msemaji katika dondoo hili. (alama 4)
  - c) Mambo yepi mengine ambayo msemaji huhojiana na wenzake wanapokutana? (alama 6)
  - d) Taja na ueleze maudhui matatu yanayojitokeza katika dondoo hili. (alama 6)
3. Kwa kurejelea hadithi zozote tano katika diwani ya, Tumbo lisiloshiba na hadithi nyingine. ‘Jadili maudhui ya nafasi ya wazazi katika malezi. (alama 20)

**4. SEHEMU YA C : USHAIRI***Soma shairi lifuatalo kisha uyajibu maswali.*

Mungu naomba subira, subira nayo imani  
Imani iliyo bora, bora hapa duniani

Duniani mwa kombora, kombora nayo hiani  
Hiani pamwe ukora wenyewe kuhini.

Kuhini kwenye kiburi, kiburi naufidhulu  
Ufidhuli wa kudhuri, kudhuri wangu muwili  
Muwili hata kidari, kidari kuwa thakili  
Thakili kisinawiri, kisinawiri misuli.

Misuli kuwa hafifu, hafifu kama muwele  
Muwele wa hitilafu, hitilafi ya nduwele  
Nduwele kutakilifu, kutakilifu milele  
Milele kutoniafu, kutoniafu na vishale.

Vishale vinitomele, vitomele vikwato  
Vikwato pia maole, maole kufanya mito  
Mito ya matozi tele, tele mithili kitoto  
Kitoto kilo vipele, vipele vyenye fiakuto.

Fukuto lanipa neno, neno hili kutamka  
Kutamka wazi vino, vino subira kutaka  
Kutaka imani mno, mno n'sipate wahaka  
Wahaka wa matukano, matukano na mashaka.

Mashaka haya ya leo, leo yawe yarne pita  
Yanie pita na vilio, vilia vipishe nyota  
Nyota njema ingara o, ing'ara o kunikita  
Kunikita salamani, salamani nikadata.

- a) Kwa nini nafsi neni inaomba subira na amani ? (alama 2)
- b) Shairi hili ni la aina gani kwa kuzingatia :
  - i) Mpangilio wa maneno (alama 4)
  - ii) Mpangilio wa vina
- c) Kwa kutokea mifano eleza mbinu mbili za lugha zilizotumika katika shairi. (alama 4)
- d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. (alama 4)
- e) Kwa kutolea mifano, eleza jinzi uhuru wa kishairi ulivyo tumiwa kutekeleza arudhi. (alama 6)

#### SEHEMU D : RIWAYA

##### K. Walibora : Kidagaa Kimemwozea

###### Jibu swali la 5 au la 6

- 5. —Naanwalisimuliana kumhusu msichana ambaye alipindua mtazamo wa wengi kuelekewa watu waitwao wale mavu”
  - a) Eleza jinsi msichana anayerejelewa alivyoleta mabadiliko ya mtazamo kuhusu wale mavu. (alama 4)
  - b) Fafanua kwa kutolea mifano mtazamo wa watu kwa wale mavu kabla ya msichana kuleta mapinduzi katika riwaya ya Kidagaa. (alama 6)
  - c) Kwa kutolea mifano, fafanua maudhui ya utengano kama yalivyo jitokeza katika riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 10)
- 6. Eleza migogoro / mivutano inayojidhihirisha katika riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 20)

#### SEHEMU E : FASIHI SIMULIZI

##### 7. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Ndimi Kisoi, dume la ukoo mtukufu

Ulojipambanua kwa mabingwa

Wachezaji hodari wa ngoma

Ndimi dume liloingia nyanjani

Makoo yakatetemeka

Yakang‘ang‘ania gozi kusakata nami

- a) Tambulisha kipera kinachojitokeza katika kifungu hiki. (alama 2)
- b) Eleza sifa tano bainifu za kipera hiki katika fasihi simulizi. (alama 10)
- c) Fafanua umuhimu wa kipera hiki. (alama 8)

#### SEHEMU F : FASIHI SIMULIZI (ALAMA 20)

- 8. a) Taja na ueleze vipera vyta maghani. (alama 10)

- b)** Eleza maana ya miviga.
- c)** Fafanua sifa nne za miviga katika jamii.

(alama 2)  
(alama 8)

for free past papers, visit: [www.freekcsepastpapers.com](http://www.freekcsepastpapers.com)

## **EMBU CLUSTER**

### **MTIHANI WA KIDATO CHA NNE MUHULA WA PILI 2018**

**102/1**

#### **KISWAHILI**

#### **Karatasi ya Kwanza**

1. Mwandikie mhariri wa gazeti la NURU ukielezea kuhusu changamoto zinazowakumba vijana siku hizi.
2. Eleza sababu mbalimbali za ukosefu wa usalama nchini.
3. Mwangata mbili moja humponyoka.
4. Matumizi ya mtandao ya kijamii yameleta madhara kuliko faida.

**102/2**

#### **KISWAHILI**

#### **Karatasi ya Pili**

**Julai / Agosti 2018**

#### **1. UFAHAMU - ALAMA 15**

##### **Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Mara kwa mara masikio yetu yamekaririwa ujumbe kwamba 'kulipa ushuru ni kujitegemea' na ujumbe huu ni ukweli mtupu kwani ni kutokana na ushuru amba wewe na mimi hutozwa unamfanya waziri, mbunge rais na wengine wapate mishahara minono na marupurupu yao.

Fauku ya hayo, ni bidii ya mlipa ushuru ambayo husababisha maendeleo ya taifa na hasa pale ushuru huu unapotumika kwa njia nzuri. Ama kweli wananchi watukufu wa Kenya hususan sisi wanachi wa kawaida, kamwe huwa hatuelewi ni jinsi gani tunakatwa ushuru na jinsi unavyotumiwa. Kwa taarifa yako aliyeajiriwa na asiye na kazi wote hulipa ushuru kupitia kwa mishahara pamwe kupitia bidhaa wanazonunua.

Ingawaje serikali ya Kenya imefanya kila jitihada kuona kwamba kila mwananchi ameubeba msalaba wa kutozwa ushuru inashangaza kuona kwamba kwenye jitihada za kuwavutia wawekezaji wa kigeni, serikali kwa miaka mingi imekuwa ikizondolea kampuni mbalimbali za kigeni ushuru. Kulingana na ripoti ya Action Aid International wakishirikiana na Tax Justice Network Afrika ya mwaka 2012, makadirio ya hivi majuzi ya serikali yanaonyesha Kenya inapoteza shilingi bilioni 100 kila 2012, makadirio ya hivi majuzi ya serikali yanaonyesha Kenya inapoteza shilingi bilioni 100 kila mwaka kutokana na ushuru unaoondolewa kwa wawekezaji wa kigeni.

Hata kama kweli tunawahitaji wawekezaji wa kigeni, ni dhahiri kwamba huenda labda hatuna utaratibu mwafaka wa serikali wa kutambua ni wawekezaji wepi wanafaa kufunguliwa mlango kama huu wa kuondolewa ushuru na ni gani wakunyimwa kibali kama hiki ambacho kwa sasa ni kaa la moto kwenye uchumi wetu hafifu.

Ni kweli kwamba tunawahitaji wawekezaji wa kigeni, lakini ni lazima sisi kama taifa tuweze kujuua kama ni faida tunapata ama ni hasara. Kupitia uchunguzi wangu, nimekuja kutambua kwamba baadhi ya makampuni ya kigeni yakiwemo pia mashirika mengine yasiyokuwa ya kiserikali, yamo kwenye mstari wa mbele wa kutowalipa wafanyakazi wao vyema, huku hata mengine yakiripotiwa kuwadhulumu wafanyakazi wao kwa kutowapa mazingira bora ya kufanya kazi.

Huu bila shaka sitosita kuuita ukoloni mamboleo. Iweje makampuni yapewe idhini ya kuagiza malighafi na mitambo ya kufanya kazi bila kulipia ushuru wowote kwa miaka kumi eti ni kuwavutia wawekezaji huku sisi tunachosalia kupata kama asante ni hasara tupu ya kuukosa ushuru wanaofaa kulipa na ajira za mapato ya kijungu jiko mekonii.

Kutokana na upofu wetu, serikali za Afrika mashariki na kati zimo mbioni zikishindana ni nani atakayeweza kuwashawishi wawekezaji wa kigeni kupitia ondoleo la ushuru. Kumbuka, mbio za sakafuni huishia ukingoni na hilo ndilo viongozi wetu wamesahau kutilia maanani.

Hebu fikiria makampuni ya humu nchini bila shaka sharti yalipe kila aina ya ushuru, uwe ni ushuru wa mapato au wa forodha haya yote yakindeka kwa jina la ujenzi wa taifa. Swalii ni je, wawekezaji wa humu nchini watafaulu vipi ikiwa washindani wao wa kigeni wanapewa kibali cha kufanya biashara bila ya ushuru wowote wa miaka kumi? Kama huu si upofu wa kisera basi ni utepetevu wa wanaosimamia idara na wizara ya fedha.

Kwa ukosefu wa uwazi hasa jinsi ondoleo hili la ushuru linavyofanywa na serikali, limetatiza wananchi kuweza kufuatilia na kujua viwango vya ushuru tunaopoteza. Kwa sasa walimu wako kwenye mgomo, kilio chao kikiwa ni kimoja, mishahara duni huku kwa upande wa serikali ikisisitiza kuwa kamwe serikali haina pesa za kutosha kuwalipa mishahara wanayodai ilhali tunapoteza mabilioni ya fedha.

Kulingana na ripoti ya Action Aid wakishirikiana na Tax Justice Network-Africa, mwaka 2010 - 2011 serikali ilitumia zaidi ya maradufu ya bajeti ya sekta ya afya kwa kuwaondolea ushuru wawekezaji wa kigeni. (tukitumia takwimu za bilioni 100) ikizingatiwa kwamba asilimia 46 ya wakenya milioni 40 wanaishi katika hali ya uchochole (chini ya dola 1.25 kwa siku) suluhu.

Kabla ya serikali kuziondolea kampuni za ugaibuni ushuru, kuna haja ya kutadhamini iwapo awekezaji wanatupa faida au wanatuletea hasara tupu, la sivyo tutabaki kujichimbia kaburi lenye kina kirefu la umaskini tutakalotumbukia na kusahaulika milele. Mwenye macho haambiwi tazama.

### **MASWALI.**

- a) Taja manufaa yoyote matatu ya kulipa ushuru kwa mujibu ya makala haya. (alama 3)
- b) Kulingana na mwandishi, kwa nini makampuni ya kigeni hayatoshi ushuru? (alama 1)
- c) Eleza madhara yanayotokana na kutotoza makampuni ya kigeni ushuru. (alama 3)
- d) Makampuni ya humu nchini yanadhulumiwa na serikali inayopaswa kuyalinda. Thibitisha. (alama 2)
- e) Mwandishi wa makala haya anapendekeza suluhisho gani kuhusu tatizo hili la ushuru. (alama 2)
- f) Taja mashirika yanayotafiti na kutoa ripoti kuhusu maswala ya ushuru. (alama 1)
- g) Eleza matumizi ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika makala. (alama 3)
  - i) marupurupu
  - ii) malighafi
  - iii) utepetevu

## **2. UFUPISHO - (Alama 15)**

### **Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Miongoni mwa mbinu za kufanya utafiti katika fasihi simulizi matumizi ya hojaji. Hojaji ni orodha ya maswali ambayo hutungwa na mtafiti wa fasihi na kuyatumia katika kupata data muhimu kuhusiana na utafiti anaofanya.

Hojaji zinazotumika zaidi katika utafiti wa fasihi simulizi ni za aina mbili, Hojaji fungo na hojaji wazi. Hojaji fungo, kama jina linavyodokeza, huwa na maswali ambayo mtafiti huyatunga hivi kwamba anayehojiwa (mhojiwa) hujifuga kwa kujibu maswali ambayo ameulizwa tu. Katika hojaji fungo, mhojiwa hatoi maelezo marefu. Mfano wa swali ambalo linaweza kupatikana katika hojaji fungo ni: Hadithi inaweza kuwa methali, na hadithi huibua wimbo. Ndiyo au la. Kwa upande mwingine, hojaji wazi, huwa ni maswali yanayompa mhojiwa nafasi ya kutoa maelezo ya kina kuhusu suala linalohusika.

Mfano wa swali ambalo linaweza kuwa katika hojaji wazi ni :- Taja methali zinazopatikana katika jamii ya wakamba.

Kabla ya mtafiti wa fasihi simulizi kuandaa hojaji sharti azingatie baadhi ya kanuni za kimsingi. Kwa mfano, ajiulize. Malengo ya utafiti ni yapi? Ni utanze upi wa fasihi simulizi unaofanyiwa utafiti?

Je, wahojiwa wana ujuzi upi wa fasihi simulizi unaofanyiwa utafiti? Je, wahojiwa ni wa kiwango kipi cha elimu? Wahojiwa wana ujuzi upi kuhusu kipera husika? Utafiti unaofanywa ni wa kiwango kipi?

Ni muhimu kwa mtafiti kufanya hojaji yake majaribio kabla ya kuisambaza kwa wahojiwa wote katika eneo linalohusika

Ni muhimu kuifanya hojaji jaribio hili ili kupima uwezo wake wa kupata data inayotarajiwa.

Mbinu ya hojaji katika utafiti wa fasihi zimulizi, kama mbinu yoyote, huwa na manufaa na upungufu wake. Faida kuu ya hojaji kama mbinu ya utafiti katika fasihi simulizi ni kuwa mtafiti anaweza kushughulikia eneo pana kijiografia, hasa ikiwa wakafitiwa ni wengi kwa muda mfupi. Hii pia hupunguza gharama ya utafiti, ikizingatiwa kuwa kikwazo kikubwa katika utafiti wa fasihi simulizi ni gharama kubwa.

Pia, wahojiwa hujaza hojaji kadri ya uwezo wao na kisha kumrejeshea mtafiti hojaji hizo. Kwa kawaida mara nyingi mtafiti huwatumiwa wahojiwa hojaji, zikiwa na stampu. Hivyo basi, hakuna gharama kwa mhojiwa anapomrejeshea mtafiti hojaji zilizojazwa.

Hojaji ni mbinu mwafaka ya utafiti wa fasihi simulizi, hasa wakati mtafiti anachunguza mada nyeti katika jamii.

Mbinu ya hojaji huhakikisha kuwa siri ya mhojiwa imehifadhiwa na pia majibu yanayotolewa hutumiwa kwa minajili ya utafiti peke. Mbinu hii hutumika kwa wahojiwa ambao wanaweza kusoma na kuandika.

Mbinu hii ni mwafaka kwa maswali ambayo ni sahili na wazi. Maswali changamano yanaweza kujibiwa kuititia mbinu zingine za utafiti kama vile mahojiano ya ana kwa ana.

Licha ya faida za hojaji, kama vile mbinu ya utafiti wa fasihi simulizi, mbinu hii ina udhaifu wake, kwanza, mbinu hii haiwezi kutekelezwa kwa wahojiwa ambao hawajui kusoma na kuandika. Huu ni upungufu mkubwa ikikumbukwa kuwa fanani wengi wa fasihi simulizi ya kiafrika ni wasiojua kusoma na kuandika.

Pia, mbinu ya hojaji, ina udhaifu hasa kwa maswali ambayo ni changamano. Udhaifu huu unatokea pale mhojiwa hawezo tulifasiri swali ipasavyo na wakati huo hana mtafiti ili amfanulie kama iliyyo kwa mbinu ya mahojiano ya ana kwa ana. Data inayopatikana si ya kuaminika kama ile ya mahojiano ya ana kwa ana.

Katika hojaji, mtafiti hawezi kuchunguza hisia za mhojiwa. Licha ya upungufu wa hojaji, ni mbinu muhimu ya utafiti wa fasihi simulizi. Mtafiti anaweza kuitumia pale inapohitajika ili kupata data yake.

Maswali.

- a) Fupishaaya za kwanza NNE. (alama 4)
- b) Eleza udhaifu wa hojaji kama mbinu ya utafiti wa fasihi simulizi. (alama 9)
- 3. MATUMIZI YA LUGHA.**
- a) Taja konsonanti mbili ambazo ni Irabu. (alama 2)
- b) Eleza tofauti baina ya mofimu huru na mofimu tegemezi. (alama 2)
- c) Andika sifa mbili za kitenzi kishirikishi kikamilifu. (alama 2)
- d) Taja aina mbili za vihusishi. (alama 2)
- e) Fafanua matumizi mawili ya ITALIKI kama alama ya uakifishaji. (alama 2)
- f) Tunga sentensi mbili zinazoanza kwa (alama 2)
  - i) Kiambishi nafsi huru
  - ii) Kiambishi nafsi kiambata
- g) Iandike sentensi ifuatayo katika kinyume (alama 2)  
Shangazi wengi walizama baharini jana asubuhi.

- h) Tambua jinsi neno wengi limetumika katika sentensi hii. (alama 2)  
Wengi wamekaribishwa katika sherehe hizo.
- i) Tunga sentensi kudhihirisha aina tatu za yambwa (alama 3)
- j) Iandike sentensi hii katika usemi wa taarifa. (alama 4)  
"Ninataka kumwona mwanafunzi aliyehusika katika sakata hii sasa hivi."
- k) Ichanganue sentensi ifauatayo kwa vistari. (alama 4)
- Wale watatu watapelekwa hospitalini kesho
- l) Tunga sentensi moja kudhihirisha maana mbili tofauti za neno **kaa**. (alama 2)
- m) Yakinisha (alama 2)  
Hasikii la mwadhini wala la mteka maji.
- n) Eleza tofauti baina ya sentensi ambatano na sentensi changamano. (alamaa 2)
- o) Tunga sentensi kuonyesha **ki** ya msharti. (alama 1)
- p) Ainisha  
Alitufia
- r) Tofautisha dhana zifuatazo. (alama 3)  
i) Kirai  
ii) Kishazi
- s) Tunga sentensi ukitumia a - unganifu. (alama 1)

#### **ISIMU JAMII**

- a) Eleza sababu zinazochangia kuzuka kwa lahaja. (alama 5)
- b) Taja na uleze mambo yoyote matano yaliyochangia maendeleo ya Kiswahili nchini Kenya baada ya uhuru (alama 5)

**SEHEMU A (SWALI LA LAZIMA)**

**A : USHAIRI.** Soma ushairi ufuatao kisha ujibu maswali.

Ulimwengu ulimwengu, ulimwengu naratibu  
 Yaliyo kichwani mwangu, nataka kuyahutubu  
 Wayasome ndu zangu, wa mbali na wa karibu  
 Cha wenyе raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ulimwengu ni kiwanja, cha wenyе raha na tabu  
 Wengine wanajikonja, kwa wengine ni adhabu  
 Kucha na kutwa twahanja, kutafuta matulubu  
 Cha wenyе raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa balaa, aliniusia babu  
 Mna mambo yamejaa, ya faraja na kusibu  
 Na machache ya kufaa, ila mengi ya udubu  
 Cha weye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni kiwanja cha Amina, Saidi Ali Rajabu.  
 Wengine kitu hatuna, tunaishia kababu  
 Wale wamejaza sana, wanashindwa kuhesabu  
 Cha wenyе raha na tabu, Ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa urongo, na kweli pia ajabu  
 Kichwa hudanganya shingo,tumbo kiuno chasibu  
 Usitumai ubongo, wa nduguyo na swahibu  
 Cha wenyе raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa walevi, pombe kwao ni dhahabu  
 Mara vile mara hivi, wakilewa majudhubu  
 Maneno ya kiujuvi, hujipaka hata shabu  
 Cha wenyе raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni kiwanja wenyе dini, wamtio wahabu  
 Mashekhe msikitini, humo humfanya muhibu  
 Mapadiri kanisani, huvihubiri vitabu  
 Cha wenyе raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja

Ni uwanja wa malofa, lofa mtu mwenye tabu  
 Kusema sana kashifa, na moyo kisebusebu  
 Tunakaribia kuja, kwa kushidwa kujimudu  
 Cha wenyе raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa faraja, alowajali habibu  
 Na wengine sitotaja, msinambe ninagubu  
 Ni uwanja wa viroja, vigumu kuvikutubu  
 Cha wenyе raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

**Maswali:**

- (a) Lipe shairi hili anwani ifaayo. (al.1)  
 (b) Kwa kutoa mfano, eleza mbinu zozote mbili za lugha zilizotumika katika shairi. (al.2)  
 (c) Eleza jinsi uhuru wa mshairi ulivytumika katika shairi. (al.2)  
 (d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha tutumbi. (al.4)  
 (e) Taja na ueleze bahari zozote mbili zilizotumika katika shairi hili. (al.2)  
 (f) Eleza umbo la shairi hili. (al.4)  
 (g) Eleza toni ya shairi hili. (al.1)  
 (h) Fafanua dhamira ya mshairi. (al.2)  
 (i) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivytumika katika shairi. (al.2)  
     (i) Malofa  
     (ii) Udubu

**SEHEMU B.****TAMTHILIA****KIGOGO – JIBU SWALI LA 2 AU 3.**

2. —Kitabu si jalada, fungua ndani usome mambo. Kitanda usichokilalia kunguni wake huwajui.”  
     (i) Eleza muktadha wa dondo hili. (al.4)  
     (ii) Kwa kurejelea tamthilia ya kigogo, thibitisha ukweli wa dondo hili. (al.14)  
     (ii) Taja tamathali za usemi zilizotumika katika dondo hili. (al.2)  
 3. Eleza mbinu alizotumia majoka kuendeleza uongozi wake. (al.20)

**SEHEMU C:****RIWAYA – KIDAGAA KIMEMWOZEA****Jibu swali la 4 au 5.**

4. —W bwana unafikiri ninatumia petroli nini?”  
     (a) Weka maneno haya katika muktadha wake. (al.4)  
     (b) Eleza sifa nne za msemewa. (al.4)  
     (c) Fafanua jinsi mwandishi wa kidagaakimemwozera amewasawiri wanawake. (al.12)  
 5. Jadili jinsi mbinu zifuatazo zimetumiwa na mwandishi kufanikisha kazi yake.  
     (i) Sadfa (al.20)  
     (ii) Mbinu rejeshi.

**SEHEMU D****HADITHI FUPI.****TUMBO LISILOSHIBA.**

6. Huku ukirejelea hadithi ya Tumbo Lisiloshiba na Shibe Inatumaliza, fafanua maudhui ya ukiukaji wa haki. (al.20)

**SEHEMU E.****FASIHI SIMULIZI – JIBU SWALI LA 7 AU 8.**

7. (a) Eleza maana ya miviga. (al.2)  
     (b) Fafanua sifa za miviga. (al.4)  
     (c) Eleza udhaifu wa miviga. (al.2)  
     (d) Toa maana ya ulumbi. (al.2)  
     (e) Ni nini umuhimu wa ulumbi . (al.8)
8. **SOMA KIFUNGU KIFUATACHO KISHA UJIBU MASWALI.**

1. Ndugu !  
Umeenda?  
Wewe nenda  
Wewe nenda  
Wewe nenda  
Mungu atakutunza
  
2. Wewe Safiri  
Wewe safari  
Wewe safari  
Maisha ni moshi  
Hata si tu safarini.
  
3. Ndugu!  
Tulikupenda  
Tulikupenda  
Tulikupenda  
Na Maulana kakupenda zaidi
  
4. Oooh!  
Ndugu  
Wewe nenda  
Wewe nenda  
Wewe nenda  
Siku yetu ikifika  
Tutapaa ka malaika  
Mungu akurehemu.

**Maswali .**

- (a) Huu ni utungo wa aina gani. (al.2)
- (b) Fafanua sifa bainifu za utungo huu. (al.8)
- (c) Tambua tamathali za usemi zilizotumika katika utungo huu. (al.4)
- (d) Ni vipi utungo kama huu ni muhimu katika jamii. (al.6)

- Hufariji waliofiwa.
  - Ni njia ya kutakasa moyo na hisia za aliyefiwa.
  - Huendeleza utamaduni wa jamii husika.
  - Huelimisha kuhusu mila na itikadi.
  - Huwapa wanajamii matumaini.
  - Huleta utangamano.
- (6x1=6)

## **COMPLIANT I**

**102/1**

### **KISWAHILI**

#### **KARATASI YA 1**

##### **INSHA**

###### **1. Inshayalazima**

- Andikaresipekuhusujinsiyakutayarishakitoweo cha nyama.
2. Matatizoyaokifamiliayamezidikitakjamii. Elezakinachosababishamizozohiikasha uelezehatuazifaazokuchukulialikutatuatatzohili.
  3. Mhininamhiniwanjiayaonimoja
  4. Andikainshaitakayomalizikiakwa:  
..... nilipoionapaa la nyumbayetunilishushapumzi, nilishukuru. Kwakwelihyo safari haikuwarahisikwangu.

**102/2**

### **KISWAHILI: LUGHA**

**(Ufahamu, Ufupisho, MatumiziyaLughanaIsimuJamii)**

#### **KARATASI YA 2**

### **UFAHAMU**

###### **1. Soma makalayaafuatayo kasha ujibumaswali:**

Shuleyabweniyawasichanaya Askofu Timotheokwakawa idailikuwanautilivuwaajabu.

Wasichanawalitarajiwakuendelezashughulizaokwutilivunausta rabuhukuwakizingatiamaadiliyahaliyajuu. Hatahivyo, asubuhiihiyaijumaahaliilikuwatofauti. Nafasiyatulivuwakawa idaulichukuliwanamzowashughuli.

Hiilikuwasakiuyakipekeenamsisimkouljaaka tikan yoyozawanafunzi. Ilikuwasakiuyatamashazamuzikina drama zashulezaeneo la mlimani.

Mwendowasaannemabasiyashulen geniyalyalikuwayameanzakuingiahukuyaki endeleakutapikawanafunziwa kike nakiumewakiandamananawalimuwao. Mara tubaadayakufika, waliteremsha, kutokamagariyao, vifaavyaovilivyohitajikakatikatamashanakuvi pelekakatikaukumbimkuuambamomashindanoyangefanyika.

Alazamuzikizakilanuinamalebayawaigizaji, vyotevilipelekwa ukumbini.

Si wotewaliofikakatikashuleyabweniyawasichanaya Askofu Timotheowalikuwas hirikiwatamasha.

Wengiwalifikakushangili amakundiyo. Mi ong onimwawaliofikakufanyahivyo alikuwa Chris Masazu, mwanafunzi washuleyawavulanaya Lengajuu.

Yeyenawanafunzi wengine wakiumewalizurukilasehemuyashulehiingenikuridhisha macho yao. Hawakuridhisha macho tu, balipiawalichezamichezoyau janaamawakijua au kutojuau waujanaunate gemo. Vijnakanamahaowalionamikutanoyashulen yingikuwa fursaya kee yakuachakumbukumbuyazi arahusika.

Masazualipendasanamichezohiyona alikuwa amewe kashabahaya keyasiku.

### **MASWALI**

- |   |          |
|---|----------|
| (a) Toa Kichwamwafakakwamakalahaya  | (alama1) |
| (b) Elezanikwaninikatikashuleza Askofu Timotheoutulivuwakawa idauliko sekanasiku inayorejele wahadithini. | (alama4) |
| (c) Je, kunamadharaganijaku andamananawana funzimichezoniamba o hawatashiriki haikwenyemichezo.           | (alama4) |
| (d) Ni ninikinachodhihirishakuwa Chris Masazunimto uwanidhamu.  | (alama4) |

- (e) Eleza maana kulingana na kifungu ya:  
 (i) Mzowa shughuli (alama2)  
 (ii) Kutapika wanafunzi wa kike nakiume. (alama2)

## 2. UFUPISHO

### **Soma makalayafuatayo kasha ujibumaswali:**

Mitihani imetumiwa siku nyingi kama kigezo cha kupima werevu wa mwanafunzi katika kutekeleza majukumu ya kiakili yenyeye kuhitaji stadi mbalimbali. Hii ni njia yakuaminika na ni rahisi ambayo imetumiwa miaka mingi na watahini kukadiria uwezowa mtu. Lakini wale wanaopinga mitihani wanasema kuwa mitihani haipimi kwa njia inayoaminika uwezo wakiakili wa mwanafunzi, badala yake, mitihani inakadiria tu uwezo wa mwanafunzi, wakukadiria mambo kama kasuku kwa muda mfupi ulioja vitisho na shinikizo.

Wasioithamini mitihani pia wanadai kuwa mitihani humpa mtahiniwa wasiwasi mwingu. Hii ni kwa sababu hadhi na umuhimu wa mitihani imekuzwa sana mionganoni mwa watahiniwa najamii nzima kwa jumla. Mitihani ndio kigezo pekee kinachokadiria kufaulu au kutofaulu kwa mwanafunzi. Mustakabali wa mwanafunzi kuamuliwa n amtihani. Watahini hawajali sana masuala mengine ambayo yanawezakuathiri jinsi mwanafunzi anavyoweza kuufanya mtihani. Kwa mfano, mtahiniwa anaweza kuwa mgonjwa, au pengine hakulala vizuri siku iliyotangulia mtihani. Haya yote ni masuala yanayoweza kumfanya mtahiniwa kutofanya vizuri katika mtihani.

Elimu nzuri humfundisha mwanafunzi kutumia akili. Lakini mfumo wa elimu unaopendelea mitihani haufanyi hivyo. Mfumo wa aina hiyo husisitiza kufundisha yaleyale yanayopatikana katika mwongozo uliotolewa tu. Mwanafunzi hapewi motisha ilikusoma kwa mapana marefu ili kupanua akili yake. Badala yake mwanafunzi hufungiwa kwenye uwanja finyu ambamo haruhusiwi kutoka. Mwalimu naye kadhalika hana uhuru wakumfundisha mwanafunzi kile anachofikiria kuwa muhimu katika maisha. Badala yake jukumu kubwa analoachiwa mwalimu huwa nikumpa mwanafunzi mbinu za kujibu maswali na kupita mtihani.

Ingawa wanaoitetea mitihani hudai kuwa matokeo ya mitihani niya kuaminika kwasababu husahihishwa na watu wasio wajua watahiniwa, lakini ni vizuri pia kukumbuka kuwa watahini ni binadamu tu. Binadamu huchoka, huhisi njaana zaidi ya yote anaweza kufanya makosa. Licha ya hayo yote, watahini hutakiwa kusahihisha rundo kumbwa la karatasi, kwa muda mfupi. Mjadala uliopo kati ya wanaopendelea mitihani na wale wasiopendelea watukumbusha kuwa kuna haja kubwa ya kuendeleza kuboresha mfumo wa mitihani ili uweze kukadiria kwayakini uwezo wa kiakili wa mtahiniwa.

- a) Fupisha aya ya kwanza na ya pili. (maneno 60)  
 b) Fupisha aya ya tatu na yanne. (maneno 50)

### **3. MATUMIZI YA LUGHA**

- a) Bainisha aina ya vivumishi katika sentensi hii. (alama2)  
 Kazi hii itaondoa matatizo mengi.
- b) Eleza tofauti baina ya sentensi hizi.  
 i) Aliugua vibaya  
 ii) Aliungua vibaya (alama2)
- c) Andika kwa wingi  
 i) Haramia huyo alimpora mlemavu.  
 ii) Mfua chuma alitengeneza zana ya vita. (alama2)
- d) Andika katika ukubwa (alamas2)  
 i) Neno hilo halimo katika kitabu  
 ii) Pakua ugali katika sahanı
- e) Tambulisha kielezi, kivumishi na mnyambuliko wa kitenzi katika sentensi ifuatayo. Msichana mrembo alikuja upesi akinikimbilia dadake. (alama3)

- f)** Eleza maana yamisemo ifuatayo. (alama2)  
 i) Piga ramli  
 ii) Daka maneno
- g)** Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia visanduku. Twiga hukimbia mbio ingawa ni mrefu. (alama3)
- h)** Andika sentensi hii upya kwa kufuata maagizo Nilikuwa nimejitayarisha vizuri kwa hivyo sikuona ugumu wowote katika safari yangu. (alama3)  
 Anza: Safari .....
- i)** Andika kinyume cha senten sihii. Amejitwika mtungi wa maji. (alama1)
- j)** Unda majina mawili kutokana na maneno ya fuatayo. (alama2)  
 i) Chora.....  
 ii) La .....
- k)** Kanusha sentensi zifuatazo. (alama2)  
 i) Nikisomeshwa Kiswahili nitaelewa.  
 ii) Nikipika chakula, mama hufurahia.
- l)** Tunga sentensi kuonyesha maana mbili za neon otea. (alama2)
- m)** Ainisha mofimu katika fungi-tenzi hili. Ameshinda (alama2)
- n)** Yakinisha (alama2)  
 i) Siji  
 ii) Halali
- o)** Tunga aina za sentensi zifuatazo. (alama3)  
 i) Sahili  
 ii) Ambatano  
 iii) Changamano
- p)** Andika katika usemi halisi Nyumba hiyo ingejengwa vyema isingebomoka. (alama2)
- q)** Tunga sentensi kubainisha matumizi yafuatayo ya “ki” (alama2)  
 (a) Masharti  
 (b) Kitendo, kuendeleza kwa muda
- r)** Tumia mzizi – zea katika sentensi kama (alama2)  
 i) Nomino  
 ii) Kivumishi
- s)** Eleza maana ya: (alama2)  
 i) Ugonezi  
 ii) Sapa

#### 4. ISIMU JAMII

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

- MWALI: Sidhani budaa taniwahi hiyo cargo. Siku hizi amekuwa muhard sana na fulusi.
- KIMATA: We nawe Maxe sikuzote chapa. Kwani umeanzisha factory yamafegi naona kinywa hakiishi kufusha misteam.
- MWALI: Sikiliza bratha. Mimi sitaki mizomo. Unaanza kuleta noma. Masaa kikusikiaanze kuleta drama zakeza twenty four seven. Utakujakuni.....
- KIMATA: Shii! Ndohuyo dad. Nenda kajaribu lock yao. Huenda akakulisten. Mimi nilimwambia aningetie chapa ya kwenda kudufu akanishow hana.

MWALI: Acha basi nijaribu japo sina hope. Juzi alianza kunitolea mapreaching yake ya every day(akiiga).—Mwanangu, nimuhimu kusoma kwa bidii ili uweze kujitegemea.Kumbuka mtegemea cha nduguye hufa maskini.”

- a) Taja muktadha wa mazungumzo haya. (alama2)
- b) Andika sifa tatu za lugha inayohusika katika mazungumzo haya. (alama3)
- c) Fafanua sababu zinazopelekea watu kubadili na kuchanganya msimbo/ ndimi. (alama5)

for free past papers, visit: [www.freekcsepastpapers.com](http://www.freekcsepastpapers.com)

**KISWAHILI****KARATASI YA 3****FASIHI****1. SEHEMU YA A: RIWAYA****KIDAGAA KIMEMWOZEA-KEN WALIBORA**

- i) Amani ni kielelezo cha vijana waliowajibika katika jamii. Thibitisha kauli hii. (alama10)  
 ii) Onyesha matumizi ya taaswira katika Kidagaa Kimemwozea. (alama10)

**2 SEHEMU YA B: TAMTHILIA****KIGOGO-PAULINEKEA**

Majoka alitumia mbinu mbalimbali ili kuudumisha utawala wake dhalimu.Thibitisha kauli hii. (alama 20)

**SEHEMU C:****TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE**

3. Alijua kwamba ingawa sahau imejipenyeza ndaniya maisha ya kila mtu, utashi wa wakubwa haujazimika kamwe. Ulikuwa tu ukivukutika ndani kwanda ni kama moto wa makumbi...‘  
 a) Eleza muktadha wa nukuu hii (alama 4)  
 b) Fafanua mbinu nne kutoka kwa nukuu (alama 4)  
 c) Andika sifa nne za anayerejelewa (alama 4)  
 d) Wana madongo poromoka wanakumbana na matatizo mengi si haba, fafanua (alama 8)

**AU****HADITHI YA KIFAUURONGO**

4. a) Eleza maudhui sita kutokana na hadithi hii (alama 12)  
 b) Fafanua sifa nne nne za wahusika hawa. (alama 8)  
 i) Dennis  
 ii) Penina

**5. SEHEMU YA D: USHAIRI**

Soma shairilifuatalokishaujibumaswali.

Iweje

Kwa  
 Niniwakulimasasa  
 Wanalima                  ofisini  
 Kwa:

Simu,  
 Kalamu  
 na kauli  
 Kuvuna  
 Ukwasi,  
 na wafiao  
 juani  
 kupata

Kitone

**Maswali**

- a) Thibitisha yakuwa hili ni shairi huru (alama3)  
 b) Taja maudhui manne kutoka kwa shairi hili (alama4)

- c) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili. (alama3)
- d) Fafanua mbinu aliyotumia mwandishi iliapate umbo la shairi hili. (alama4)
- e) Taja mbinu zingine mbili zilizotumi kakatika shairi. (alama2)
- f) Fafanua maana ya
  - (i) Na wafiao Juani
  - (ii) Kuvuna ukwasi(alama2)

**6. SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

- (a) Eleza maana ya misimu.
- (b) Taja nauitolee mifano miwilimiwili aina mbalimbali za misimu. (alama8)
- (c) Fafanua jukumu la misimu mionganoni mwa mwanajamii. (alama10)

for free past papers, visit: [www.freekcsepastpapers.com](http://www.freekcsepastpapers.com)

## **COMPLIANT II**

**102/1**

### **KISWAHLI**

#### **KARATASI YA 1**

#### **INSHA**

1. Kumekuwa na ongezeko la migomo ya wafanyakazi nchini katika siku za hivi karibuni. Wewe ni katibu wa tume iliyobuniwa na rais kusimamia suala hili. Andika ripoti
2. Ufisadi umechangia pakubwa kuwepo kwa maendeleo duni nchini. Jadili.
3. Andika insha inayoafikiana na methali Baniani mbaya kiatu chake dawa.
4. Andika insha itakayomalizikia kwa;  
...walipofungua mlango huo hatimaye, wengi hawakuweza kuzuia hisia zao. Waliangua vilio kwa maafa waliyoshuhudia.

**102/2**

### **KISWAHLI: LUGHA**

**(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya Lugha na Isimu Jamii)**

#### **KARATASI YA 2**

##### **A. UFAHAMU: (Alama 15)**

##### **Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Tokea muundo mpya wa serikali ya ugatuvi uanze kutekelezwa miaka miwili iliyopita, kumeendalea kushuhudiwa matatizo mengi hali iliyopelekea kushuhudiwa kwa msururi wa migomo na maandamano ya raia. Fujo za karibuni kabisa ni zile zinazoshuhudiwa katika mijji mikubwa za wachuuzi na wafanyibiaashara wakipinga hatua za serikali za kaunti kuwatoza ushuru takribani kwa kila huduma na bidhaa ikiwemo wanyama, kuku na ndege. La kuhuzunisha zaidi katika baadhi ya majimbo imeripotiwa kuwa raia wamelazimishwa kulipa ushuru kwa kutaka tu kuona maiti za jamaa zao kwenye vyumba vya kuhifadhiya maiti!

Wanasasa wameonekana kuwa na wakati mgumu kutetea mfumo huu mpya wa ugatuvi huku baadhi wakisema kwamba matatizo yanayoshuhudiwa kwa sasa yametokana na ugeni wa mfumo huo. Wengine wameinyoshea kidole serikali ya kitaifa kwamba ndiyo inayosambaratisha muundo huu. Wengine wanahoji kuwa bado ni mapema na kwamba kunatajika muda mrefu ili kufaulu

Ni wazi kwamba kumekosekana nidhamu bora ya kusimamia maisha ya raia nchini Kenya. Matatizo yanayokumba raia kwa sasa ni dalili kuwa mfumo wa serikali ya ugatuvi umeongeza chumvi kwenye kidonda badala ya kutibu. Swali ni je, hadi limi nidhamu ya kusimamia raia itakuwa ni suala la majaribio na makosa?

Hatua ya kuwarundikizia raia ushuru mkubwa ni kitendo cha unyonyaji na cha dhuluma kinachofaa kupingwa. La kufahamishwa hapa ni kwamba ushuru ndio njia kubwa ya kuzalisha mapato ya serikali zinazojifunga na mfumo wa kimagharibi wa kiuchumi wa kibepari ikiwemo Kenya. Asilimia 90 ya mapato ya serikali za kibepari huegemea ushuru. Kwa hivyo hatua ya serikali za kaunti katika kuwanyonya raia kwa kuwalipisha ushuru si ajabu bali ni thibitisho kuwa jamii ya Kenya inaongozwa na nidhamu ya kiuchumi ya ubepari mfumo wa unyonyaji na ukandamizaji. Ukweli unabakia kuwa ndani ya serikali za kibepari raia ndio hubebeshwa mzigo wa ushuru unaoishia matumboni mwa viongozi!

Miito ya mabadiliko ya katiba na ya miundo mipyä ya kiutawala si lolote ila ni moja tu ya hatua za mfumo wa kibepari kujipa muda wa kuishi na kuziba aibu zake za kushindwa kusimimia maisha ya watu. Kufeli huku kwa mfumo huu kunashuhudiwa hadi kwenye nchi kubwa za kibepari kama Marekani na Uingereza hivyo nazo zimekumbwa tele na maandamano na fujo za raia wakilalamikia hali ngumu ya maisha.

##### **Maswali**

- a) Yape makala haya anwani mwafaka. (alama 1)
- b) Eleza mtazamo wa wanasiwa kuhusu utepetevu wa mfumo huu. (alama 3)
- Utuvi nchini Kenya ni mfumo wa kibepari” Thibitisha kauli hii kwa kurejelea makala (alama 3)

- c) Migomo ni zao la matatizo yaliyogatuliwa kutoka serikali kuu. Toa sababu nyingine zinazosababisha migomo katika serikali za ugatuza (alama 4)
- d) Thibitisha jinsi mfumo wa ugatuza umeongeza chumvi kwenye kidonda badala ya kutibu (alama2)
- e) Eleza maana ya maneno yafuatayo (alama 2)
  - (i) Ugatuza
  - (ii) Kibepari

## B. UFUPISHO (Alama 15)

### Soma makala yafuatayo na ujibu maswali.

Mojawapo kati ya misingi na nguzo za maendeleo ulimwenguni ni viwanda. Viwanda ni muhimu kwa kuwa ndivyo vinavyoigeuza malghafi yanayopatikana na kuwa bidhaa zinazoweza kutumiwa na watu. Katika nchi zinazoendelea, ambazo hazina uwezo mkubwa wa mitaji, viwanda vinavyoimarika ni vile vidogo. Hivi ni viwanda ambavyo huhusisha amali za mikono. Kuimarika kwa viwanda hivi vidogo kunatokana na sababu mbalimbali.

Nchi zinazoendelea huwa na masoko finyu hasa kwa kuzingatia uwezo wa ununuzi wa wanaolengwa na bidhaa za viwanda. Katika misingi huu, viwanda vikubwa vitawiwa vigumu kufanya biashara katika mazingira ambako masoko yake ni finyu au utashi wa bidhaa zake sio mkubwa. Viwanda vidogo pia vina uwezo wa kuwaajiri wafanyakazi wengi hasa kwa kuwa havina uwezo wa kugharamia mashine.Uajiri huu wa wafanyakazi wengi ni muhimu katika maeneo mengi ambako tatizo la uajiri ni mojawapo wa matatizo sugu. Tofauti na mataifa ya kitasnia, mataifa yanayoendelea hayana mifumo imara ya kuwakimu watu wasiokuwa na kazi. Utegemezi wa jamaa wanaofanya kazi kwa hivyo unakuwa nyenzo ya pekee ya kuyamudu maisha.

Kuanzisha viwanda vidogo hakuhitaji mtaji mkubwa tofauti na viwanda vikubwa. Hali hii inasahilisha uwezekano wa watu wengi kujasurisha shughuli yoyote ile. Sambamba na suala hili ni kuwa ni rahisi kujaribisha bidhaa mpya kwa kiwango kidogo cha kiwanda kidogo. Ikiwa mzalishaji ye yoyote atazalisha bidhaa mpya kwa mapana, kwa mfano kama ilivyo kwa viwanda vikubwa, pana uwezekano wa kupata hasara kubwa. Huenda utashi wa bidhaa hizo uwe mdogo ukilinganishwa na ugavi wa bidhaa zenye.

Majaribio mazuri huwa ni kwa kiwango kidogo. Kuwepo kwa viwanda vidogo huwa ni chocheo kubwa la usambazaji wa viwanda hadi maeneo ya mashambani. Hali hii inahakikisha kuwa nafasi za ajira zimesambazwa nchini hali ambayo inasadidua kuhakikisha kuwa pana mweneo mzuri wa kimapato nchini. Mweneo huu wa mapato unachangia katika kuboresha uwezo wa kuununuzi wa umma. Huu ni misingi muhimu wa maendeleo. Upanuzi na ueneaji wa viwanda vidogo vidogo ni misingi mkubwa wa kujitegemea kiuchumi. Aghalabu viwanda vikubwa huegemea kwenye mitaji ya mashirika ya kimataifa na huwa misingi wa kuendelezwa kwa utegemezi wa kiuchumi.

Licha ya faida zake, ueneaji au kutanda kwa viwanda hukabiliwa na matatizo mbalimbali. Tatizo la kwanza linahusiana na mtaji. Lazima pawepo na mbinu nzuri za kuweka akiba ili kuwa na mtaji wa kuanzishia biashara. Njia mojawapo ya kufanya hivi ni kwa kutegegemea masoko ya mitaji ambayo katika mataifa mengi hayajaendelezwa vyema. Inakuwa vigumu katika hali hii basi kupata pesa kwa uuzaaji wa hisia kwenye masoko hayo.

Tatizo jingine linalotokana na ukosefu wa mikopo ya muda mrefu ya kibiashara kwa wenyewe viwanda vidogo. Mikopo ya aina hii huwa muhimu hasa pale ambapo anayehusika ana mradi wa kununua vifaa kama mashine. Mikopo ya muda mfupi inayopatikana kwenye mabenki huweza kuwashinda wengi kutokana na viwango vya riba kuwa juu. Haimkiniki kwa viwanda kama hivi kukopa kutoka nje ya nchi zao. Juhudi za kuendeleza viwanda hivi huweza pia kukwamizwa na tatizo la kawi kama vile umeme. Gharama za umeme huenda ziwe juu sana. Isitoshe, si maeneo yote ambayo yana umeme. Matatizo mengine huhusiana na ukosefu wa maarifa ya kibiashara, ukosefu wa stadi za ujasiriamali au kuwa na ujasiri wa kuijiingiza kwenye shughuli Fulani na miundo duni.

Ili kuhakikisha kuwa viwanda vimekuzwa na kuendelezwa pana haja ya kuchukua hatua kadha. Kwanza, kuwepo na vihamasisho kwa wanaoanzisha viwanda vidogo vidogo kama vile punguzo la kodi, kuhimiza kuanzishwa kwa viwanda vidogo vidogo na kusaka kuyapanua masoko kwa ajili ya bidhaa zinazozalishwa na viwanda hivyo. Aidha kuanzishwa na kupanuliwa kwa taasisi za kuendeleza upanuzi huo. Pana haja ya kuwekeza kwenye rasilimali za kibinadamu; kuelimishwa na kupanua uwezo wao wa kuyaelewa mambo mbalimbali. Miundo misingi haina budi nayo

kupanuliwa na kuimashwa. Upo umuhimu pia wa kuongeza kasima inayotengewa maendeleo na ukuzaji wa viwanda ili kuharakisha maendeleo yake pana umuhimu wa kupambana na ufisadi unaoweza kuwa kikwazo kikubwa. Inahalisi kutambua ikiwa viwanda vitatanda nchini, uchumi wa nchi nao utawanda.

- (a) Kwa **maneno 65-75**, eleza ujumbe muhimu unaopatikana katika aya ya pili hadi ya nne.

(alama 8,1 utiririko)

- (b) Kwa **maneno (50-55)** fafanua mambo yanayotinga ukuaji wa viwanda.

(alama 5, 1 utiririko)

### C. MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)

- a) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa  
Nyuso za vijana wale zilichujuka walipoanguka (alama 2)
- b) Tumia **KI** katika sentensi kuonyesha masharti yanayowezekana (alama 2)
- c) Tunga sentensi sahihi ukitumia kitenzi **abudu** katika kauli ya kutendesheana (alama 2)
- d) Akifisha  
aisee yale mawimbi ya tsunami yaliyotokea bahari hindi yaliangamiza biashara nyingi sana alisema bomet (alama 4)
- e) Changanua sentensi hii kwa njia ya mstari.  
Rais alihutubu lakini walimpuuza (alama 4)
- f) Huku ukitolea mfano eleza tofauti kati ya kishazi huru na kishazi tegemezi (alama 3)
- g) Ainisha sentensi ifuatayo kwa kuzingatia jukumu lake  
Pika ugali kwa kuku kila Jumamosi ukitumia gesi (alama 2)
- h) Tunga sentensi moja ya kuonyesha rai (alama 1)
- j)  
i Eleza maana ya chagizo (alama 2)  
ii. Bainisha chagizo katika sentensi ifuatayo (alama 1)  
Shamba lilipaliliwa haraka na mkulima
- k) Andika katika usemi wa taarifa  
—**Hilo** kijicho cha paka cheupe leo marufuku kwangu” alisema Mzee Kambumbu (alama 3)
- l) Tunga sentensi moja ukitumia kitenzi kimoja kilichoundwa kutokana na nomino **zawadi** (alama 2)
- m). Tambua matumizi ya kiambishi **ji** katika sentensi ifuatayo  
Jino la jitu hilo lililiwezesha kujilia chakula kingi kuliko mkimbiasi yule (alama 2)
- n) Tunga sentensi moja kuonyesha maana ya neno: **ilmradi**. (alama 2)
- o) Andika sentensi moja ukitumia kihisishi cha bezo (alama 1)
- p) Ainisha viambishi katika neno **walibiana** (alama 2)
- q) Nini maana ya kiimbo? (alama 1)
- r) (i) Vokali ni nimi?  
(ii) Eleza sifa mbili za sauti ifuatayo / / (alama 2)
- s) Panda ni kuatika mbegu ardhini au kuparaga mti. Andika maana nyingine mbili (alama 2)

### D. ISIMU JAMII (Alama 10)

- a. Eleza nadharia tatu kuhusu chimbuko la Kiswahili. (alama 6)
- b. Fafanua istilahi zifuatazo:  
i. UwiliLugha  
ii. LinguaFranka  
iii. Misimu  
iv. Sajili (alama 4)

**SEHEMU YA A : USHAIRI****1. Swali la Lazima.**

*Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.*

Naujuwa mwanzo wake, vile ulivyochipuza,  
 Kilofanya mkereke, na kisichowaumiza,  
 Ya kuwa sepatu mke, katu hakuwapendeza,  
 Nenani mutamaliza, yeze nampenda vivyo !

Mwasema matako hana, yako sawa kama meza,  
 Tena pua yako pana, kama ya kubandika,  
 Lakini mimi naona, yenu sitoyasikiza,  
 Nenani mutamaliza, yeze nampenda vivyo !

Kipita nae pahali, sakubimbi hubwagiza,  
 Nzitonzito kauli, asengenywazo aziza,  
 Nywele za kipilipili, hasongi asongomeza,  
 Nenani mutamaliza, yeze nampenda vivyo !

Munenayo ni mazito, hadi yeze humliza,  
 Bali kwangu ni matoto, muhali kunichukiza,  
 Japo miguuye fito, haitoshi intembeza ?  
 Nenani mutamaliza, yeze nampenda vivyo !

Nataka watowa khofu, kwa munayo mtangaza,  
 Si yule mpenda pofu, kawambia ni kengeza,  
 Ni mwenyewe nimeshufu, muhali kunigeuza,  
 Nenani mutamaliza, yeze nampenda vivyo !

Tafadhalini mwachie, musilumbe kumaliza,  
 Unyonge musitumie, kila siku kumaliza,  
 Haya ni yeze na mie, yawaje mukachagiza,  
 Nenani mutamaliza, yeze nampenda vivyo !

Hakujiumba mwenyewe, musighafilike wenza,  
 Aloumba mimi nawe, ndiye aliyemtweza,  
 Tusijitie kiwewe, tukakufuru muweza,  
 Nenani mutamaliza, yeze nampenda vivyo !

**Maswali**

- a) Eleza bahari za shairi hili kwa kutoa ithibati kamili (alama 3)
- b) Kwa kutoa mifano mwafaka, eleza methali zozote mbili kwenye shairi (alama 4)
- c) Bainisha mambo yoyote manne nafsineni anayazungumzia (alama 4)
- d) Fafanua idhini ya mshairi (alama 4)
- e) Andika ubeti wa tatu kwa lugha tutumbi (alama 3)
- f) Eleza maana za vifungu hivi kama vilivyatumiika kwenye shairi
  - (i) Sakubimbi hubwagiza (alama 1)

(ii) Musighafilike wenza

(alama 1)

## SEHEMU YA B : RIWAYA

Said A. Mohamed : *Kidagaa Kimemwozea*

Jibu swalii la 2 au la 3

2. Alaa ! Mtoto mdogo hata ubwabwa haujakutoka shingoni unakimbilia nini...?  
a) Eleza muktadha wa dondo hili (alama 4)  
b) Bainisha tamathali mbili za usemi katika dondo (alama 2)  
c) Kwa kutoa mifano mitatu, onyesha kwamba kwa hakika ubwabwa ulikuwa umemtoka shingoni anayerejelewa (alama 6)  
d) Asasi inayorejelewa katika muktadha huu inakumbwa na matatizo mengi. Kwa kurejelea riwaya nzima, jadili matatizo yoyote manne kwa mifano mwafaka (alama 8)
3. Kifo cha Uhuru ni jazanda ya hali ya mambo katika jumuiya ya kidagaa kimemwozea. Thibitisha. (alama 20)

## SEHEMU YA C: TAMTHILIA

Pauline Kea: Kigogo

Jibu swalii la nne au la tano.

4. Umeshindwa kufuga kuku, kanga wafikiri utamweza ?  
a) Eleza Muktadha wa dondo hili. (alama 4)  
b) Fumbua wanaowakilishwa na kuku na kanga. (alama 2)  
c) Fafanua sifa za Msemewa. (alama 6)  
d) Bainisha maudhui ya utetezi wa haki katika tamthilia kigogo. (alama 8)
5. Masaibu yanayowafuata wanasagamoyo ni wazi katika tamthilia ya kigogo kama meno ya ngiri. Fafanua kauli hii. (alama 20)

## SEHEMU YA D: HADITHI FUPI

Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine.

Jibu swalii la 6 au 7

**Mapenzi ya kifauroongo.**

6. a) Onyesha jinsi maudhui ya utabaka na mapenzi ,yanavyojitekeza katika hadithi ya mapenzi ya kifauroongo. (alama 10)  
b) Penina ni kielelezo cha msichana wa kisasa katika jamii .Thibitisha kwa kurejelea sifa zake zozote tano. (alama 10)
7. Tumbo lisiloshiba‘  
a) Eleza jinsi ambavyo mbinu ya jazanda na ishara zimetumika katika hadithi hii. (alama 10)  
b) Onyesha mchango wa mzee Mago katika jamii ya Tumbo lisiloshiba kwa kurejelea sifa zake zozote tano (alama 10)

## SEHEMU YA E : FASIHI SIMULIZI

8. a) Eleza maana ya maigizo (alama 2)  
b) Fafanua dhima tano za michezo ya chekechea (alama 10)  
c) Eleza sifa nne za mivigha (alama 8)

**NAKURU CLUSTER**

**102/1**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA 1**

**(INSHA)**

**Insha ya lazima**

1. Kumekuwa na matokeo mambaya ya Kiswahili kwa kipindi cha miaka mitatu mtawalia. Umeteuliwa kama mtaalamu katika kaunti yako kuchunguza kiini cha matokeo haya mabaya. Andika ripoti ya uchunguzi wenu.
2. Umasikini ni changamoto kubwa katika maendeleo ya magatuzi. Jadili
3. Mchumia juani hulia kivulini.
4. Mlango wa nyuma ulibishwa mara tatu Ngo! Ngo! kufungua tu, nikasikia sauti *Alala chini.....* Endelea.

for free past papers, visit: [www.freekcsepastpapers.com](http://www.freekcsepastpapers.com)

**KISWAHILI: LUGHA****(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya Lugha na Isimu Jamii)****KARATASI YA 2****Sehemu A****Ufahamu.****Soma makala yafuatayo kasha ujibu maswali.**

Kweli, taarifa zimeonekana katika vyombo vya habari kuwa vijana wetu wanajua mengi kutushinda. Wengi wameshiriki ngono ilhali tukiwa nyumbani sisi wazazi tunawaona kuwa malaika.

Kwa kweli taarifa hizo ni sawa na mbiu ya mgambo kuwa tuzungumze na watoto wetu kuhusu suala hili. Ni vyema wajue kutoka kwetu kuliko kufahamu kutoka kwa wengine ambaa badala ya kuwaelekeza wanawapotosha. Mara nyingi wakiwa katikati ya marika, wao hushinikizana kujaribu na wengi wanaamini kuwa kufanya mara moja si tatizo. Lakini kile ambacho hawaelewii ni kuwa hiyo mara moja inaweza kuwabebesha mimba ama kuwaambukiza ukimwi na maradhi ya zinaa. Aihda, utu huumbuliwa na hivyo kupotoka kimaadili. Hayo ni masuala ambayo wazazi hawafai kuyaonea haya tena kwa sababu watoto wetu wanayafahamu lakini cha msingini kuja ukweli na hatari zilizopo.

Wazazi wengi wamewatelekeza watoto wao. Wengi husema kuwa wanawatimizia kila hitaji. Hii inamaanisha kuwa unalipa karo kwa wakati unaofaa, kuna chakula cha kutosha nyumbani, mavazi wako nayo na pia pesa za mfukoni wanazo. Lakini kile ambacho hawana ni muda wa kuwa na watoto wao. Baadhi ya matatizo tunayokumbana nayo yanaweza kutatuliwa ikiwa wazazi watatenga muda wa kuzungumza ana kwa ana na watoto wao.

Ni kweli wengi wamesingizia kazi zao kwa sababu wanaamka mapema na kurudi usiku. Lakini hiyo kazi ina maana gani ikiwa kesho utajipata na mjukuu wa kulea bila kutarajia? Kwa hivyo, wazazi lazima waache kuwaachia wafanyakazi wa nyumbani jukumu lao ama kuwapeleka katika shule za bweni mapema kwa sababu wanawaona kuwa mzigo. Pia kuna wale ambaa huwachwa hata vilabuni kwa madai kuwa wanakutana tu na marafiki zao.

Baadhi ya mavazi, ingawaje huwfanya watoto wao kuonekana kama wanaoenda na wakati ama ya kisasa, huwa hayafai. Lazima wafunzwe tangu wakiwa wachanga kuhusu suala la kuijheshimu. Haifai kufikiria kwamba kwa sababu ni mtoto anaweza kuvala chochote kile. Mtoto anafaa kuvishwa mavazi ya heshima. Pia, wazazi wachunguze mavazi yao wenyewe.

**Maswali.**

- a) Eleza dhamira ya mwandishi wa makala haya. (alamu 2)
- b) Kushirika ngono mapema kwa vijana kuna athari gani kilingana na makala haya? (alamu 4)
- c) Wazazi wamechangia vifaa shida zinazokumba vijana chipukizi? (alamu 4)
- d) Taja majukumu manne makuu ya mzazi kulingana na makala haya. (alamu 4)
- e) Eleza maana ya maneno haya kimuktadha.
  - (i) Madai (alamu 1)
  - (ii) Mbui ya mgambo (alamu 1)

**MUHTASARI.****Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Sekta za umma humu nchini hazina kifani katika uzembe. Unapohitaji huduma za posta, umeme, maji, mawasiliano, utayarishaji wa mishahara na malipo mengine, utalazimika kusubiri kwa siku, miezi na hata miaka ili upate haki yako, hata wakati mwingine ukakosa!

Wafanyakazi wa sekta hii hukosa kutimiza majukumu yao ipasavyo kutokana na ukosefu wa motisha yaani mishara duni, uhaba wa nyezo za kutekeleza majukumu yao na kutozingatia kazi kwa wakaguzi na viongozi wa wafanyakazi.

Minghairi ya hali hii, visa vya ufisadi ndiyo sifa inayopambanua huduma za umma. Baadhi ya wafanyakazi hupatikana maofisini na katika maeneo yao ya kikazi kwa nadra sana kwa sababu hukimbilia kwingineko kutafuta malipo ya kujazia mishahara yao duni kujikimu kimaisha. Athari za matendo haya zimekuwa kukokota kukua kwa uchumi, ukosefu wa imani kwa huduma za umma na utoaji wa huduma hafifu.

Kufuatia udhaifu huu, katika siku za majuzi, sekta za kibinafsi zimetambulika kuwa muhimu sana katika utoaji huduma kwa wananchi. Uchumi wa mataifa yanayopendelea sekta za kibinafsi yanetambuliwa kukua kwa kasi kuliko yale yanayoandamana mfumo kongwe wa serikali kutawala shughuli za uzalishaji mali.

Lakini kwa kuwa mashirika ya kibinafsi, aidha, yamebainika kuwa na udhaifu wa aina yake, serikali inaposhirikiana kindakindaki na sekta hii, uwastanishaji wa hali za kazi utajiri. Kwa kuwa dhamira kuu ya mashirika ya kibinafsi huwa kujizolea faida kemkem, yamekuwa yakifanyisha wafanyakazi wao kazi nyingi kupita kiasi ambayo mara nyingine huwadhuru kiafya. Japo mshahara wao ni afadhali kuliko wa sekta ya umma, baadhi ya sera huwa kandamizi na hutinga fursa za wafanyakazi kukuza majukumu yao binafsi, mengi yakiwa muhimu kwa jamii kwa jumla. Ushirikiano wa serikali na mashirika ya kibinafsi, kwa hiyo, una uwezo mkubwa wa kustawisha na kupanua mawanda ya uchumi. Utakuwa dawa mujarabu kwa udhaifu wa pande zote. Sekta za kibinafsi zinazolenga kujipatia faida nyingi, kwa upande mmoja, zitasaidia katika kuondoa uzembe, utepetevu na mapuuu yanayotamalaki huduma za serikali kwani yatalenga uzalishaji mwangi ili kutimiza malengo yao.

### **Maswali**

- a) Eleza mawazo muhumu ya aya tatu za kwanza kwa maneno 50-55 (alama 6) (1 utiririko)  
Fupisha aya tatu za mwisho bila kubadilisha maana iliyokusudiwa kwa maneno 75-80 (alama 7) (2 utiririko)
3. **SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA – ALAMA 40**
- a) Ainisha sentensi ifuatayo. (alama 3)  
Alituogofya.
- b) Eleza matumizi ya viambishi ki na na katika sentensi hizi (alama 2)  
i) Uji bila sukari haunyweki.  
ii) Wizi ule uliongozwa na Wanugu.
- b) Eleza maana mbili za sentensi hii; Wizi wa silaha umeongezeka (alama 2)
- c) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika hali zilizo kwenye mabano. (alama 2)  
i) Tua (Tendama)  
ii) Fumba (Tendata)
- d) Bainisha vielezi na ueleze ni vya aina gani. (alama 2)  
i) Ngozi imenyooka twaa  
ii) Arusi iliahirishwa hadi baadaye
- e) Changanua hii sentensi kutumia jedwali.  
Rehema ambaye huimba taarab ni mwanamke mpole.
- f) Tunga sentensi mbili kutofautisha vitate hivi kimaana. (alama 2)  
i) Hawara  
ii) Hawala
- g) Andika kwa wingi (alama 2)  
Zigo lile la kuliwa halilemei
- h) Geuza kwa ukubwa (alama 2)  
Mtoto aligutuka baada ya kumkanya nyoka  
i) Tumia viashiria vya kuthibitisha kujaliza pengo (alama 2)  
i) Tingatinga .....huegeshwahapa kila siku  
ii) Maarifa.....ndiyo yaliyomfanikisha
- j) Kanusha mbila kutumia amba’ (alama 2)  
Nitavaa nguo ambayo ni safi
- k) Andika nomino moja moja yenye sauti zifuatazo. (alama 2)  
i) Kituo kikwaruzo  
ii) Kimadende

- l) Bainisha aina za yambwa na chagizo ( alama 3)  
Binti yake Omari aliozwa Salim kwa arusi mwezi uliopita.
- m) Geuza sentensi iwe katika wakati uliopita, hali timilifu (alama 1)  
Aliomba msamaha kwa kuchelewa.
- n) Andika sentensi hii katika usemi halisi (alama 2)  
Amina alishangaa na kutaka kujua ni nani aliyejewa amekila chakula chake.
- o) Eleza maana ya; (alama 2)  
i) Mofimu  
Kiambishi
- ii) Taja aina za mofimu na kuzitolea mifano (alama 2)
- p) Eleza matumizi mawili ya alama ya ritifaa. (alama 2)

**4. ISIMU JAMII.**

Lugha ya magazeti ina upekee wake. Fafanua sifa tano kisha ueleze upekee huu ukusudia nini.

(alama10)

for free past papers, visit: [www.freekcsepastpapers.com](http://www.freekcsepastpapers.com)

**KISWAHILI  
KARATASI YA 3  
FASIHI**

**SWALI LA LAZIMA**

**KIGOGO**

1. .... Hivi vishahada vyao wanavyovipata siku hizi vinawavimbisha kichwa! Mtu anaitwa daktari na hata kazi ya maana hana....  
 a. Weka dondo hili hili katika muktadha wake (Alama 4)  
 b. Fafanua mbinu mbili za sanaa alizozitumia mwandishi (Alama 4)  
 c. Ukrejelea tamthilia ya Kigogo, dhihirisha kuwa mtu anaitwa daktari na hata kazi ya maana hana. (Alama 12)

**SEHEMU YA B: RIWAYA:**

**KIDAGAA KIMEMWOZEA – KEN WALIBORA**

**Jibu swali la 2 au 3**

2. Ujenzi wa jamii mpya ni wajibu wa vijana. Thibitisha ukweli wa kauli hii ukrejelea riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 20)  
 AU
3. —Lowela tunapendana mno na ni msiri wangu wala hakuogopa kuniambia yaliyojiri.  
 (a) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)  
 (b) Fafanua „yaliyojiri“ kwa mujibu wa msemaji. (alama 8)  
 (c) Lowela ni kielelezo kibaya cha msichana wa kisasa.  
 Thibitisha. (alama 8)

**SEHEMU C: HADITHI FUPI: TUMBO LISILOSHIBA**

**Jibu swali la 4 au 5**

4. —Hakchukua muda mrefu, akili zao zilipowaamsha kuwapeleka kwenye maana hasa ya kile kilichokuwa kikitokea ...”  
 a. Eleza muktadha wa dondo hili (Alama 4)  
 b. Fafanua tamathali ya usemi aliyoitumia mwandishi katika dondo hili (Alama 2)  
 c. Fafanua kile kilichokuwa kikitokea (Alama 2)  
 d. Eleza juhudzi zilizofanywa kuzuia kilichokuwa kikitokea kisitokee (Alama 12)
5. a. Ulezi umewapa wazazi wengi changamoto nyingi. Ukrejelea hadithi ya shogake, dada ana ndevu dhihirisha ukweli wa kauli hii (Alama 10)  
 b. Fafanua changamoto zinazokabili asasi ya ndoa ukrejelea hadithi ya Masharti ya kisasa (Alama 10)

**SEHEMU YA D: USHAIRI**

**Jibu swali la 6 au 7**

**6. Soma shairi hili kasha ujibu maswali yanayofuata:**

Jukwani naingia, huku hapa pasokota,  
 Kwa uchungu ninalia, hii tumbo nitaikata,  
 Msiba mejiletea, nimekila kiso takata,  
 We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

Wazee hata vijana, wote umewasubua,  
 Huruma nao hauna, heshima kawakosea,  
 Ukambani na Sagana, hata mbwa wararua,  
 We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

Wahasibu ofisini, kibwebwe mejifunga,  
 Miaka mingi vitabuni, ili wasikose ungua,

Nadhari wanadhamini, hesabu wanazirenga,  
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

Wapenzi wa kiholela, pia wanakuogopa,  
Baada yao kulala, wana wao wanatupa,  
Wakihitaji chakula, wanachokora mapipa,  
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

Wafugaji hata nao, kama dawa wakwamini,  
Hawajali jiranio, wamesusia amani,  
Wanaiba ng'ombe wao, na kuzua kisirani,  
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

Nayo mizozo ya maji, kaonekana kwa mara,  
Hiyo nayo ni dibaji, sababu sio harara,  
Njaa wahepe wenyeji, huo ndio mkarara,  
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

Ningeweza kukuza, ingekuwa siku njema,  
Tena kwa bei ya meza, sokoni nimesimama,  
Wala tena singewaza, kuhusu wali na sima,  
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?  
Hatima umefikika, naenda zangu nikale,  
Mate yanidondoka, kwa mnukio wa wale,  
Naomba kwenda kukaa, wala sio nikalale,  
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

### **Maswali**

- (i) Lipe anwani mwafaka shairi hili. (alamu 2)
- (ii) Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu. (alamu 2)
- (iii) Huku ukitolea mifano mwafaka, taja arudhi zilizotumiwa katika ubeti wa tatu. (alamu 4)
- (iv) Andika ubeti wa nne kwa lugha nathari. (alamu 4)
- (v) Thibitisha kuwepo kwa idhini ya ushairi. (alamu 2)
- (vi) Taja madhila anayoelezea mtunzi wa shairihili yaletwayo na tumbo. (alamu 4)
- (vii) Elezea maana ya maneno yafuatayo.
  - (a) Dibaji
  - (b) Harara(alamu 2)

AU

### **7. FASIHI SIMULIZI.**

- i. (i) Eleza maana ya misimu. (alamu 2)  
(ii) Eleza dhima ya misimu. (alamu 4)
- ii. Taja aina **nne** za ngomezi za kisasa. (alamu 4)
- iii. Eleza sifa **nne** za maapizo. (alamu 4)
- iv. Eleza kikwazo **vitatu** vinavyokumba Fasihi simulizi. (alamu 6)

**KASSU**  
**102/1**  
**KISWAHILI**  
**Karatasi ya 1**  
**INSHA**

**SWALI LA LAZIMA**

1. Kamati ya uajiri ya kaunti yako imekualika kwa mahojiano ya afisa msimamizi wa kukabiliana na janga la mafuriko. Andika tawasifu utakayoiwasilisha kwa kamati hiyo.
2. Ufisadi umekuwa tatizo sugu nchini. Jadili vyano vyake na upendekeze suluhu kwa uovu huo.
3. Pang'okapo jino pana pengo  
Kisha kidhihirishe maana ifuatayo.
4. Andika insha itakayoanza kwa maneno haya;  
Nilishusha pumzi, nikashukuru. . Masaibu yangu yalikuwa yamefika kikomo na maisha ya siku zijazo yalijaa matumaini.

**KASSU – 2018**  
**KIDATO CHA NNE**  
**102/2**  
**KISWAHILI**

**LUGHA**

**1. UFAHAMU**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.*

Athari za muda mrefu za pombe hutapakaa baina ya uwezekano wa faida za kiafya kwa watumiaji wa viwango vyta chini nya pombe hadi madhara makubwa katika hali ya matumizi mabaya ya pombe kwa muda mrefu.

Viwango nya juu nya matumizi ya pombe huhusiana na ongezeko la hatari ya kuendeleza ulevi, ugonjwa wa moyo, kutofyonza vyakula, ugonjwa sugu wa kongosho, ugonjwa wa ini kutokana na pombe, na kansa. Uharibifu kwa mfumo mkuu wa neva na mfumo wa neva za pembeni unawenza kusababishwa na matumizi kila mara ya pombe. Matumizi ya pombe kupita kiasi kwa muda mrefu yanaweza kuharibu takribani kila kiungo na mfumo katika mwili. Ubongo unaokua wa kijana aliyeboleghesha hadi kipatikanza na kipataki kwa pombe.

Kihistoria, madaktari wametetea pombe kwa faida zake za kiafya na hivi karibuni kwa ajili ya uwezo wake wa kulinda watumiaji dhidi ya ugonjwa wa moyo. Kuna ushahidi wa faida kwa mishipa ya moyo inayotokana na kutumia kinywaji kimoja hadi viwili kwa siku, hata hivyo, faida za kiafya kutokana na unywaji pombe kwa wastani ni swala lenye utata. Shauku zimetolewa kuwa sawa na ilivyo katika sekta ya dawa, wadau wa sekta ya pombe pia wamehusika katika kutila chumvi faida za kiafya za pombe. Pombe inapaswa kuonekana kama dawa ya burudani yenye uwezo mkubwa wa kusababishwa athari mbaya kwa afya na haipendekezwi kwa ulinzi wa moyo badala ya mbinu nyinginezo za salama na zilizothibitika za jadi kama vile lishe bora mazoezi na tiba.

Baadhi ya wataalamu wanadai kuwa faida za matumizi ya pombe ya wastani zinaweza kupitwa na ongezeko la hatari ikiwa ni pamoja na majeraha, vurugu, uharibifu wa mimba, aina fulani za saratani, ugonjwa wa kongosho na presha. Kwa vile faida bainifu za kiafya za matumizi ya pombe ya wastani ni ndogo kwa watu walio katika hatari ndogo ya kupata maradhi ya moyo, wataalamu wengine wanatahadharisha itumike kwa tahadhari kwa sababu ya uwezekano kwamba kupendekeza matumizi wastani ya pombe kunaweza kusababishwa ongezeko la hatari ya matumizi mabaya ya pombe, hasa mionganini mwa vijana.

Madhara mabaya ya matumizi ya pombe kwa muda mrefu kupita kiasi ni sawa na yale yanaoonekana katika vitulizi-hipnoti vingine (mbali na sumu kwa viungo ambayo hutatiza zaidi katika pombe). Athari za kujiondoa katika pombe na utegemezi hukaribia sana kufanana. Pombe cha kiwango wastani ina athari chanya na hasi kwa afya. Athari hasi ni pamoja na ongezeko la hatari ya magonjwa ya ini, saratani ya orofarinji, kansa ya umio na ugonjwa wa kongosho. Kinyume na hayo, unywaji wastani wa pombe unawenza kuwa na athari za faida kwa gastriti na kolelithiasi. Matumizi

sugu na mabaya ya pombe huwa na athari kubwa wa afya ya mwili na akili. Unywaji sugu wa pombe kupita kiasi au utegemezi pombe, unawenza kusababisha uharibifu mpana wa viungo mbalimbali vya neva za ubongo, mfumo wa neva ama ugonjwa wa mishipa ya moyo, maradhi ya ini, na neoplasmsi isiyopona. Matatizo ya akili ambayo huhushishwa na ulevi ni pamoja na mfadhaiko mkubwa, disthimia, mania, hipomania, tatizo la hofu, tatizo la wasiwasi wa kijumla, tatizo la tabia za mtu, skizofrenia, kujinyonga, upungufu wa mfumo wa utendakazi mwilini (kwa mfano kazi za kumbukumbu, hisia, kazi za uamuzi, uwezo wa kuona, mwendo na uwiano) na uharibifu wa ubongo. utegemezi wa pombe ni huhushishwa na shinikizo la damu, ugonjwa wa moyo na kiharusi cha iskemi, kansa ya mfumo wa upumuaji, mbali pia na saratani ya mfumo wa mlo, ini, kifua na ovari. Unywaji kupita kiasi huhushishwa na ugonjwa wa ini, kama vile sairosi. Tafiti zimelenga wanaume na wanawake, vikundi vya umri mbalimbali na watu wa makundi mengi ya kijamii. Machapisho kwa sasa yanafikia jumla ya mamia huku tafiti zikiweza kuonyesha uwiano uliopo kati ya matumizi wastani ya pombe na afya ambayo labda yanaweza kuwa yalitokana na athari za manufaa ya maingiliano ya kijamii ambayo mara nyingi huambatana na matumizi ya pombe. Baadhi ya njia mahususi ambapo pombe huweza kuathiri afya ya mishipa ya moyo zimetafitiwa.

## Maswali

- a. Yape makala haya mada faafu. (alama 1)
- b. Eleza madhara yanayotokana na uharibifu wa mfumo mkuu wa neva za pembeni. (alama 2)
- c. Eleza faida za matumizi ya pombe kwa mujibu wa kifungu. (alama 3)
- d. Mwandishi anapendekeza vipi kwa matumizi ya pombe ya kiwango cha wastani? (alama 3)
- e. Matumizi sugu yana malipo yapi kulingana na madaktari. (alama 3)
- f. Tafiti zilizofanywa zililenga jinsia ya kiume pekee. Thibitisha. (alama 1)
- g. Eleza maana ya misamiati hii kulingana na taarifa (alama 2)
  - (i) wadau .....
  - (ii) aliyebaleghe .....

## 2. UFUPISHO

Ni dhahiri shahiri kwamba uharamia umechipuka kama desturi na mfumo wa maisha katika siku za hivi karibuni. Janga hili limeshamiri hususan pembeni mwa bara la Afrika na kanda ya Afrika Mashariki. Taarifa za uharamia zimetawala vyombo vya habari, kiasi kwamba haipiti siku bila kuripotiwa visa vipyta vya matendo haya mabovu ambayo yanaweza tu kumithilishwa na uhayawani. Matukio haya yamewalimbikizia mabaharia wa nchi husika, simanzi na masaibu yasiyoweza kuatiwa kwenye mizani.

Yamkini tatizo hili halitokei pasi na kumotishwa na kitita kikubwa cha fidia kinachodaiwa na maharamia hawa. Aghalabu, suala hili lahusishwa pakubwa na azma na ari ya kuendeleza ujambazi wa kimataifa sawia na ulipuaji wa bomu mjini Nairobi na Dare-es salaam mnamo Agosti 7,1998 na tukio la Septemba 11, mwaka wa 2001 kule Marekani. Maafa na uharibifu wa mali si hoja, la mno kwa maharamia ni kutosheleza matakwa yao. Kwa upande mwagine, ukosefu wa tawala-wajibika katika maeneo kunakotokea unyama huu ni thibitisho tosha la mazingira yanayowezesha na kuruhusu kuchipuka kwa janga hili.

Mchipuko wa baa la uharamia umelengwa jamii ya kimataifa ambayo ni mhudumu mkuu wa harakati za kusitisha majanga makubwa kama vile njaa, umasikini na magonjwa yaliyosheheni pakubwa barani. Bila shaka, hili ni suala linalosawisishwa na 'kinyume mbele'. Maharamia wanatishia utangamano wa kimataifa wanapotibia usafiri wa abiria na shehena zinazoelekezwa sehemu tofauti ulimwenguni.

Matumizi ya kidiplomasia na mashauriano hayaelekei kuzalisha matunda katika juhudhi za kudhibiti uharamia. Zaidi ya hayo, matumizi ya nguvu yahusishayo mashambulizi pamoja na maharamia kufunguliwa mashtaka nchini Kenya

na Ufaransa kunaelekea kuzipiga jeki juhudzi za uharamia ulimwenguni. Aidha, utawala wa nchi kunakochipuka uharamia haujajizatiti kuhamisha doa hili linalotisha ustawi wa kimataifa.

Mathalan, ni jambo lisilopingika inapobainika kuwa uharamia umedumaza biashara ya kimataifa, hali inayochangia upungufu na ucheleweshaji wa bidhaa muhimu zinazoendeleza ustawi wa uchumi. Dosari hii inaelekea kukwamiza mojawapo wa malengo ya maendeleo ya milenia yanayosisitiza uimarishaji na ushirikiano wa maendeleo na upanuzi wa masoko ulimwenguni. Harakati za kitalii katika kanda mashariki ya bara la Afrika zimehujumiwa. Ni muhalii kwa utali kustawi kwenye maeneo yaliyo na tishio la usalama. Itakumbukwa bayana kwamba watalii hawasafiri tu kwa ndege bali hata kwa meli.

Jitihada za kuweka laini za mawasiliano chini ya bahari ili kurahisisha na kupunguza gharama za **mtando** ulimwenguni ni ndoto ambayo hajatimia hadi hivi sasa, kufuatia juhudzi za maharamia katika bahari ya Hindi. Kwa mujibu wa hali hii, mawasiliano mepesi na nafuu yasitarajiwe hivi karibuni. Licha ya hayo, shughuli za uvuvi na biashara nyinginezo kwenye kanda ya mwambao zimetiliwa shaka si haba.

Itabidi mikakati kabambe na suluhisho la kudumu liweze kupatikana ili vitendo vya uharamia viweze kusitishwa.

- (a) Fupisha aya mbili za kwanza kwa maneno 70 (alama 8, 1 ya mtiririko)  
(b) Onyesha jinsi ambavyo Kenya imeathiriwa na uharamia na namna hali hii inatia hofu. Maneno 60, (alama 7, 1 ya mtiririko 1)

### MATUMIZI YA LUGHA

- (a) Andika neno lenye silabi mbili za irabu. (alama 1)  
(b) Ni sauti gani haifai kuwa mionganii mwa hizi? Toa sababu. (alama 2)  
/ng/, /g/, /t/, /k/  
(c) Tunga sentensi mbili tofauti kwa kutumia neno walakini kama: (alama 2)  
(i) kiunganishi  
(ii) nomino  
(d) Panga maneno yafuatayo ili kutunga sentensi sahihi ya Kiswahili. (alama 2)  
Walikataliwa wanasiasa baadhi ya katika nchi wachache uhasama waliochochea.  
(e) Ainisha mofimu katika neno lifuatalo Hakumjia (alama 3)  
(f) Tambua shamirisho katika sentensi hii Chema alimuuzia mtalii wa Kimarekani lesi za Kimaasai. (alama 2)  
(g) Uganisha sentensi zifuatazo ukitumia o rejeshi tamati katika wingi. (alama 2)  
Kambare amenaswa demani.  
Kambare atauzwa sokoni.  
(h) Tunga sentensi yenye kivumishi cha jina. (alama 2)  
(i) Changanya kwa jedwali Kama atasoma kwa bidii, atapita mtihani. (alama 3)  
(j) Tunga sentensi sahihi ukitumia visawe vya neno \_dalali'. (alama 1)  
(k) Andika udongo wingi wa sentensi ifuatayo Njia hii inafaa zaidi kuliko ile. (alama 2)  
(l) Mwajiri wao amekuja kuwalipa mshahara. (Andika katika hali ya ukatavu) (alama 2)  
(m) Andika sentensi hii upya ukitumia chagizo cha wakati. Bata alienda njini. (alama 1)  
(n) Geuza sentensi ifuatayo iwe katika usemi halisi. (alama 2)  
Moraalituhidi kuwa angetutembelea mwaka ambao ungefuata.  
(o) Andika upya kulingana na maagizo (alama 2)  
(i) Mgonjwa amelazwa hospitalini (kutendesheka)  
(ii) Mama ameinjika chungu mekonii. (tendua)  
(p) Andika miundo miwili ya kirai nomino. (alama 2)  
(q) Mbali na kutumika mwanzoni mwa sentensi na nomino za pekee, eleza matumizi mengine mawili ya herufi kubwa. (alama 2)  
(r) Kwa kutoa mifano, onyesha miundo mitatu ya ngeli ya U – ZI. (alama 3)  
(s) Onyesha matumizi mawili ya kiambishi {i} (alama 2)

(t) Tumia kishazi tegemezi katika sentensi kuvumisha nomino.

(alama 2)

## ISIMU JAMII

### *Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.*

- Mwatani: Rusha hiyo ball haraka tumechelewa five minutes. Twende daro.  
Omoshi: Harakisha mode anacome.  
Bwana Kipiti: Nendeni darasani haraka! Kisha kiranja awape vitabu vyenu nya insha ili mwandike barua.  
Mwatani: Sawa mwalimu. Samahani kwa kuchelewa uwanjani.  
Omoshi: Je, tutaandika barua rasmi au barua ya kawaida?  
Bwana Kipiti: Mwandike barua rasmi. Je, mnakumbuka muundo wake?  
Omoshi na Mwatani: Ndio mwalimu. Ulitufundisha jana. Asante sana mwalimu.  
Bwana Kipiti: Kumbukeni idadi ya maneno. Idadi ya maneno ni muhimu katika uandishi wa insha.

## Maswali

- (i) Eleza sajili katika dondoo.  
(ii) Eleza sifa nane za sajili hii zinazopatikana katika dondoo.

(alama 2)  
(alama 8)

**SEHEMU A : RIWAYA – LAZIMA****K. Walibora: Kidagaa Kimemwozea**

1. —Kvani wewe wajua wamefanya nini?”  
 —Suu na sitaki kujua.”  
 (i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)  
 (ii) Eleza mbinu ya kisanaa iliyotumika katika dondoo. (alama 2)  
 (iii) Fafanua hulka za anayeulizwa swali. (alama 4)  
 (iv) —Unhianiye ndiye kumbe siye.” Fafanua kauli hii kwa kurejelea riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 10)

**SEHEMU B: TAMTHILIA YA KIGOGO****AMA**

2. Uliona nini kwa huyo zebe wako? Eti mapenzi!  
 i) Eleza muktadha wa dondoo. (alama 4)  
 ii) Andika mbinu mbili za lugha zinazojitokeza kwenye dondoo hili. (alama 4)  
 iii) Taja hulka za mnenaji unaojitokeza katika dondoo. (alama 2)  
 iv) Mwanamke ni kiumbe wa kukandamizwa. Thibitisha kauli hii ukirejelea tamthilia. (alama 10)  
**AU**  
 3. Ni bayana kwamba viongzoi wengi katika nchi zinazoendelea wamejawa na tamaa na ubinafsi. Thibitisha kauli hii ukirejelea tamthilia ya kigogo. (alama 20)

**SEHEMU C: TUMBO LISIOSHIBA NA HADITHI ZINGINE****SHIBE INATUMALIZA****AMA**

4. —Ndug yangu kula kunatumaliza”  
 —Kunatumaliza au tunakumaliza”  
 (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)  
 (b) Fafanua maana ya kitamthali katika kauli kula tunakumaliza“ (alam 10)  
 (c) Kwa mujibu wa hadithi hii, nbi kwa namna gani wasemaji wanadai kula kunawamaliza? (alama 6)  
**AU**  
 5. (a) —Mame Bakari”  
 Kwa mujibu wa hadithi hii, ubahaimu anaotendewa mwanamke unakuwa na athari mbaya kwake. Onyesha kwa mifano mwafaka. (alama 10)  
 (b) —Masharti ya Kisasa”  
 —...mapenzi ni mateso, ni utumwa, ni ukandamizaji , ni ushabiki usio na maana.”  
 Thibitisha ukweli wa kauli hii kama unavyojitokeza kwenye hadithi. (alama 10)

**SEHEMU D : SHAIRI A****AMA**

6. MWANA  
 1. Kwani mamangu u ng‘ombe, au u punda wa dobi?  
 Nakuuliza usambe, nayavunja madhehebi  
 Nalia chozi kikombe, uchungu wanisibabi  
 Hebu nambie  
 Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

**MAMA**

2. Nong‘ona mwana nong‘ona, sitafute angamiyo  
 Sinipe kuja sonona, kwa uchungu na kiliyo

Babayo mkali sana, kubwa pigo la babayo  
Kwani kelele kunena, huyataki maishiyo?  
Hilo nakwambia.

#### MWANA

3. Sitasakamwa kauli, nikaumiza umiyo  
Nikabeba idhilali, nikautweza na moyo  
Siuvuwati ukweli, hazidisha gugumiyo  
Baba hafanyi halali, nawe hwachi vumiliyo  
Hebu nambie  
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

Nambie ipi sababu, ya pweke kwenda kondeni  
Nini yako matulubu, kulima hadi jioni?  
Na jembe ukidhurubu, ukilitua guguni  
Yu wapi wako muhibu, Baba kwani simuoni?  
Hebu nambie  
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

Baba kwani simuoni, kuelekea shambani?  
Kutwa akaa nyumbani, na gumzo mitaani  
Hajali hakuthamini, wala haoni huzuni  
Mwisho wa haya ni nini, ewe mama wa imani?  
Hebu nambie  
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

Na kule kondeni kwako, ukate kuni kwa shoka  
Ufunge mzigo wako, utosini kujitwika  
Kwa haraka uje zako, chakula upate pika  
Ukichelewa vituko, baba anakutandika  
Hebu nambie  
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

Chakula kilicho ndani, ni jasho lako hakika  
Kiishapo u mbioni, wapita kupokapoka  
Urudi nje mekonzi, uanzze kushughulika  
Ukikosa kisirani, moto nyumbani wawaka  
Hebu nambie  
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo

#### MAMA

Wanitonesha kidonda, cha miaka na miaka  
Usidhani nayapenda, madhila pia mashaka  
Nakerwa na yake inda, na sasa nimeshachoka  
Ninaanza kujipinda, kwa mapambano hakika  
Hilo nakwambia

#### MASWALI

- a) Mtunzi wa shairi hili alikuwa na dhamira gani katika kutunga shairi hili. (alama 2)
- b) Shairi hili la aina gani. Toa ithibati. (alama 2)
- c) Yataje mambo yoyote matano anayoyalalamikia mwana. (alama 5)
- d) Eleza kanuni zilizotumika kusarifu ubeti wa tatu. (alama 5)
- e) Andika ubeti wa saba kwa lugha tutumbi. (alama 4)

- f) Eleza maana ya maneno haya yaliyotumika katika shairi hili.

(i) jaza  
(ii) muhibu

(alama 1)  
(alama 1)

## AU

### 7. SHAIRI B

Soma shairi hili kisha ujibu maswali

1. Punda kalibebe gari, gari limebeba punda  
Mwalimu ana pakari, muashi vyuma adunda  
Jaji gonga msumari, sonara osha vidonda.  
Kinyume mbele
2. Saramala ahubiri, muhunzi tiba apenda  
Mganga anaabiri, baharini anakwenda  
Hata fundi wa magari, anatomea vibanda  
Kinyume mbele
3. Wakili anahiyari, biashara kuitenda  
Mtazame askari, akazakaza kitanda,  
Mkulima mashuhuri, jembe limemshinda  
Kinyume mbele
4. Apakasa daktari, ukili anaupinda  
Saveya kawa jabari, mawe anafundafunda,  
Hazini wa utajiri, mali yote aiponda,  
Kinyume mbele
5. Msemi huwa hasemi, wa inda hafanyi inda  
Fahali hawasimami, wanene waliishakonda  
Walojitia utemi, maisha yamewavunda  
Kinyume mbele
6. Kiwapi cha kukadiri, twavuna shinda kwa shinda  
Tele haitakadari, huvia tulivyopanda  
Mipango imehajiri, la kunyooka hupinda  
Kinyume mbele

### MASWALI

- a) Mtunzi alikuwa na malengo gani alipotunga shairi hili? (alama 3)
- b) Licha ya tarbia, eleza bahari nyingine zinazojiteza katika shairi hili. (alama 4)
- c) Eleza namna mtunzi alivyoutumia uhuru wake. (alama 5)
- d) Ni mbinu gani inayotawala shairi hili? (alama 2)
- e) Uandike ubeti wa nne katika lugha nathari. (alama 4)
- f) Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)

### SEHEMU E:

### 8. FASIHI SIMULIZI

1. Eleza vigezo vinne vya kuainisha methali . (alama 4)
2. Eleza fani zinazozijenga vitendawili vifuatavyo:
  - i) Ajenga ingawa hana mikono
  - ii) Jani la mgomba laniambia habari zinazotoka ulimwenguni kote(alama 4)
3. Nini tofauti kati ya misimu na lakabu? (alama 2)
4. i) Miviga ni nini?  
ii) Fafanua hasara zozote tano za miviga (alama 2)
-

5. i) Tambua kipera cha makala yafuatayo (alama 2)  
—Wwe ni mbumbumbu kiasi kwamba ukiona picha yako kwenye kioo unashangaa ulimwona wapi mtu huyo.  
ii) Ngomezi ni nini? (alama 1)

for free past papers, visit: [www.freekcsepastpapers.com](http://www.freekcsepastpapers.com)

## GATANGA

102/1

### KISWAHILI

#### KIDATO CHA NNE

#### KARATASI YA 1

##### 1. Lazima.

Wewe umehitmu shahada ya uzamifu kutoka Chuo Kikuu cha Malishoni. Umetuma barua ya kuomba kazi katika taasisi moja inayoshughulika na uhifadhi wa mazingira. Andika tawasifu utakayoiwasilisha kwa wanajopo.

2. Fafanua umuhimu wa viranja shulen .

3. Tunga kisa kitakachodhahirisha maana ya methali ifuatayo: Uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti .

4. Andika insha itakayoanza kwa maneno:

Siku hiyo nilitoka nyumbani nikiwa nimezongwa na mawazo mengi baada ya mkasa huo.

102/2

### KISWAHILI - KARATASI YA 2

#### KIDATO CHA NNE

#### UFAHAMU ( ALAMA 15)

##### Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali .

Tokea muundo mpya wa serikali ya ugatuzi uanze kutekelezwa miaka mitano iliyopita,kumeendelea kushuhudiwa matatizo mengi hali iliyopelekea kushuhudiwa kwa msururu wa migomo na maandamano ya raiya. Fujo za karibuni kabisa ni zile zinazoshuhudiwa katika miji mikubwa za wachuuzi na wanafanyibiashara wakipinga hatua za serikali za kaunti kuwatoza ushuru takribani kwa kila huduma na bidhaa ikiwemo wanyama, kuku na ndege.La kuhuzunisha zaidi katika baadhi ya majimbo imeripotiwa kuwa raia wamelazimishwa kulipa ushuru kwa kutaka tu kuona maiti za jamaa zao kwenye vyumba vya kuhifadhi maiti !.

Wanasiasa wameonekana kuwa na wakati mgumu kutetea mfumo huu mpya wa ugatuzi huku baadhi wakisema kwamba matatizo yanayoshuhudiwa kwa sasa yametokana na ugeni wa mfumo huo. Wengine wameinyoshea kidole serikali ya kitaifa kwamba ndiyo inayosambaratisha muundo huu. Wengine wanahoji kuwa bado ni mapema na kwamba kunahitajika muda mrefu ili kufaulu.

Ni wazi kwamba kumekosekana nidhamu bora ya kusimamia maisha ya raiya nchini Kenya. Matatizo yanayokumba raia kwa sasa ni dalili kuwa mfumo wa serikali ya ugatuzi umeongezea chumvi kwenya kidonda badala ya kutibu. Swalii ni je, hadi lini nidhamu ya kusimamia raia itakuwa ni suala la majaribio na makosa?

Hatua ya kuwarundikizia raia ushuru mkubwa ni kitendo cha unyonyaji na cha dhuluma kinachofaa kupingwa.. La kufahamishwa hapa ni kwamba ushuru ndio njia kubwa ya kuzalisha mapato ya serikali zinazojifunga na mfumo wa kimagharibi wa kiuchumi wakibepari ikiwemo Kenya. Asilimia 90 ya mapato ya serikali za kibepari huegemea ushuru. Kwa hivyo hatua ya serikali za kaunti katika kuwanyonya raia kwa kuwalipisha ushuru si ajabu bali ni thibitisho kuwa jamii ya Kenya inaongozwa na nidhamu ya kiuchumi ya ubepari mfumo wa nyonyaji na ukandamizaji. UKweli unabakia kuwa ndani ya serikali za kibepari raia ndio hubebeshwa mzigo wa ushuru unaoishia matumboni mwa viongozi!.

Miito ya madadiliko ya katiba na ya miundo mipyä ya kiutawala si lolote ila ni moja tu ya hatua za mfumo wa kibepari kujipa muda wa kuishi na kuziba aibu zake za kushidwa kusimamia maisha ya watu. Kufeli huku kwa mfumo huu kunashuhudiwa hadi kwenye nchi kubwa za kibepari kama Marekani na Uingereza hivyo nazo zimekubwa tele na maandamano na fujo za raia wakilalamikia hali ngumu ya maisha.

## **Maswali**

- a) Yape maka haya anwani mwafaka. (alama 1)
- b) Eleza mtazamo wa wanasiasa kuhusu utepetevu wa mfumo huu ( alama 3)
- c) —Ugatu ni chini Kenya ni mfumo wa kibepari — Thibitisha kauli hii kwa kurejelea makala (alama 3)
- d) Migomo ni zao la matatizo yaliyogatuliwa kutoka serikali kuu. Toa sababu nyingine zinazosababisha migomo katika serikali za ugatu ( alama 4)
- e) Thibitisha jinsi mfumo wa ugatu umeongeza chumvi kwenye kidonda badala ya kutibu ( alama 2)
- f) Eleza maana ya meneno yafuatayo . ( alama 2 )
  - i) Ugatu
  - ii) Kibepari .

## **UFUPISHO : ALAMA 15**

*Soma kifungu kifuatacho cha habari kisha ujibu maswali yanayofuatia.*

### **Utoaji wa Huduma ya Kwanza .**

Inaaminika kuwa majeruhi wengi katika mikasa ya ajali huaga au huadhirika vibaya zaidi kutokana na hali mbaya ya uokoaji. Watu wengi ambao hujitolea kuokoa majeruhi baada ya ajali kama za barabarani, maporomoko ya ardhii au nyumba huwa hawang'amui hata chembe jisni ya kukabiliana na uokoaji. Hatima ya juhudii zao ambazo hulenga kutenda mema ni kuathirika zaidi kwa majeruhi.

Hali ya uokoaji inaweza kurekeblishwa kwa kutoa elimu ya huduma ya kwanza kwa umma.. Elimu hii yahitajika na kila mkenya kwani mikasa ya ajali za barabarani na nyinginezo inaendelea kutokea kila siku. Ajali zinapotokea, si ajabu kuona makundi ya waokoaji yakibeba majeruhi hobelahobelaa bila kuzingatia madhara yanayoweza kuwaongeza kutokama na ubebaji wao. Kutojua namna ya kumbeba majeruhi kunaweza kumhatarisha na hata kusababisha kifo.

Kuna mambo mbalimbali ambayo makundi ya waokoaji yanatakiwa kuzingatia wakati wa huduma ya kuokoa. Kwanza ni muhimu kuchunguza kama kuna hatari yoyote inayoweza ikatokea na kuwatia majeruhi na waokoaji hatarini zaidi. Makundi ya waokoaji yaweza kuhatarisha majeruhi kwa kiliingilia eneo la ajali mbumbumbu kama mzungu wa reli

Hatua ya pili ni kutafuta idadi ya majeruhi. Pana uwezekano wa majeruhi kutupwa mbali na eneo la ajali. Vivyo hivyo, kuna mejeruhi ambao huweweseka baada ya ajali na kuanza kutembea wasijue wanakoelekea. Wengi wao huanguka karibu na eneo la ajali au wakaenda mbali.

Hatua ya tatu ni kuchunguza kama majeruhi amezimia, moyo unapiga na jinsi anavyopumua . Ili kuhakikisha kuwa majeruhi anapumua ,mwokoaji atazame kama kifua kinapanda na kushuka . Hali kadhalika, mwokoaji anaweza kusikiliza au kuguza kifua na kuona kama kuna ishara za kupumua. Iwapo majeruhi anapumua,mwokoaji amweke hali amabayo itaimarisha kupumua kwake. Anaweza akamlaza chali au kumgeuza kwa pamoja na kichwa chake ili kufungua mkondo wa hewa. Pia mwokoaji ahakikishe hamna chochote kiywani kinachowenza kumsakama. Ikiwa hapumui, mwokoaji anaweza kujaribu kumfanya apumue kwa kupuliza hewa mdomoni mwake. Fauka ya hayo, upulizaji wa hewa utahakikisha kuwa damu inazunguka mwilini vizuri.

Hatua nyingine ni kuchunguza vile amejeruhiwa. Chunguza kama majeraha ni vindonda tu au kuna kuvunjika kwa mifupa, ni muhimu kutotumia kiungo kilichovunjika anapobebwa.

Pia. Kuchunguza vile majeruhi amejeruhiwa, humwezesha mwokoaji kujua huduma ya dharura atakayotumia . Majeruhi akiwa anavuja damu sana, ni muhimu kuzuia uvujaji huu. Iwapo ni kidonda kidogo, kinahitaji kifungwa ili kuzuia uambukaji. Mwokoaji anaweza kutumia kifaa chochote kilicho karibu kutolea huduma hizi. Kwa mfano anaweza kupasua nguo ya majeruhi ili apate kitambaa cha kusaidia kuzuia kuvuja kwa damu au kumfunga kidonda. Hatua inayofaa ni kumhamisha majeruhi kutoka eneo la ajali hadi hospitalini .Mwokoaji anaweza kuwatumia watu wengine kutafuta msaada. Wanaweza kupiga simu wakitumia nambari za simu za dharura kama zile za polisi,wazimamoto au makundi ya wataalamu wa shughuli za uokoaji. Nambari hii ya simu huwa 999 popote na haina malipo. Wanaopiga simu ni vyema kutoa maelezo ya mahali ambapo ajali imetokea, aina ya ajali na huduma

za dharura zinazohitajika pamoja na idadi ya majeruhi. Iwapi makundi haya ya uokoaji yameahidi kufika, ni bora kuyasubiri.

Ikiwa makundi ya wataalamu wa uokoaji hayakupatikana, ni jukumu la mwokoaji kuhakikisha majeruhi wamehamishwa na kupelekwa hospitalini. Majeruhi wakiwa wengi ni bora kuanza na wale waliozimia au wenye matatizo ya kupua kisha kuwaendea wanaovuja damu sana. Baadaye, mwokoaji awasadie waliovunjika mifupa huku akimalizia na wenye majeraha yasiyohatarisha maisha. Ni muhimu kuwabeba majeruhi kwa kutumia machela. Hii hupunguza kuathirika zaidi kwa majeruhi. Iwapo hamna machela karibu, mwokoaji anaweza kuunda moja kwa kutumia vipande viwili vya mba, blanketi, shuka au makoti. Ujuzi wa huduma ya kwanza ni mojawapo ya mambo muhimu ambayo kila mtu anapaswa kuwa nayo.

#### Maswali :

- a) Fupishaaya mbili za kwanza kwa maneno 55 – 65. ( alama 7 , 1 utiririko )
- b) Eleza kwa kutumia maneno 90 – 100 hatua zinazotakiwa kufuatwa wakati wa uokoaji . ( alama 8, utiririko 1)
- 3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40 )**
- a) Andika sifa **mbili mbili** bainifu za sauti zifuatazo ( alama 2)
- i) /gh/  
ii) /b/
- b) i) Eleza maana ya sauti mwambatano ( alama 1)  
ii) Taja silabi **mbili** mwambatano za mdomoni ( alama 1)
- c) Ainisha viambishi katika kitenzi kifuatacho : Alijikatia ( alama3)
- d) Tunga sentensi tatu kuonyesha matumizi matatu ya kiambishi li. (alama3)
- e) Tunga sentensi yenye kitenzi kishirikishi kipungufu katika ngeli ya **KU** ( alama 2)
- f) Mtume ni tamko la kuonyesha mshutuko , \_\_\_\_\_ ni tamko la kuonyesha kuridhika ( alama 1)
- g) Andika sentensi zifuatazo upya kulingana na maagizo .  
i) Wanafunzi wengine wameadhibiwa ( Tumia kiwakilishi) ( alama 1)  
iii) Mtoto alimpiga mbwa kwa kijiti (Andika katika ukubwa wingi ) ( alama 2)
- h) Tunga sentensi ukitimia kiunganishi cha kujumuisha. ( alama 2)
- i) Tunga sentensi ukitimia neno **-mpaka**” kama,  
i) Kihusishi cha kiwango ( alama 1)  
ii) Kihusshi cha wakati ( alama 1)
- j) Tambua na ueleze virai katika sentensi ifuatayo:  
Kischana kile kimejirembesha kwa manukato mazuri ajabu. ( alama 3)
- k) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao ( alama 4)  
i) RN + RT  
ii) Nomino + Kivumishi + Kivumishi + Kishazi tegemezi + Kitenzi kishirikishi + Kivumishi
- l) Tunga sentensi ukitimia kielezi mfanano ( alama 2)
- m) Yakinisha sentensi ifuatayo :  
Nisipomwona darasani sitampa kitabu chake. ( alama 2)
- n) Andika sentensi ifuatayo katika wakati uliopita hali timilifu . ( alama 2)  
Dobi huwapigia watu nguo pasi .
- o) Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi mawili tofauti ya ritifaa. ( alama 2)
- p) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo:  
Msichana aliitwa mara nyngi . (alama 1)
- q) Tunga sentensi katika hali ya amri wingi ( alama 1 )
- r) Andika sentensi hii katika usemi wa taarifa.  
—Nampokea mjomba iwapo nitampata.“Rehema alimwambia shangazi yake. ( alama 2)
- s) Eleza maana **mbili** ya neno pora’ ( alama 1)
- 4. ISIMU JAMII ( ALAMA 10 )**
- a) Fafanua wajibu wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa ( alama 5)
- b) Eleza sifa za lugha ya Kiswahili ( alama 5)

**KISWAHILI KARATASI YA 3: FASIHI****KIDATO CHA NNE : MACHI 2018****SEHEMU A: LAZIMA: SHAIRI****WASIA**

Huno wakati mufti, vijana nawausia  
 Msije juta laiti, mkamba sikuwambia  
 Si hayati si mamati, vijana hino dunia  
 Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula

Japo aula kushufu, na machoni vyavutia  
 Dunia watu dhaifu, yaugua nasikia  
 Vijana nawasarifu, falau mkisikia  
 Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula.

Jepusheni na zinaa, miale penye sheria  
 Msije andama baa, makaa kujipalia  
 Jepusheni na zinaa, madhara kukadiria  
 Uonapo yyang'aria, tahadhari vitakula.

Ngawa waone wazuri, nadhifu kukuvalia  
 Wajimwaie uturi, na mapoda kumichia  
 Si mlango nyumba nzuri, ngia ndani shuhudia  
 Uonapo vyang'aria , tahadhari vitakula.

Wawapi leo madume, anasa walopapia?  
 Wamepita ja umeme, leo yao sitoria  
 Shime enyi wana shime, bora kumcha Jalia  
 Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula

Nambie faida gani, nambie ipi fidia  
 Upatayo hatimani, waja wakikufukua  
 Ila kufa kama nyani, kasoro yako mkia  
 Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula

Vyatiririka tariri, vina vyanikubalia  
 Alo bora mshairi, pa tamu humalizia  
 Nahitimisha shairi, dua ninawapigia  
 Uonapo vyang'aria , tahadhari vitakula.

Ewe Mola mtukuka, si shaka wanisikia  
 Wakingie wanarika, na anasa za dunia  
 Amina wangu Rabuka, dua yangu naishia  
 Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula.

**MASWALI:**

- a) Ni ujumbe gani wanaopewa vijana kupitia shairi? ( alama 4)
- b) Bainisha tamathali mbili za usemi katika shairi hili. ( alama 2)
- c) Eleza bahari ya shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo.
  - i) idadi ya vipande katika mshororo
  - ii) mpangilio wa vina katika beti.
- d) Eleza mbinu zozote mbili za kishairi zilizotumika katika shairi hili. ( alama 2)
- e) Andika ubeti wa pili kwa lugha nathari ( alama 4)

- f) Eleza toni ya shairi hili. ( alama 1)  
 g) Tambua:  
   i) Nafsi neni ( alama 2)  
   ii) Nafsi nenewa  
 h) Eleza umuhimu wa mbinu ya kimiridhi iliyo tumika katika ubeti wa tano. ( alama 2)  
 i) Eleza maana ya msamiati: aula‘ ( alama 1)

### **SEHEMU B: RIWAYA**

#### **KIDAGAA KIMEMWOZEA : KEN WALIBORA**

#### **JIBU SWALI LA 2 AU LA 3**

2. ``Huyu mwenda wazimu anakuja nini kwenye sherehe hizi? Anafikiri sherehe hizi ni za watu wenye kichaa kama yeeye?“  
 a) Eleza muktadha wa dondo hili. ( alama 4)  
 b) Thibitisha kuwa mrejelewa ni mwendawazimu na vile vile si mwendawazimu. ( alama 16)  
 3 a) Onyesha jinsi mbandishi wa riwaya ya kidagaa alivyoshughulikia nafasi ya vijana katika jamii. ( alama 10)  
 b) Thibitisha kauli kuwa, mla nawe huliwa zamu yake ifikapo , ukirejelea riwaya ya kidagaa kimemwozea. ( alama 10)

### **SEHEMU C: TAMTHILIA**

#### **KIGOGO: PAULINE KEA**

4. ``Tunajivunia kuwa na kampuni kubwa zaidi ya uzalishaji sumu ya nyoka barani.“  
 a) Eleza muktadha wa kauli hili. ( alama 4)  
 b) Andika mbinu moja ya lugha iliyo tumika katika kauli hii. ( alama 2)  
 c) Kwa kutumia mifano mwafaka, onyesha kwa hoja **kumi na nne(14)** jinsi sumu ya nyoka ilivyoathiri eneo la Sagamoyo katika tamthilia ya kigogo. ( alama 14)  
 5. Fafanua jinsi mbandishi wa tamthilia ya kigogo alivyofaulu kutumia mbinu zifuatazo za uandishi.  
 a) Jazanda ( alama 10)  
 b) Majazi ( alama 10)

### **SEHEMU YA D: HADITHI FUPI**

#### **TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE (ALIFA CHOKOCHO NA DUMU KAYANDA)**

#### **TUMBO LISILOSHIBA ( S. A MOHAMMED )**

6. ``Hakuna aliye weza kukiteguu kitendawili chenyewe lakini...“  
 a) Eleza muktadha wa dondo hili. ( alama 4)  
 b) Tambua tamathali ya usemi iliyo tumika katika dondo hili. ( alama 2)  
 c) Fafanua chanzo na hatima ya kitendawili kinachorejelewa katika dondo hili. ( alama 10)  
 d) Eleza wasifu wa warejelewa katika dondo hili. ( alama 4)

### **SEHEMU YA E: FASI HI SIMULIZI**

#### **JIBU SWALI LA 7 AU 8**

7. a) Ulumbi ni nini? ( alama 2)  
 ii) Ulumbi hutekeleza majukumu gani katika jamii?. ( alama 5)  
 iii) Fafanua mambo **manne** yanayomfanya mtu awe mlumbi bora. ( alama 8)  
 b) Eleza namna ambavyo hadhira hulusishwa katika uwasilishaji wa fasihi simulizi. ( alama 5)  
 8 a) i) Eleza sifa **sita** za maghani. ( alama 6)  
 ii) Fafanua aina zozote **nne** za maghani. ( alama 4)  
 b) i) Fafanua majukumu **manne** ya hurafa katika jamii. ( alama 4)  
 ii) Eleza vipengele **sita** vya kuzingatia katika uchanganuzi wa hadithi. ( alama 6)

- Hukuza utangamano , watu wanapokuja pamoja kutambiana hadithi. ( zozote 4 x 1) = 4

- ii) vipengele vya kuzingatia katika uchanganuzi wa hadithi**
- Dhamira – lengo/nia inayokusudiana na hadithi
- Maudhui- mambo yanayoelezwa katika hadithi k.m hekaya
- Ploti – mtiririko wa utushi ama tukio katika hadithi.
- Mandhari- mazingira ya wakati , hali au kimaeneo. Ya kuogofya, yenyenye misitu na majitu au mazimwi.
- Wahusika- viumbe wa hadithi wa aina gani.
- Usimulizi- hadithi inasimuliwa katika nafsi ya kwanza au ya tatu.
- Muundo- miundo maalum ya kuanza na kufunga hadithi
- Lugh- luga ya moja kwa moja( sahili) na inayoweza kutumia tamathali za lugha. ( zozote 6 x 1)= 6

### **BUURI**

**102/1**

### **KISWAHILI**

#### **KARATASI YA 1**

##### **INSHA**

1. Wewe ni mhariri wa Gazeti la Mamboleo. Andika tahariri ukieleza athari za mitandao ya kijamii.
2. Mazingira bora ni muhimu katika maisha ya binadamu. Jadili.
3. Mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani.
4. Nilikuwa nimetoka nyumbani nikielekea mjini, mara nikasikia mngurumo wa radi ulioandamana na umeme..... Endeleza.

### **BUURI**

**102/2**

### **KISWAHILI**

#### **KARATASI YA 2**

##### **LUGHA**

###### **UFAHAMU.**

Dunia inakumbwa na mustakabali finyu sara kuhusu hali yake ya kimazingira. Mabadiliko ya ghafla ya hali ya hewa ambayo tumekuwa tukishuhudia mara kwa mara, yanaashiria hali ya hatari ambayo inakikabili kizazi cha sasa na vile vijavyo.

Kwa miaka kadhaa iliyopita, hali ya anga ingetabirika. Kwa mfano, nyanyangu angeeleza kwa urahisi kuwa msimu wa upanzi ulikuwa kati ya mwezi Machi na Mei. Kwa kauli yake, ni wakati huo ambapo —Miungu walitiririsha machozi ya furaha —kwa jamii. Sasa? Mambo ni tofauti sana.

Kwanza, ghadhabu ya mwanadamu dhidi ya mazingira asilia ndicho kiini kikuu cha madhila tunayoshuhudia. Kasumba dhiafu na tamaa ya maendeleo ilifanya kuvamia chemchemi za maji na kukata miti.

Kinaya cha mwanadamu wa sasa na yule wa zamani ni kwamba, wale wa zamani waliyajali mazingira. Hata ikiwa walikata miti, waliikata na kupanda mingine.

Zaidi ya hayo, kuna miti ambayo haingekatwa, kwani ilichukuliwa kwa uzito mkubwa kama chemchemi ya baraka kwa jamii. Hilo lilihakikisha kwamba, hata ikiwa kulikuwa na ukataji miti, chemchemi muhimu za maji hazikukauka.

Kinyume cha hayo, msukumo wa mwanadamu wa sasa ni tamaa tupu. Hajali wala habali! Kasumba na dhana za kibepari zimemfanya kujipenda, kiasi cha kutoyajali mazingira kwa vyovoyote vile.

Mfano halisi ni uvamizi ambao umefanywa katika misitu muhimu nchini. Katika msitu wa Mau, kuna madai kwamba kundi la wanasiasa —maarufu” waliuvamia na hata kujenga kiwanda cha majani chai. Wengine walitengeneza viwanda nya kusagia mbao za ujenzi.

Hali hii ni sawa na misitu ya Abedares na Mlima Kenya, ambayo imegeuka kuwa kama falme za wakataji miti. Unapopita karibu na misitu hiyo, kitakachokukaribisha ni sauti za mashine za kukata miti, iwe usiku ama mchana. Hawaogopi lolote.

Kwao lengo kuu huwa ni kutimiza —maagizo ya —wakbwaa” wao. Kinaya cha haya yote ni kuwa, baadhi ya watu ambao wamekuwa wakinufaika kwa biashara hii haramu ni wale walio serikalini ambao sauti hazikosi kusikika zikhimiza athari za kukosa kuhifadhi mazingira.

Hivyo, ukweli mtupu uliopo ni kwamba, tumekuwa tukiogelea katika bahari ya hadaa tupu; tunajiumiza sisi wenyewe! Ni kama chachandu anayejipalilia makaa.

Ni dhahiri kwamba suluhisho la majanga haya yote ya kimazingira ni rahisi kuondoa unafiki na tamaa. Tulinde mazingira kutoka kwa nafsi zetu.

#### **MASWALI YA UFAHAMU.**

- (a) Yape makala haya anwani mwafaka. (al.1)
- (b) Taja ishara ya hatari inayokikibili kizazi kipyaa. (al.1)
- (c) Eleza tofauti za mwanadamu wa sasa na wa hapo awali. (al.2)
- (d) Ni hatua zipi ambazo mwanadamu wa hapo awali alizichukua ili kuhifadhi mazingira? (al. 2)
- (e) Binadamu amekuwa ni kama chachandu anayejipalilia makaa. Thibitisha kutoka kwa kifungu. (al.2)
- (f) Mwanadamu wa sasa ana tamaa. Toa mifano mitatu kudhibitisha haya. (al.3)
- (g) Ni suluhisho lipi linalopendekezwa la kumaliza majanga ya kimazingira? (al. 1)
- (h) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika kifungu. (al.3)
  - (i) Haramu
  - (ii) Anayejipalilia makaa
  - (iii) Ghadhabu

#### **(B) UFUPISHO.**

##### **Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Pikipiki za uchukuzi wa abiria, maarufu, boda boda, hupendwa na watu wengi ncini kutokana na unafuu wake pamoja na uwezo wa kupenya mitaani na vijijini ambako magari ya uchukuzi wa umma hayawezi kufika.

Hii ndiyo maana sekta ghii ya uchukuzi imekuwa kwa kasi katika miaka ya hivi karibuni ambapo mwaka jana wahudumu wa bodaboda waliweza kuchuma zaidi ya sh219 bilioni.

Licha ya kiwango hiki cha faida, bodaboda hizi zimekuwa zikitumika kama vyombo nya kurahisisha utekelezaji wa uhalifu katika maeneo mengi mijini na mashambani.

Msemaji wa polisi anasema siku hizi kati ya visa kumi nya wizi katika maeneo ya mijini, sita hutekelezwa na wahalifu wanaosafiri kwa pikipiki hizo wakijifanya wahudumu wa bodaboda. Wahalifu hupenda kutumia pikipiki ili waweze kukwepa maafisa wa polisi katika barabara za miji zenyé misongamano ya magari pamoja na vichochoroni katika mitaa na vijiji. Magari ya polisi hukabiliwa na wakati mgumu wanapowaandama wahalifu wanaotumia pikipiki.

Huenda baadhi ya waendesha bodaboda hushirikiana na wahalifu ambao huwahangaisha wakazi katika miji mikuu nchini.

Lakini wahudumu wa bodaboda wanasema kuwa sio wote huhusika katika visa nya uhalifu. Kiongozi wa wanabodaboda anasema kuna wachache watundu ambao hushirikiana na wahalifu. Alisema wako tayari kuketi na

serikali ya kaunti ya Nairobi na idara ya polisi kukabili ana na wachache mionganoni mwao ambao hudaiwa kushirikiana na wahalifu.

Mkurugenzi wa idara ya ulinzi katika kaunti ya Nairobi alisema maafisa wake wangeendelea kushirikiana na polisi kuendesha operasheni ya kuwaondoa bodaboda na wachuuzi katikati ya jiji katika harakati za kuimarisha usalama .

Baadhi ya pikipiki ambazo hutumika katika uhalifu huwa zinafanana na zile ambazo hutumika kuwasafirisha abiria. Bodaboda hawa, japo si wote, wamegeuka kuwa kizingiti kikuu kwa juhudhi za kudhibiti usalama haswa katikati mwa jiji. Wahalifu huwatumi kutoroka baada ya kuwaibia wafanyabiashara na hata wapiti njia.

Mbunge wa starehe aliwasilisha kesi mahakamani kupinga marufuku ya bodaboda katikati mwa jiji. Alidai sharti kuwe na mashauriano kabla ya tendo hilo kutekelezwa.

Katika kaunti za pwani visa kadhaa vimeripotiwa ambapo wahalifu, wenyewe silaha wamekuwa wakiwashambuliwa watu mchana na kuwapora, kisha kutoroka kwa pikipiki za bodaboda.

Wahudumu wa bodaboda pia wamekuwa wakichukua sheria mikononi mwao kwa kuharibu magari yanapohusika katika ajali na mmoja wao.

Kwa mfano, mapema mwaka huu walichoma basi la kampuni ya Simba coach huko Malindi. Hii ni baada ya basi hilo kugonga mwanabodaboda mmoja na kumuua katika bararabra ya Malindi – Mombasa.

Ni mnamo Desemba mwaka jana wahudumu hao katika kaunti ya Homa Bay walichoma basi jingine la abiria lililohusika katika ajali na mmoja wao. Basi hilo la kampuni ya Otange lilikuwa limeshusha abiria ndipo mwanabodaboda akaligonga kutoka nyuma na akajeruhwi. Wenzake walifika hapo kwa wingi na kuliteketeza basi hilo. Zaidi ya abiria 20 waliokuwa ndani ya basi hilo walitoroka kupitia madirisha kuokoa maisha yao.

**Maswali.**

- (a) Jadili mzozo kati ya msemaji wa polisi na wanabodaboda kuhusu uhalifu mijini. **(maneno 90 – 100) al. 8,1)**  
(b) Fupisha aya za mwisho nne. **(maneno 40- 45) al.5,1)**
- C) MATUMIZI YA LUGHA. (AL.40)**
- (a) (i) Taja konsonati mbili zinazotamkiwa katika kaakaa gumu. **(al.2)**  
(ii) Sauti ulizotaja hapo juu ni za aina gani? **(al.2)**
- (b) Shadda ni nini? **(al.1)**  
(i) Weka shadda katika maneno yafuatayo. **(al.2)**  
    Ua  
    Kiwakilishi
- (c) Tunga sentensi mbili kuonyesha dhana tofauti zinazobainishwa na kiimbo. **(al.2)**  
(d) (i) Kiambishi ni nini? **(al.1)**  
(ii) Ainisha mofimu katika neno lifuatalo. **(al.3)**  
    Kilicholiwa.
- (e) Bainisha maneno katika sentensi ifuatayo. **(al.3)**  
    Kumbe mtu mfupi anarukia lile zuri.
- (f) Maneno yafuatayo yamo katika ngeli gani. **(al.2)**  
(i) Wembe  
(ii) mnyoo
- (g) Andika sentensi ifuatayo kwa ukubwa wingi.  
    Ngamia alibeba hema lililotengenezwa kwa ngozi ya chui. **(al.3)**  
(h) Tunga sentensi inayodhahirisha matumizi ya „O“ rejeshi tamati. **(al.2)**  
(i) Onyesha hali iliyotumika katika sentensi ifuatayo. **(al.1)**  
(i) Mganga aonekana akiwa uchi.  
(ii) Kanusha. **(al.1)**

- Ningekuwa kasisi ningewafanya mwende mbinguni.
- (j) Eleza matumizi mawili ya kiambishi -ji- (al.2)
- (k) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya visanduku. (al.4)  
Ng‘ombe akamuliwaye atachinjwa kesho.
- (l) Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi. (al.3)  
Mtaalamu alituambia kuwa kusoma kwa mapana kungepalilia ubunifu wa wanafunzi hao wao.
- (m) Andika maneno yafuatayo katika kauli ulizopewa mabanoni. (al.2)  
(i) Fumba (tendata)  
(ii) Kwaa (tendama)
- (n) Tunga sentensi mbili tofauti kudhihirisha maana mbili za kitawe \_somo‘. (al.2)
- (o) Tambua shamirisho na chagizo katika sentensi hii. (al.2)  
Juma alimjengea nyanya nyumba kwa mawe vizuri sana.
- (D) ISIMU JAMII. (AL.10)**
- a) Eleza istilahi zifuatazo za isimu jamii. (al.4)  
(i) Lugha ya taifa.  
(ii) Lugha sanifu.  
(iii) Lugha rasmi.  
(iv) Lahaja.
- (b) Fafanua maswali sita yanayochangia kustawi kwa lugha ya Kiswahili nchini Kenya. (al.6)

for free past papers, visit: [www.freekcsepastpapers.com](http://www.freekcsepastpapers.com)

Soma ushairi ufuatao kisha ujibu maswali.

Ulimwengu ulimwengu, ulimwengu naratibu  
 Yaliyo kichwani mwangu, nataka kuyahutubu  
 Wayasome ndu zangu, wa mbali na wa karibu  
 Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ulimwengu ni kiwanja, cha wenye raha na tabu  
 Wengine wanajikonja, kwa wengine ni adhabu  
 Kucha na kutwa twahanja, kutafuta matulubu  
 Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa balaa, aliniusia babu  
 Mna mambo yamejaa, ya faraja na kusibu  
 Na machache ya kufaa, ila mengi ya udubu  
 Cha weye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni kiwanja cha Amina, Saidi Ali Rajabu.  
 Wengine kitu hatuna, tunaishia kababu  
 Wale wamejaza sana, wanashindwa kuhesabu  
 Cha wenye raha na tabu, Ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa urongo, na kweli pia ajabu  
 Kichwa hudanganya shingo,tumbo kiuno chasibu  
 Usitumai ubongo, wa nduguyo na swahibu  
 Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa walevi, pombe kwao ni dhahabu  
 Mara vile mara hivi, wakilewa majudhubu  
 Maneno ya kiujuvi, hujipaka hata shabu  
 Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni kiwanja wenye dini, wamtiio wahabu  
 Mashekhe msikitini, humo humfanya muhibu  
 Mapadiri kanisani, huvhubiri vitabu  
 Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja

Ni uwanja wa malofa, lofa mtu mwenye tabu  
 Kusema sana kashifa, na moyo kisebusebu  
 Tunakaribia kuja, kwa kushidwa kujimudu  
 Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa faraja, alowajali habibu  
 Na wengine sitotaja, msinambe ninagubu  
 Ni uwanja wa viroja, vigumu kuvikutubu  
 Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

**Maswali:**

- (a) Lipe shairi hili anwani ifaayo. (al.1)
- (b) Kwa kutoa mfano, eleza mbinu zozote mbili za lugha zilizotumika katika shairi. (al.2)
- (c) Eleza jinsi uhuru wa mshairi ulivyotumika katika shairi. (al.2)
- (d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha tutumbi. (al.4)
- (e) Taja na ueleze bahari zozote mbili zilizotumika katika shairi hili. (al.2)
- (f) Eleza umbo la shairi hili. (al.4)
- (g) Eleza toni ya shairi hili. (al.1)
- (h) Fafanua dhamira ya mshairi. (al.2)
- (i) Eleza maana ya msamia ufuatao kama ulivyotumika katika shairi. (al.2)
- (ii) Malofa
- (iv) Udubu

**SEHEMU B.****TAMTHILIA****KIGOGO – JIBU SWALI LA 2 AU 3.**

2. —Kitbu si jalada, fungua ndani usome mambo. Kitanda usichokilalia kunguni wake huwajui.”
- (i) Eleza muktadha wa dondo hili. (al.4)
- (ii) Kwa kurejelea tamthilia ya kigogo, thibitisha ukweli wa dondo hili. (al.14)
- (iii) Taja tamathali za usemi zilizotumika katika dondo hili. (al.2)
3. Eleza mbinu alizotumia majoka kuendeleza uongozi wake. (al.20)

**SEHEMU C:****RIWAYA – KIDAGAA KIMEMWOZEA****Jibu swali la 4 au 5.**

4. — W bwana unafikiri ninatumia petroli nini?”
- (a) Weka maneno haya katika muktadha wake. (al.4)
- (b) Eleza sifa nne za msemewa. (al.4)
- (c) Fafanua jinsi mwandishi wa kidagaa kimemwozea amewasawiriwanawake. (al.12)
5. Jadili jinsi mbinu zifuatazo zimetumiwa na mwandishi kufanikisha kazi yake.
- (i) Sadfa (al.20)
- (ii) Mbinu rejeshi.

**SEHEMU D****HADITHI FUPI.****TUMBO LISILOSHIBA.**

6. Huku ukirejelea hadithi ya Tumbo Lisiloshiba na Shibe Inatimaliza, fafanua maudhui ya ukiukaji wa haki. (al.20)

**SEHEMUE.****FASIHI SIMULIZI – JIBU SWALI LA 7 AU 8.**

7. (a) Eleza maana ya miviga. (al.2)
- (b) Fafanua sifa za miviga. (al.4)
- (c) Eleza udhaifu wa miviga. (al.2)
- (d) Toa maana ya ulumbi. (al.2)
- (e) Ni nini umuhimu wa ulumbi . (al.8)

**8. SOMA KIFUNGU KIFUATACHO KISHA UJIBU MASWALI.**

5. Ndugu !  
Umeenda?  
Wewe nenda  
Wewe nenda  
Wewe nenda  
Mungu atakutunza

6. Wewe Safiri  
Wewe safari  
Wewe safari  
Maisha ni moshi  
Hata si tu safarini.

7. Ndugu!  
Tulikupenda  
Tulikupenda  
Tulikupenda  
Na Maulana kakupenda zaidi

8. Oooh!  
Ndugu  
Wewe nenda  
Wewe nenda  
Wewe nenda  
Siku yetu ikifika  
Tutapaa ka malaika  
Mungu akurehemu.

**Maswali .**

- |   |        |
|---|--------|
| (e) Huu ni utungo wa aina gani.                               | (al.2) |
| (f) Fafanua sifa bainifu za utungo huu.                       | (al.8) |
| (g) Tambua tamathali za usemi zilizotumika katika utungo huu. | (al.4) |
| (h) Ni vipi utungo kama huu ni muhimu katika jamii.           | (al.6) |

**CEKENA****102/1****KIDATO CHA NNE  
KARATASI YA INSHA****Swali la kwanza ( lazima)**

1. Wewe ni katibu wa kamati ya wataalamu wanaoshughulikia jinsi ya kukabiliana na uhaba wa maji. Andika kumbukumbu za m Kutano wenu. (alama 20)
2. Hatua ya serikali kuu kumpa kila mwanafunzi wa darasa la kwanza tarakilishi ni ya manufaa sana. Jadili (alama 20)
3. Mwenye kovu usidhani kapoa. (alama 20)
4. Lo! Jambo lililotendeka katika makazi ya jirani yetu usiku huo liliwa la kutisha sana. Kumbe baba watu alikuwa amegeuka kuwa hayawani. Hayawani mla watu..... (alama 20)

**CEKENA****102/2****KIDATO CHA NNE  
LUGHA****1. Ufahamu: ( alama 15)****Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.**

Binadamu anazidi kuibuka na mbinu mbalimbali za kuboresha maisha yake. Hapo awali, maisha yake yalikuwa duni kama wanavyodai wanahistoria katika nadharia. Wanadai kwamba binadamu alipitia hatua nyingi za ukuaji wake. Kumekuwa na maendeleo yanayokusudia kuboresha maisha ya binadamu. Nchi zilizo katika ulimwengu wa kwanza, hasa za magharibi ndizo zinaongoza katika juhudhi hizi.

Moja kati ya sekta ambazo zimeshamiri sana, ni ile ya kiteknolojia. Teknolojia ni maarifa ya kisayansi yaliyowekwa katika matumizi ya vitu. Binadamu amenawiri sana katika kuboresha maisha yake kwa kutumia teknolojia. Usafiri umeimarika si haba. Binadamu anaweza kusafiri masafa marefu kwa muda mfupi sana. Anaweza kuabiri ndege hapa Nairobi na baada ya saa chache tu atakuwa ametua katika uwanja wa ndege wa kimataifa, Dar-es-salaam, Tanzania.

Uchumi pia umekua kupitia kwa teknolojia. Viwanda vingi vimejengwa kutumia tecknolojia ya kisasa na kuzalisha bidhaa tele ambazo huuzwa katika mataifa ya kigeni na hivyo kujipatia pesa za kuboresha uchumi wa nchi.

Mawasiliano duniani yameboreshwa kupitia teknolojia. Tarakilishi, rununu, televisheni, tovuti, redio na barua pepe ni baadhi ya njia za kuwasiliana zinazohusu teknolojia. Watu wanawasiliana na kukuza urafiki wao kupitia mbinu hizi za mawasiliano. Habari zinapitishwa kupitia televisheni na redio kwa kutumia mitambo ya kisasa iliyokuzwa na teknolojia.

Fauka ya hayo, miundo msingi imeboreshwa kwa kiasi kikubwa na teknolojia ya kisasa. Barabara kuu ya Thika ni mfano wa kazi nzuri iliyofanywa kwa kuzingatia teknolojia anuwai. Licha ya utata unaokumba mradi wa reli uliozinduliwa na rais kutoka Mombasa hadi mataifa jirani, teknolojia hii ya usafiri inanuiwa kuboresha uchukuzi na kuiletea nchi hii utajiri mkubwa.

Hata hivyo, hakuna chema kisichokuwa na dosari. Usalama umepungua kwa kiasi kikubwa kupitia teknolojia. Kisa cha hivi majuzi cha Westgate ambapo magaidi waliwaua raia zaidi ya sabini, kilitokana na kutumia teknolojia. Magaidi hao walitumia bunduki za kisasa katika tukio hilo haramu. Fauka ya hayo walitumia simu kuwasiliana ili kutimiza tendo hilo la kihayawani.

Maadili katika jamii yamezorota kwa kiasi kikubwa kupitia teknolojia. Vijana wengi hutumia muda wao mrefu wakitatama filamu za kuudhi katika mitandao iliyoboreshwa kiteknolojia. Picha hizi huwa ni kero hata kwa maisha yao ya baadaye kwa sababu madhara ya picha hizo huwafuata na kuwadhuru hata waingiapo katika ndoa.

Kuongezeka kwa joto ulimwenguni na kubadilika kwa hali ya hewa kunatokana na maendeleo ya kiteknolojia. Zilizala za kila mara, vimbunga, pamoja na matukio kama Tsunami hutokana na uchafuzi wa mazingira unaochangiwa sana na teknolojia. Jambo hili limesababisha mabadiliko ya hali ya hewa kwa kiasi kubwa.

Ni jukumu la kila mtu kujizatiti katika kutahadhari na athari za kiteknolojia na kuboresha maisha yao bila kujingiza katika maovu yanayotokana na teknolojia.

**Maswali ya ufahamu**

1. Toa anwani mwafaka ya kifungu hiki (alama 1)
2. Kwa nini mwanadamu anathamini sana maendeleo (alama 2)
  
3. Teknolojia imeimarishaje usafiri (alama 2)
4. Uchumi unaimarikaje kupitia teknolojia ya kisasa? (alama 2)
5. Mawasiliano yana umuhimu gani? (alama 2)
6. Jadili madhara mabaya ya teknolojia (alama 3)
7. Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika taarifa (alama 3)
  - (i) Duni
  - (ii) Shamiri
  - (iii) Zilizala

## **2. Ufupisho. (alama 15)**

### **Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali**

Mfumo wa elimu nchini unatilia mkazo mafunzo mengine ambayo, japo yamo nje ya masomo ya kawaida, yanahusiana na kwenda sambamba na masomo hayo ya kawaida. Vyama vya wanafunzi shulen vinachangia pakubwa kupitisha mafunzo haya ya ziada.

Vyama vya wanafunzi hutofautiana kulingana na majukumu. Mathalani, vipo vyama vya kidini, vya kitaaluma na vya michezo. Pia, kuna vyama vya kijamii kama vile Chama cha Kupambana na Matumizi Mabaya ya Dawa na vya kiuchumi kama vile Chama cha Wakulima Chipukizi.

Imadhihirika kwamba vyama vya wanafunzi vina **manufaa ya kuhusudiwa**. Hii ndiyo sababu shulen, kila mwanafunzi anahimizwa kujiunga na angaa vyama viwili. Vyama vya wanafunzi huwasaidia kukuza vipawa na kuimarisha stadi za kujieleza. Haya hufikiwa kupitia kwa shughuli za vyama kama vile ukariri wa mashairi, mijadala, utegaji na uteguaji vitendawili, chemsha bongo na ulumbi. Aidha, vyama hivi huhimiza utangamano miongan mwa wanachama kwani wao hujiona kuwa watu wenye mwelekeo mmoja. Vilivile utangamano wa kitaifa na kimataifa hujengeka.

Mwanafunzi ambaye amejiunga na vyama vya wanafunzi huweza kukabiliana na changamoto za maisha kwa urahisi kuliko Yule ambaye hajawahi kujiunga na chama chochote. Katika vyama hivi, wanafunzi hufunzana mikakati na maarifa ya kutatua matatizo na mbinu za kuepuka mitego ya ujana. Kupitia kwa ushauri wa marika kwa mfano, mwanafunzi hushauriwa kuhusu masuala kama vile uteuzi wa marafiki, kuratibu muda, kujikubali na kuwakubali wenzake.

Hali kadhalika, mwanafunzi hujifunza maadili ya kijamii na kidini. Kupitia kwa vyama vya kidini na vinginevyo, ye ye hujifunza kujistahili na kuwa na stahamala ya kidini, kiti kadi na kikabilia. Kadhalika, majukumu ambayo mwanafunzi huenda akapewa hupalilia uwajibikaji, uaminifu na kipawa cha uongozi. Hata anapohitimu masomo yake, mwanafunzi huyu huendeleza sifa hizi.

Vijana wana nafasi kubwa katika kukabiliana na maovu ya kijamii kwani wao ndio wengi zaidi. Kupitia kwa vyama hivi, wanafunzi wanaweza kuwahamasisha wenzao dhidi ya tabia hasi kama vile kushiriki mapenzi kiholela, ulanguzi wa dawa za kulevyo na kujilingiza katika burudani zisizofaa. Pia, shughuli na miradi ya vyama hivi huwawezesha wanafunzi kutumia nishati zao kwa njia ya kujinuafisha na kuepuka maovu. Kwa mfano, wanaweza kwenda kukwea milima, kufanya matembezi ya kukusanya pesa za kuwafadhili wahitaji, kuendeleza shughuli za kunadhifisha mazingira na kutembelea vituo vya mayatima na wazee.

Kushiriki katika vyama vya michezo hakumwezeshi mwanafunzi kuimarisha afya na kujenga misuli tu, bali pia huweza kuwa msingi wa kupata chanzo cha riziki baadaye. Wapo wachezaji maarufu amba walitambua na kuvienda leza vipawa vyao kupitia kwa vyama aina hii, na hivi sasa wana uwezo wa kuyaendesha maisha yao na ya familia zao.

Ifahamike kuwa vyama vya wanafunzi vinapaswa kuwa msingi wa mshikamano na maridhiano. Visitumiwe kama vyombo vya kuwagawa wanafunzi kitabaka. Mwanafunzi hana budi kusawazisha muda anaotumia. Atenge muda wa shughuli za vyama na wa kudurusu masomo yake.

### **Maswali**

- (a) Fupisha ujumbe wa aya tano za kwanza kwa maneno 80 (alama 9, 1 utiririko)
- (b) Fafanua masuala ambayo mwandishi anaibua katika aya tatu za mwisho (maneno 60)(alama 6, 1 utiririko)

## **3. Matumizi ya Lughu**

- a) Eleza tofauti ilipo kati ya sauti /e/ na /u/ (alama 2)
- b) Onyesha muundo wa silabi ya kwanza katika maneno yafuatayo. (alama 2)
  - (i) Ng‘arisha
  - (ii) Nzi

- c) Ainisha vipashio vya kisarufi katika sentensi ifuatayo. (alama 3)  
 Amenifia
- d) Andika katika kauli yakinishi (alama 2)  
 Hatakuja tusipomuarifu mapema
- e) Geuza katika usemi halisi (alama 3)  
 Mwanafunzi alishangaa na kusema kuwa hakuamini alipata alama nyingi  
 vile katika insha.
- f) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali (alama 4)  
 Yule mwandishi aliyeshinda tuzo ni maarufu sana.
- g) Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo (alama 3)  
 Mtoto alipikiwa chai na mamake kwa sufuria chafu.
- h) Tunga sentensi mbili kubaini matumizi mawili tofauti ya Mkwaju (alama 2)
- i) Unda nomino mbili mbili kutohana na vitenzi vifuatavyo (alama 2)  
 (i) Jaribu -  
 (ii) Chuma –
- j) Onyesha matumizi ya kwa‘ katika sentensi ifuatayo. (alama 2)  
 (i) Ameenda kwa Musa  
 (ii) Alipata alama saba kwa kumi
- k) Nyambua katika kauli zilizo mabanoni (alama 2)  
 (i) Tua (Tendama)  
 (ii) Pwa (Tendeka)
- l) Andika katika udogo wingi (alama 2)  
 Ndovu wa kiafrika ameharibu mboga shambani
- m) Tunga sentensi kudhihirisha maana ya maneno yafuatayo (alama 2)  
 Susuwaa  
 Zuzuwaa
- n) Onyesha kijalizo katika sentensi ifuatayo. (alama 1)  
 Yeye ni mwizi
- o) Bainisha vishazi katika sentenzi ifutayo (alama 2)  
 Aliyempeleka mjini, amemwajiri kazi
- p) Tumia kivumishi –pi pamoja na ngeli ya YA-YA kutunga sentensi (alama 2)
- q) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kufuata maagizo (alama 2)  
 Kupanda mchongoma, kushuka ndio ngoma  
 (Anza kwa) kushuka
- r) Ainisha virai. (alama 2)  
 Mzee alilala kando ya barabara

### Isimujamii

- a) Eleza mambo yaliyochangia katika maenezi ya Kiswahili katika Afrika Mashariki kabla ya uhuru (alama 5)
- b) Eleza sifa tano za lugha rasmi. (alama 5)

**CEKENA**

102/3

**FASIHI****SEHEMU A:****TAMTHILIA; KIGOGO Pauline Kea****LAZIMA**

—Utaka wahamie wapi siku kama hizi? Wamekuja kuuguza majeraha yao ya kufungiwa soko.”

- a) Weka maneno haya katika muktadha wake. (alama 4)
- b) Tambua mbinu mbili za lugha katika dondoo hili (alama 2)
- c) Kando na kufungiwa soko, Wanasmayo wanauguza majeraha yepi mengine yanayosababishwa na utawala wa Majoka (alama 5)
- d) Fafanua sifa za msemaji wa dondoo hili. (alama 9)

**SEHEMU B:****KIDAGAA KIMEMWOZEA**

Jibu swali la 2 au la 3

2. —Huy Msichana wa Kibri atakiona cha mtema kuni”
- a) Fafanua umuhimu wa msichana anayerejelewa katika kukuza msuko wa riwaya. (alama 5)
  - b) Tambua maudhui yanayojitokeza katika dondoo hili (alama 1 )
  - c) Kwa kutumia hoja kumi na nne thibitisha vile maudhui uliyotaja yanavyojitokeza kwingineko riwayani (alama 14)
3. Kwa kurejelea wahusika wowote kumi katika riwaya hii, thibitisha kuwa wao ni vielelezo muhimu katika jamii (alama 20)

**SEHEMU C: HADITHI FUPI****TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE**

4. —hbu sikiza jo! Pana hasara gani nzi kufia kidondani?
- a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
  - b) Tambua mbinu tatu za lugha zilizotumika katika dondoo hili na umuhimu wake (alama 6)
  - c) Onyesha jinsi dhana ya nzi kufia kidondani inabainika hadithini (alama 4)
  - d) Hali ya kutowajibika inajitokeza vipi katika hadithi? (alama 6)
5. Huku ukirejelea diwani ya Tumbo lisiloshiba fafanua matatizo yanayokumba vijana katika jamii (alama 20)

**SEHEMU D: FASIH SIMULIZI**

1. a) Miviga ni nini? (alama 2)  
b) Eleza sifa sita za miviga (alama 6)  
c) Miviga inafaaa kupigwa marufuku katika jamii ya kisasa. Thibitisha kauli hii kwa kutoa hoja saba (alama 7)
2. Taja mifano mitano yangomezi za kisasa (alama 5)

**SEHEMU E: USHAIRI**

(ALAMA 20)

**Jibu swali la 7 au 8****MBONA KITANZI JITIA?**

1. Moyongu utungu jaa, mwana wewe kulegea  
Yako masomo puzia, uzembe umezidua  
Muda wako yoyomea, maishayo wahinia  
Kitanzu unajitia, utakuja kujutia.
2. Tabia zako potoka, yako matendo udhia  
Penzi penzi taka, masomoyo puuzia  
Wewe umedanganyika, maisha jiharibia  
Kitanzu unajitia, utakuja kujutia.
3. Kingi kiu kakupata, mvinyo unabugia  
Uchu wadai wakata, vilabuni kahamia  
Yako afia wakata, masomo yako umia  
Kitanzu unajitia, utakuja kujutia.

4. Tawa tawa watumia, maisha yako kakwama  
Darahimu wachomea, mkuki umejichoma  
Makaa wajipalia, matokeo yako zama  
Kitanzi unajitia, utakuja kujutia.
5. Wazazi wako kachoka, peso unaharibia  
Zao nyoyo zahinika, yao bidii potea  
Mienendo badilika, laana kuepukia  
Kitanzi unajitia, utakuja kujutia.
6. Sita beti tamatika, mengi mi' kakunenea  
Yote maovu ukazika, kaburi kukomea  
Masomoni makinika, mema maisha andaa  
Kitanzi unajitia, utakuja kujutia.

### MASWALI

1. Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili (alama 2)
2. Taja na ueleze tamathali mbili za usemi ambazo zimetumiwa na mwandishi (alama 4)
3. Andika umbo la shairi hili (alama 4)
4. Eleza uhuru wa mshairi ambao umetumiwa na mshairi (alama 4)
5. Mshairi analalamikia mambo gani? (alama 4)
6. Liweke shairi hili katika bahari tofauti tofauti kwa kurejelea kigezo cha (alama 2)
  - a) Vina
  - b) Ujumbe

### AU Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali

Kila nikaapo husikia tama  
Na kuwazia hali inayonizunguka

Huyawazia madhila  
Huziwazia shida  
Hujiwazia dhiki

Dhiki ya ulezi  
Shida ya kudhalilishwa kazini  
Madhila ya kufanyiwa dharau  
Kwa sababu ya jinsia ya kike  
Hukaa na kujidadisi  
Hujidadisi kujua ni kwa nini  
Jamii haikisikii kilio changu  
Wezangu hawanishiki mikono  
Bali wanandharau kwa kuikosea utamaduni

Hukaa na kujiuliza  
Iwapi raha yangu ulimwengu huu?  
Iwapi jamaa nzima ya wanawake?

### Maswali

- a) Taja sifa mbili za shairi huru zinazojitokeza katika shairi hili (alama 2)
- b) Eleza dhamira ya mshairi (alama 2)
- c) Kwa kutoa mifano, eleza maana ya mistari mishata (alama 3)
- d) Bainisha tamathali mbili za usemi zilizotumika katika shairi hili (alama 4)
- e) Eleza nafsineni katika shairi hili (alama 2)
- f) Tambua toni ya shairi hili (alama 2)
- g) Taja maudhui matatu katika shairi hili (alama 3)

- h) Eleza maana ya msamiai ufuatao kama ulivytumiwa katika shairi (alama 2)
- (i) Madhila
  - (ii) Kudhalilishwa

for free past papers, visit: [www.freekcsepastpapers.com](http://www.freekcsepastpapers.com)

## **WESTSCENT KISWAHILI**

Karatasi ya Kwanza

(INSHA)

### **1. LAZIMA**

- Katika ofisi ya ubalozi wa Kichina, kuna nafasi ya kufundisha wageni kazi fupi ya Kiswahili na Kiingereza. Andika Tawasifu utakayoambatanisha na ombi lako.
2. Mvua ya masika imeleta hasara nyingi hapa nchini kuliko faida. Jadili.
  3. Andika kisa kinachothibitisha ukweli wa methali, Kutangulia sio kufika.
  4. Mara tu nilipovuka daraja la ule mto, nilijua kwamba maisha yangu yalikuwa yanachukua mkondo mpya....

## **WESTSCENT EXAMINATION**

**102/2**

### **KISWAHILI**

**Karatasi 2**

#### **1. UFAHAMU**

**Soma taarifa ifuatayo kasha ujibu maswali yanayofuata.**

Wahenga walisema kutoa ni moyo usambe ni utajiri. Iwapo wangefufuka leo hii wangeongezea kuwa ujasiri ni moyo usiseme ni umri. Kauli hii kama ile ya kwanza imesheheni ujumbe muhimu. Katika jamii nyingi, mtoto haruhusiwi kukaa au kuzungumza mbele ya watu wazima. Akiwa wa kike ndiyo basi. Ni ajabu basi kwa mtoto wa kike kutoka jamii yenye imani kali za jadi zinazomduunisha mwanamke kuweza kupata tuzo yenye staha ya juu zaidi.

Malala Yousafzai alishinda Tuzo ya Nobel mwaka 2014, akiwa na umri wa miaka 17. Aliyeshinda naye tuzo hii adhimu ni Kailash Satyarthi. Kigoli huyu alituzwa tunu hii kwa kupigania haki za wasichana

kupata elimu nchini Pakistan. Harakati hizi hakuzianza juzi. Mwaka 2012 alipigwa risasi na mijibaba ya ugaidi la kundi fulani, linaloegemea mrengo wa siasa kali kwa „hatia“ za kuwatetea mabanati. Inasemekana alishambuliwa alipokuwa akisafiri kwenye mtandao wa shirika la Utangazaji la BBC alilokua akichangia maandishi alipokuwa na umri wa miaka 11. Maandishi yake yalikuwa na ujumbe wa kupinga juhudhi za makundi Fulani kuwanyima wanawake elimu.

Haikuwezekana hata baada ya kupona kurudi pakistani. Alihamia Uingereza alipofadhiliwa na wahisani. Licha ya kuwa aliishi ugenini na bila aila yake mwana huyu hakupoteza makali ya ari yake ya kielimu ya wenzake wa kike.

Yeye ndiye mwenye umri wa chini zaidi katika historia kupata tuzo hili. Baadhi ya wale walioshinda Nobel katika umri mkubwa ni Desmond Tutu, Nelson Mandela na Wangari Maathai. Kila mmoja wao alitambuliwa kwa sababu mahususi zinazohusu jitihada za kuboresha maisha ya wanajamii.

Njia nyingine kuu aliyoitumia Malala ni hotuba. Mwaka 2013 alihutubia kongamano la vijana la umoja wa mataifa katika hafla iliyoandaliwa kwa heshima yake. Aliwashangaza wengi kwa ufasaha na uwezo wake wa kutongoa hoja. Kila mtu aliguswa na dharti ya kauli zake. Katibu mkuu hakuwa na jingine ila kulipa kongamano hilo jina Malala. Mtoto huyu wa kimaskini alipewa taadhima ambayo watu wachache sana wamepata kutunukiwa. Hii, ni heshima inayotengewa marais na wafalme. Na wanapoipata huruhusiwa kuhutubia kwa dakika tano tu.

Mwaka 2014, viongozi wenyе sifa za ubabe wa kuwabinya wapinzani wao lakini wameshindwa kuwaokoa wanyonge walipokuwa wakilaza damu, yeye alisafiri hadi Naijeria kudai kuachiliwa kwa wasichana 200 waliotekwa nyara na kundi haramu. Katika hotuba iliyojaa hisia ambazo huhushishwa tu akina mama wenyе uzazi mkubwa aliyoitoa

Naijeria, aliwaasa watoto wenzake wasimruhusu mtu yejote awaambie kuwa wao ni wanyonge au hawana uwezo. Aliwanasihi kuwa wao sio wadhaifu kuliko wavulana na wasijione wanyonge kuliko watoto wa kitajiri wala wale wanaotoka nchi zenye uwezo mkubwa. Alihitimisha kwa kuwahimiza kuwa wao ndio watakaoijenga jamii na kuwa wana uwezo wa kuyaendesha mambo.

Mshindi wa tuzo hii yenye thamani ya dola za kimarekani milioni moja ameitaraku kwa watoto wenzake ulimwenguni. Bila shaka mwanzilishi wa tuzo ya Nobel ameguswa na tendo la mtoto huyu huko kuzimuni. Kama kumbukizi tunu hii hutolewa wakati wa kuadhimisha kifo cha Mwanaviwanda wa Kiswidi aliyeasisi tuzo hii kufuatana na wosia wake mwaka 1895. Kama Alfred Nobel mwenyewe, kwake Malala, ngwenje au darahimu si muhimu. Lililo muhimu ni ukombozi wa watoto na hasa wa kike kielimu. Malala bado anavaa mtandio wake huku

akidhibhirisha adabu na unyenyekevu wa kupigiwa mfano.

### **MASWALI**

1. Jamii ya Malala ina mtazamo upi kuhusu watoto wa kike? Ukrejelea aya mbili za kwanza, eleza. (alama 3)
2. Unafikiria Malala alistahili kutuzwa Tuzo ya Nobel? Fafanua kwa kutoa hoja kutoka aya mbili za kwanza. (alama 4)
3. Kwa kurejelea aya ya pili hadi nne bainisha njia alizotumia Malala kutetea haki ya watoto wa kike kupata elimu (alama 3)
4. Kwa nini inasemekana kuwa tuzo ya Nobel ina staha ya juu zaidi? (alama 3)
5. Andika visawe vya maneno yafuatayo.
  - a. Tunu
  - b. Ubabe.
  - c. Aliwanasihi

### **2. Ufupisho**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.***

#### **Manufaa ya taka**

Mirundiko ya taka pamoja na utaratibu usiofaa wa uzoaji wake ni tishio kubwa kwa siha ya uma pamoja na mazingira. Hii ni kwa kuwa taka huwa ni makaazi ya wadudu na wanyama waharibifu kama nzi, mbu, kombamwiko na panya ambaa hueneza magonjwa na kuharibu vitu vyenye thamani. Maji taka nayo, pamoja na mifuko ya sandarusi, huwa na maskakimu ya wadudu na virusi vinavyoleta magonjwa mbalimbali.

Mifuko ya sandarusi ina madhara zaidi kwa kuwa huziba mitaro ya maji na kuzuia upitaji wa maji.

Madhara hutokeza wakati wa mvua za gharika. Maji hukosa njia yake ya kawaida ambayo huwa imezibwa na mifuko hii. Maji haya husababisha mafuriko ambayo huleta hasara ya mali na wakati mwengine ya uhai. Fauka ya hayo, mifuko hii huwasakama tumboni wanyama sio wa nyumbani tu, bali wa porini na majini.

Kwa sababu ya hatari zitokanazo na taka, pana haja ya kutafuta njia na teknolojia ya kuweza kukabiliana na tatizo hili ili kuyatunza mazingira na siha ya uma. Njia mojawapo ya kufanya hivi ni

Kuelimisha na kuhimiza uma kuwa na uangalifu katika matumizi ya bidhaa na raslimali ili kupunguza

uzalishaji wa taka. Matumizi ya bidhaa kwa njia ya ubadhirifu huwa chanzo cha uzalishaji wa taka kwa wingi. Kwa mfano, maji ni raslimali ambayo imendelea kutumiwa kwa ubadhirifu na hiyo huzalisha maji taka kwa wingi. Raslimali hii inaweza ikatumia kwa nia endeleu. Kwa mfano, badala ya kutumia bafu ya manyunu kuogea, mtu anaweza kutumia maji ya karai.

Watu wengi huchukulia taka kuwa kitu kisicho na manufaa yoyote. Hawajui kuwa kwa kutumia teknolojia endelezi, taka nyingi zinaweza zikageuzwa na kuwa na manufaa mengi. Vijana wadogo sehemu za mashambani wanahitaji pongezi kwa kuwa na utambuzi na mifuko ya sandarusi kutengenezea mipira wanayoitumia kuchezee. Hii ni teknoloji endelezi ambapo taka hugeuzwa na kuwa na manufaa.

Baadhi ya wananchi wenge ubunifu nao wameanzisha miradi ya kuzoa takataka kutoka majumbani mwa watu kwa ada. kisha huzipeleka taka hizi kule zitakako badilishwa ili ziwe bidhaa za plastiki kama matangi, mitungi, sapatu na champali. Taka hizi huwa malighafi ya kutengenezea bidhaa nyingine.

Taka za chupa na chuma nazo huuzwa katika viwanda vinavyozigeuza kuwa na manufaa tena. Taka za karatasi hutumiwa kutengenezea bidhaa kama vitabu, katoni, shashi za chooni na magazeti.

Taka zinaweza pia kugeuzwa kuwa zenye faida kuzitumia kufanya mboji. Ni muhimu kutambua kuwa si kila aina ya taka inaweza kutumiwa hapa. Taka zinazowenza kufanyiwa mboji ni zile ambazo huoza kwa haraka kama vile mabaki ya vyakula, mboga na matunda. Kwa sadfa, hizi ndizo taka zinazozalishwa zaidi siku hizi na hasa sehemu za mijini na katika maeneo ya biashara kama mikahawa na hospitali.

Mtu akiwa na nafasi anaweza kuchimba shimo ambalo atafukia taka hizi ili kutengeneza mbolea.

Hii ni njia isiyodhuru mazingira na yenye manufaa kemkem. Kwanza, hugeuzwa taka ambayo inaweza kuwahatari na

kuifanya iwe yenyne manufaa kwa hivyo hutatua matatizo ya kiafya yanayoweza kutokana na mirundiko ya taka. Mchanga nao hufaidika kupata virutubishi. Mbolea kama hii inaweza ikatumika kukuzia mboga au maua katika bustani.

Maji taka, hasa yanayotumika kuoshea vyombo, nayo yanaweza kutumika kunyunyizia mashamba madogo ya mboga au bustani za maua. Maji taka haya yanahitaji kutayarishiwa njia mahususi ya kuyaelekeza katika mashamba haya baada ya kutumiwa.

Aghalabu watu wengi wana mazoea ya kuchoma taka. Ni kawaida kupata matanuri ya kuchomea taka katika baadhi ya mitaa, shule na hospitali. Badala ya kupoteza moto huu bure bilashi, inawezekana pakawekwa baridi kubwa au tangi la chuma ambalo litatumia moto huo kuchemsha maji. Maji haya yanaweza yakatumiwa katika shughuli za nyumbani.

Hata hivyo, ni muhimu kukumbuka kuwa kuna baadhi ya taka ambazo ni hatari na huenda zisigeuzwe ili kutumika kwa njia yenyne faida. Taka hizi ni kama vile mikebe au vifaa vingine vyenye kubeba sumu au dawa hatari. Ni bora kuvitupa vifaa hivi katika mashimo marefu au vyoo vya mashimo.

Kwa vyovycote vile, si jambo muhali kwa watu popote wanapoishi kulinda siha yao pamoja na kutunza mazingira. Ulinzi na utunzi huu huhitaji uangalifu mkubwa katika utupaji taka.

### **Maswali**

- a. Bila kupoteza maana iliyokusudiwa, fupisha aya za kwanza tatu. (maneno 70) (alama 2)
- b. Kwa kutumia maneno yasiyozidi 80, eleza manufaa ya taka kwa waja kisha madhara yake. (alama 2)
- 3. MATUMIZI YA LUGHA.**
  - a. Taja na utofautishe sauti sighuna za ufizi (alama 2)
  - b. Taja ala za kutamkia zinazotumiwa kuelezea sifa za irabu yoyote ile. (alama 2)
  - c. Andika neno lenye muundo ufutao wa vitamkwa. Kipasuo si ghuna cha mdomo + irabu ya mbele tandazwa + nazali ya mdomo + irabu ya kati tandazwa. (alama 2)
  - d. Fafanua tofauti iliyopo kati ya kiambishi na mofimu. (alama 2)
  - e. Tunga sentensi ukionyesha matumizi ya vitenzi vya silabi moja katika jinsi ya kutendesha.
    - i. La
    - ii. Nywa
    - iii. Fa(alama 2)
  - f. Onyesha matumizi ya kiambishi ki‘ katika sentensi ifuatayo. Salim atakupikia chakula kitamu kisha upeleke kule chumbani. (alama 2)
  - g. Onyesha sauti mwambatano kwenye maneno yafuatayo.  $(\frac{1}{2} \times 4 = 2)$ 
    - i. Mandhari
    - ii. Kunywa
    - iii. Vushwa
    - iv. Changamka(alama 2)
  - h. Huku ukitoa mifano miwili, fafanua miundo ya majina katika ngeli ya LI-YA. (alama 3)
  - i. Kanusha katika wingi. Uliko ndiko kuliko navyo. (alama 1)
  - j. Tumia kihusishi katika‘ kwenye sentensi kuionyesha :
    - i) Mahali
    - ii) Hali(alama 2)
  - k. Bainisha vitate katika sentensi ifuatayo na ueleze maana yazo. Nyumba hio itahamwa na mbwa aliye na watoto wanaoamwa. (alama 2)
  - l. Akifisha sentensi ifuatayo kuionyesha usemi halisi. hewala amefaulu katika mtihani wake (alama 2)
  - m. Changanua vipashio vya kisarufi katika kiarifa cha sentensi ifuatayo : Wanasagamoyo hawakupendana (alama 2)
  - n. Tunga sentensi na ubainishe namna mbili za uamilifu wa kundi nomino. (alama 2)
  - o. Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu. Mama huwafulia watu nguo zao (alama 2)

- p. Fafanua maana ya kirai, kisha utunge sentensi sahihi ambayo haina nomino kuonyesha kirai nomino.
  - q. Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya matawi. (alama 4)  
Yule abiria aliyejeruhiwa vibaya alipelekwa hospitali kisha jamaa zake wakaarifiwa
  - r. Andika kinyume. (alama 1)  
Sufuria iliyoinjikwa mekonii chafu.
  - s. Sahihisha kwa kutumia kirejeshi cha mazoea. (alama 1)  
Kambarau ambao iliyoundwa vyema haitatizi.
4. **ISIMU JAMII (ALAMA 10)**
- a. Ukiwa mkaguzi mwalikwa katika mashindano ya Kiswahili, fafanua na kueleza mambo yanayochangia wanafunzi kufanya makosa ya kisarufi na ya kimatamshi katika lugha ya Kiswahili.
  - b. Eleza umuhimu wa Isimu Jamii. (alama 5)

for free past papers, visit: [www.freekcsepastpapers.com](http://www.freekcsepastpapers.com)

**FASIHI**

**SEHEMU A : RIWAYA**

**KEN WALIBORA : KIDAGAA KIMEMWOZEA**

**LAZIMA.**

1. ....ukazae watoto ....wakaikomboe Tomoko toka kwa mkoloni mweusi.  
a. Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)  
b. Eleza umuhimu wa msemewa. (alama 4)  
c. Uwajibikaji ni maudhui yaliyodokezwa katika dondoo hili. Thibitisha jinsi mwandishi wa riwaya ya Kidagaa kimemwozea alivyofanikisha maudhui haya ya uwajibikaji. (alama 12)

**SEHEMU B : TAMTHILIA**

**Puline Kea : Kigogo**

**Tibu swali la 2 au 3**

2. Tusiwaruhusu watu wachache waliojazwa kasumba....kutrejesha ....hatuwezi kukubali kutawaliwa kidhalimu tena.  
a. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)  
b. Kwa kumrejelea mzungumzaji wa maneno haya, bainisha unafiki katika kauli hii. (alama 16)  
3. Eleza jinsi mbinu ya tataruki iliviyotumika kufanikisha maudhui katika tamthilia ya kigogo. (ala 20)

**SEHEMU C : HADITHI FUPI**

Jibu swali la 4 au 5.

**Eunice Kimaliro : Mtihani wa Maisha.**

4. —....limuradi mawazo yanamwadhibu sasa”  
a. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)  
b. Fafanua sifa za anayerejelewa katika dondoo hili. (alama 6)  
c. Onyesha mawazo yanayomwadhibu anayerejelewa na dondoo hili. (alama 10)

**Alfa Chokcho : Tulipokutana tena**

5. a. —Mamangu siku ile aliniamsha mapema”  
i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)  
ii) Tathmini umuhimu wa usimulizi wa mzungumzaji katika kuendeleza dhamira ya hadithi hii. (a 8)  
b. Onyesha jinsi mashaka linavyomwafiki mhusika mwenyewe katika hadithi ya —Ndoto ya Mashaka” (alama 8)

**SEHEMU D : FASIHI SIMULIZI**

6. a. Huku ukitoa hoja sita linganisha aina mbili kuu za fasihi. (alama 6)  
b. Jadili vipengele sita vya kuzingatia katika uchanganuzi wa hadithi. (alama 6)  
c. Jadili sifa mbili za vitanza ndimi kwa kurejelea sauti. (alama 2)  
d. Tambua istiatiu zinzotokana na maelezo haya.  
i. Msimulizi wa fasihi simulizi anaitwaje kwa jumla? (alama 1)  
ii. Shujaa katika mighani pia anaweza kuitwa nani? (alama 1)  
iii. Sherehe za kitamaduni ambazo hufungwa na jamii katika kipindi fulani maalum huitwaje? (alama 1)  
iv. Mavazi au vifaa vinavyotumiwa na wasanii kuakisi hali halisi ya mambo wakati wa kuwasilisha fasihi huitwaje? (alama 1)  
v. Mtambaji wa hadithi hutumia ujuzi gani anapoibadilisha hadithi yake moja kwa moja mbele ya hadhira bila kuathiri usimulizi wake? (alama 1)  
vi. Wanaosimuliwa ili kuonyesha kazi ya fasihi simulizi hupewa jina hili. (alama 1)

7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.
1. Wakati tunywapo chai hapa upenuni,  
Na kuwatazama watoto wetu  
Wakicheza bembea kwa furaha.  
Tujue kamba ya bembea yetu imeshalika  
Na bado kidogo tutaporomoka
  2. Kulikuwa na wakati ulinisukuma juu  
Nikaenda zaidi ya nusu duara  
Kulikuwa na wakati nilikudaka  
Ulipokaribia kuanguka  
Na kulikuwa na wakati tulibebana kwa zamu  
Mmoja wima akisukuma mwингine amekaa
  3. Wakati huo, japo tulipaa mbele na nyuma  
Tulicheka kwa matumaini yaliyotiwa chumvi  
Na kisha tukaongozana jikoni kupika chajio  
Ililiwa adhuhuri yetu
  4. Sasa tukisubiri ndoto tusizoweza kuzitekeleza tena  
Tumalizie machicha ya chai yetu ya jioni  
Bila ya kutematema na kwa tabasamu  
Na baada ya hapo tujilambe utamu utamu.  
Uliobakia kwenye midomo yetu
  5. Tukikumbuka siku ilee ya kwanza  
Tulipokutana jioni chini ya mwembe  
Tukitafuta tawi zuri gumu  
La kufunga bembea yetu  
Naye mbwa simba akisubiri
  6. Lakini kabla hatujaondoka kimya kimya  
Kukamilisha nusu duara iliyobaki  
Tuhakikishe vikombe vyetu ni safi. (E. Kezilahabi)

for free past papers, visit: [www.freekcsepastpapers.com](http://www.freekcsepastpapers.com)

## MASWALI

- a. Fafanua maana ya kijuujuu na maana ya kitamathali ya shairi hili. (alama 4)
  - b. Bainisha matumizi ya vipengele vifuatavyo katika shairi. (alama 6)
    - i. Usimulizi.
    - ii. Usambamba.
    - iii. Taswira
  - c. Tambulisha mzungumzaji (nafsi nenii) katika shairi hili. (alama 2)
  - d. Fafanua toni ya shairi hili. (alama 2)
  - e. Eleza maana ya mshororo —Tuhakikishe vikombe vyetu ni safi.” (alama 2)
  - f. Changanua muundo wa shairi hili. (alama 4)
8. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Tuunganeni vijana, ili tugawane kazi,  
Wazee nguvu hatuna, mazito hatuyawezi,

Bora kubadilisha, nanyi vichanga vizazi.

Sisi tulijulikana, miaka iliyopita,  
Tulipokuwa vijana, wenyе siha na mafuta.  
Vikali tulipambana, kuguru mawanda ya vita.

Tulipigana kiume, kuwang'oa walowezi,  
Mikuki yetu na sime, ilichimba yao mizizi  
Ikawabidi wahame, kugura yetu makazi.

Ni kazi itambueni, tuliyoyafanya wahenga,  
Nchi tumeiauni, tokana na kubwa janga,  
Sasa vijana linden, na wazee twaijenga.

Mjitolee maisha, kuilinda kwa adabu.  
Muize kuibadilisha, japo mupewe dhahabu,  
Wazee tutawalisha, kama ilivyo wajibu.

Toka pwani hadi bara, vijana nchi linden  
Tokeni muwe imara, hasa humo mipakani,  
Ajaribuye kupora, vijana mchafueni.

Onyesheni uzalendo, washtuke vibaraka  
Muonyeshe kwa vitendo, na nia zilosafika  
Mujivue na mwenendo, tamaa ya madaraka

Twawahusia wazee, wakongwe wenyе ujuzi,  
Kabisa msilegee, kuridhia upuzi  
Mtu asiwachezee, katika yetu makazi.

### **MASWALI**

- a. Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili.
- b. Bainisha nafsi neni na nafsi nenewa katika shairi hili.
- c. Eleza bahari zozote tatu kwa shairi hili.
- d. Andik ubeti wa tatu kwa lugha nathari.
- e. Huku ukitoa mifano, onyesha ajna mbili za uhuru wa kishairi uliotumiwa katika shairi hili.
- f. Eleza maana ya maneno ya fuatayo kulingana na namna yaliyotumika katika shairi.
  - i. Walowezi      ii. Tumeiauni.
- g. Pendekesa anwani mwafaka katika shairi hili.

**KANGEMA**  
**KISWAHILI**  
Karatasi ya Kwanza  
(INSHA)

**1. LAZIMA**

- Umepata nafasi ya kumhoji Msimamizi mkuu wa Baraza la Mitihani nchini, kuhusu athari za wizi wa mtihani wa Kitaifa katika shule za Sekondari. Andika mahojiano haya.
2. Pendekesa njia za kukabiliana na ongezeko la visa vya utovu wa maadili mionganoni mwa vijana katika jamii.
3. Andika kisa kinachooana na methali mchelea mwana kulia hulia mwenyewe.
4. Tunga kisa kinachomalizika kwa maneno haya.  
... hapo ndipo iliponipambazukia kuwa nilikuwa naogelea baharini pekee kinyume na wenzangu wote.

**KANGEMA**  
**Karatasi ya Pili**  
**(Ufahamu, ufupisho, matumizi ya lugha na Isimujamii)**

**A. UFAHAMU (alama 15)**

Soma ufahamu unaofuata kisha ujibu maswali yanayofuatia

Macho ya Abdul yalipigwa na mwali mkali wa jua la asubuhi. Ilikuwa ndio mara yake ya kwanza kuuona mwanga halisi wa ombwe lijiitalo dunia tangu alipohukumiwa kifungo gerezani. Punde tu komeo la mlango wa seli lilipofunguliwa, ilimlazimu Abdul ayafumbe macho kabla ya kuyafumbua tena taratibu ili yazoee mabadiliko yake.

Ilikuwa ndio siku ya Abdul ya kuachiliwa huru kutoka kwenye kifungo kirefu kilichoyapa macho yake mazoea ya giza la kaburi mle gerezeni. Macho yake yalipokwishaizoea ile hali na kumhakikishia kuwa kila alichokuwa akikiona si kizuka ila uhalisia, alipiga hatua. Akatoka nje ya mlango wa seli, kisha kwa kutoamini, akageuka nyuma kulitazama tena lile pango alimokuwa ametikwa katika muda huo wote. Akayafikicha macho kwa kutoamini huku machozi yakimondoka asijue kama yaliwu ya furaha au.ya huzuni. Alipogeuka kuanza safari ya uhuru wake, macho yake yaliitungu na lango la gereza . Hapo, akasita kidogo, labda kuhakikisha kama kweli alikuwa huru. Bila shaka, hakuna askari wa gereza aliymshikia bunduki au kumuamuru asimame. Walimtzama tu na kumpa tabasamu.

Taratibu, Abdul aliendelea kupiga hatua. Mhemko aliokuwa nao kutokana na hewa safi iliyompenya mapafuni uliufanya moyo wake upige kwa kasi. Ghafla, tabasamu ikapasua mashavuni pake. Akasita. Akaiinua pua yake iliyompa hakikisho kuwa uvundo na uozo wa seli haukuwa naye tena. Ingawa mwili wake uiijaa mabaka ya uchafu na matambara yaliyouficha uchi wake kuvunda, hilo halikumkera tena. Kwa hivyo, akatia tena tabasamu. Lake kuu liliwu shukrani kwa kuepuka yale madhila ya joto na rundo la wafungwa. Na kama hilo halikutosha, aligeuka tena ili sasa kuliangalia lile gereza. Bila kutarajia, alipiga magoti, akainua mikono kupiga dua, —Ew Mungu, niepushe na balaa nyingine.”

Safari ya Abdul kutoka katika majengo ya gereza ilikumbwa na mseto wa mawazo. Alipokuwa katika ujia uliomwelekeza katika barabara kuu, mambo mengi yalimpitikia mawazoni asipate jawabu. Hakujua kama wazazi wake walikuwa wangali . hai, na kama walikuwa bado wanaishi katika nyumba ile ya kukodi kwa miaka hiyo kumi aliyokuwa jela, 'Je, nikiwakosa, nitaenda wapi? Nitaanza wapi kuwatafuta?' Mawazo hayo yaliifungua mifereji ya machozi, kisha ile ya makamasi, Balagha hiyo ilimfikisha katika kituo cha magari ya uchukuzi kwa ule aliuona kuwa muda wa kufumba na kufumbua. Aliyafuta.machozi yake haraka kwa kiganja kisha akaziba tundu la pua, tayari kupenga kamasi. Hata hivyo, kabla hajafanya hivyo, nafsi yake ilimtahadharisha kuwa hatua hiyo ingekatiza uhuru aliopewa kwa kuchafua mazingira. Kwa hivyo akaghairi. Akavuta ncha ya shati lake na kuitumia kama hankachifu kutimiza azma yake.

Hapo kituoni, matatu iliyokuwa mbele ilikuwa na watu wachache. Abdul akaingia na kukaa upande wa kioo ambapo tafakuri nyingi zilimjia. Akakumbuka jinsi kesi yake ilivyoendeshwa kinyume kabisa na ukweli na hukumu kutolewa kinyume cha haki. Mimi Abdul, mtoto twaa tangu kuzaliwa kwangu hata mdudu sijawahi kumponda kwa udole

wangu, ndiyo sasa nije kusingiziwa kuua mtu? Mungu wangu! Kwa nini dunia hii haina wema? Kwa nini wanaodaiwa kuwa wasomi hata wakapewa jukumu la kuwakilisha maslahi ya raia ndio wanaowadhulumu hao raia? Hivi, hata hukimu na tajiriba yake aliamua kufuatalia zile porojo za wanaojiita majasusi? Angeahirisha hukumu yake ili kufanya uchunguzi zaidi, bila shaka nisingepata mapigo na dhuluma hizo zote. Kwa kweli, hii ni dunia ya mwenye nguvu mpishe! Abdul alijisemea.

### Maswali

- a) Kwa nini Abdul alifungwa? (alama 2)
- b) Kwa kurejelea kifungu eleza mashaka katika asasi za kurekebisha tabia. (alama 4)
- c) Ni kinyume kipi kinachoonekana katika kifunga hiki? (alama 2)
- d) Ni mambo yapi yaliyomtia Abdul machugamachuga alipoachiliwa huru. (alama 3)
- e) Abdul anaelekea kuwa na hulka gani. Fafanua kwa kurejelea kifungu. (alama 2)
- f) Msamati ufuatao una maana gani kwa mujibu wa kifungu hiki. (alama 2)
  - i) Ombwe
  - ii) Mhemko

## **2. MUHTASARI (alama 15)**

Soma makala yafuatayo kisa ujibu maswali.

Swala la nidhamu ni nyeti sana ambalo lafaa kushughulikiwa ipasavyo ili mambo yawe shwari katika ulimwengu. Nidhamu inapodiumshwa basi maswala mengine huwa rahisi kutekeleza popote pale. Katika Biblia ni dhahiri kuwa Bwana Mungu aliumba mwanadamu kamilifu, Adamu, akamweka katika bustani ya Edeni ili atawale viumbe wengine. Mungu alimpa Adamu uhuru wa kula chochote alichotaka katika bustani ya Edeni lakini akamkataza kula matunda kutoka kwa mti uliokuwa katikati ya bustani hiyo. Baadaye Mungu akagundua kuwa Adamu alikuwa na kitwea cha ajabu kisha akaamua kuumba Hawa ili awe msaidizi wake. Bila shaka Adamu alifurahi kwa hatua hii. Hata hivyo, Hawa alindanganywa na shetani aliyejuja, kwa mfano wa nyoka, akala tunda walilokatazwa na Mungu na hatimaye akampelekea Adamu naye akala. Matokeo yalikuwa kwamba walijipata uchi kisha Mungu akasirika nao na kuwafukuza kutoka kwa bustani na kuwapa adhabu.

Mwanamume aliambiwa kuwa angefanya kazi na kutokwa na jasho ili apate chakula. Mke naye aliambiwa kuwa kujifungua kungekuwa na uchungu mwingu. Naye nyoka akaambiwa atakuwa na uadui mkubwa kati yake na mwanadamu na angekuwa akifa kwa kugongwa kwenye kichwa. Hata hivyo Mungu hakuwatekeleza wanadamu kabisa. Bwana Mungu alimtuma Yesu akifa mtini ili kila amwaminiye asije akaangamia, bali aweze kupata uzima wa milele. Ni dhahiri kuwa Mungu alikosewa sana na wanadamu aliowaumba lakini hakuwatupa kabisa bali alijajalia nafasi nyingine ya kuwawana wake. Ikiwa Mungu alifanya haya, sembuse sisi binadamu?

Kila mwanadamu hukosea na ni vyema njia mwafaka zifuatwe katika kutekeleza adhabu ili anayeadhibiwa aweze kubadilika na kuona makosa yake. Adhabu inapotolewa ni vyema kwanza kuchunguza cha kitendo. sababu zinazopelekea kutendeka kwa kitendo hicho, dhamira ya mtendaji na athari za kitendo husika, Baada ya haya. mhusika atakuwa katika hali bora ya kutekeleza adhabu.

Katika nchi yetu kwa mfano, adhabu hutolewa katika asasi mbalimbali kama vile shule, vyuo, ndoa kanisa msikiti mionganoni mwa asasi nyingine. Katika ndoa kwa mfano, mke anapokosea mumewe adhabu lazima iambatane na sera za kijamii na kimataifa. Kwa mfano, swala la kuwapiga wanawake au wanaume katika ndoa halifai kabisa katika ndoa yoyote hata kama mtu amefanya kosa gani! Kuna njia mwafaka za kuleta masikilizano katika ndoa kama vile kushauriana, kuomba ushauri, nasaha au pia kwenda kanisani. Pia mambo yamezidi sana ambapo wanawake wakidhulumiwa wanaishia kuwaumiza waume zao sana au hata kuwaua! Swali ni je, ukiua mtu umesuluhisha tatizo lolote? Adhabu yoyote lazima iambatane na uzito wa kosa na pia athari zake kwa mhusika lazima zichunguzwe kabla ya adhabu yenye kutolewa.

### Maswali

- a) Fupisha aya mbili za kwanza. (maneno 60 - 80) (alama 10, moja ya utiririko)

- b) Fupisha aya ya tatu. (alama 5, Moja ya utiririko)

**3. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA. (alama 40)**

- a) Andika sifa zozote mbili za sauti zifuatazo. (alama 2)  
i) /u/  
ii) /ch/
- b) Tenga silabi katika maneno yafuatayo kisha uandike muundo wake. (alama 2)  
i) igwa  
ii) oa
- c) Andika upya sentensi kwa kutumia 'O' rejeshi tamati. Gari lililoanguka si lile unalolizungumzia. (alama 2)
- d) Unda nomino kutoptaka na kivumishi kifuatacho. Tepetevu. (alama 1)
- e) Badilisha katika usemi wa taarifa. Afisa wa usalama alisema kuwa wangemsaidia ikiwa angeshirikiana nao. (alama 3)
- f) Pambanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha Vishale. Letu lilopaliliwa limetuletea mazao wengi. (alama 4)
- g) Ainisha virai vyovytote vitatu. Mwanafunzi yule mtoro hpenda kutembea katikati ya barabara kila wakati. (alama 3)
- h) Tunga sentensi moja kutoptisha vitate vifuavyo:  
i) Chaka  
ii) Shaka
- j) Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao, hali timilifu. Mwanafunzi aliandika insha nzuri. (alama 2)
- k) Andika sentensi hii katika udogo wingi. Mtoto amefunga mlango wa nyumba yao. (alama 2)
- l) Onyesha matumizi mawili ya alama ya vifungo katika sentensi. (alama 2)
- m) Eleza maana ya kishazi. (alama 1)
- n) Nyambua vitenzi vifuatavyo kama ulivyoelekezwa.  
i) Suka (kauli ya kutendata)  
ii) Pa (kauli ya kutendeka)
- o) Onyesha yambwa na chagizo katika sentensi ifuatayo. Babu alijengewa nyumba kwa mawe na Juma. (alama 3)
- p) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kufuata maagizo uliyopewa. Mzazi alishangilia matokeo ya mwana. (Anza: Mwana . . . .)  
(alama 2)
- q) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo. Mama aliniletea Kanga. (alama 2)
- r) Yakinisha. Usiponiita sitaandamana nawe. (alama 2)
- s) Ainisha kitenzi katika sentensi ifuatayo. Mgeni amewasili leo. (alama 1)

**4. ISIMU JAMII.**

1. Tofautisha kati ya uwili lugha na wingi lugha. (alama 4)  
2. Taja sababu sita zinazosababisha watu kubadili na kuchanganya ndimi. (alama 6)

**KANGEMA  
KARATASI YA TATU  
FASIHII**

**1. SEHEMU YA 'A'**

**RIWAYA:**

**Kidagaa Kimemwozea ; Ken Walibora**

1. "Ahaa. Kusema kweli Afrika imepiga hatua kubwa za kimaendeleo baada ya uhuru."

- a) Fafanua muktadha wa maneno haya. (alama 4)  
b) Onyesha kinyume katika usemi huu. (alama 10)  
c) Jadili sifa sita za msemaji wa maneno haya. (alama 6)

**SEHEMU YA B**

**TAMTHILIA:**

2. Tamthilia ya Kigogo ni taswira kamili ya matatizo yanayokumba mataifa mengi barani Afrika. Fafanua ukirejelea Tamthilia nzima. (alama 20)

**SEHEMU YA C**

**HADITHI FUPI**

**Tumbo liloshiba na Hadithi nyingine**

**Jibu swali la 4 au la 5**

3. "Penzi lenu na nani? . . . Mgomba changaraweni haupandwi ukamea. Potelea mbali mkate wee!"

- a) Eleza muktadha wa dondoo hii. (alama 4)  
b) Taja naufafanue mbinu mbili za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili. (alama 4)  
c) Onyesha vile maudhui ya utabaka yanavyo jitokeza katika hadithi nzima. (alama 6)  
d) Eleza sifa sita za mzugumzaji kwenye dondoo. (alama 6)

AU

4. Ilikuwa kama vile katia saini ya kutiwa kitanzil bila ya kutambua vipengele vya sheria za utiaji huo wa kitanzil.

- a) Fafanua tamathali mbili zilizotumika katika dondoo. (alama 4)  
b) Jadili vipengele vitano vya sheria zinazorejelewa katika hadithi nzima. (alama 10)  
c) Onyesha dhiki iliyompata mrejelewa kwa kukosa kivitambua vipengele hivyo. (alama 6)

**SEHEMU YA D:**

**USHAIRI**

**Jibu swali la 6 au la 7**

6. Soma shairi lifautalo kisha ujibu maswali.

Daima alfajiri na mapema  
Hunipitia na jembe na kotama  
Katika njia iendayo kondeni  
Kama walivyofanya babuze zamani;  
Nimuonapo huwa anatabasamu  
Kama mtu aliye na kubwa hamu  
Kushika mpini na kutokwa jasho  
Hi kujikimu kupata malisho.

Anapotembe anasikiliza  
Videge vya anga vinavyotumbuiza

Utadhani huwa vimemngojea  
Kwa usiku kucha kuja kumwimbia;  
Pia pepo baridi kumpepea  
Rihi ya maua zikimletea  
Na ao umande kumbusu miguu;  
Na miti yote hujipinda migongo  
kumpapasa, kumtoa matongo;  
Na yeche kuendelea kwa furaha  
kuliko yeyote ninayemjua  
Akichekelea ha ha ha ha ha ...

Na mimi kubaki kujiuliza  
Kuna siri gani inayomliwaza?  
Au ni kujua aukutojua?  
Furaha ya mtu ni furaha gani  
katika dunia inayomhini?  
Ukali wa jua wamnyima zao  
Soko la dunia lamkaba koo;  
Dini za kudhani zamsonga roho  
Ayalimia matumbo ya waroho;  
Kuna jambo gani linamridhisha?  
Kama si kujua ni kutokujua  
Laiti angalijua, laiti angalijua!

- a) Eleza hali ya mzungumziwa katika shairi hili. (alamu 4)
- b) Huku ukitoa mifano, onyesha aina **mbili** za uhuru wa kishairi ujotumiwa katika shairi hili. (alamu 2)
- c) Fafanua aina **tatu** za taswira ukirjelea ubeti wa pili. (alamu 3)
- d) Eleza umuhimu wa maswali ya balagha katika shairi hili. (alamu 2)
- e) Bainisha vipengele vifuatayo vya kimtindo katika shairi hili:
  - i) tashisi
  - ii) kinaya
  - iii) tashbihi(alamu 3)
- f) Eleza toni ya shairi hili. (alamu 2)
- g) Bainisha nafsineni katika shairi hili. (alamu 1)
- h) Changana muundo wa shairi hili. (alamu 3)

AU

#### 7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yatakayofuata.

Leo kitaka nifike, natamani, ila wauma mwili  
Kwa kazi nihusike, samahani, unahiliki mwili  
Napenda nihesabike, makundini, ila huwezi mwili.

Vitisho pamwe kelele, ninavicha, kwa nafsi na mwili  
Ha ugonjwa utimile, umechacha, na kuudhili mwili  
Msikose simile, magalacha, si gurudumu mwili.

Vingekuwepo viraka, kuutia, ngeushuruti mwili  
Kifundi kivipachika, kuingia, hata kuridhi mwili  
Upya ukaungilikia, kuvutia, roho na wake mwili.

Lakini kamwe haiwi, kuvipata, vipande vyake mwili  
Sihofu kupata mawi, sitajuta, kupigania mwili.

Hata kufutwa sikawi, nitakita, kidete nao mwili.

Kazi ninaithamini, ni hakika, akilini na mwili  
Ila kamwe siamini, kusagika, damu, jasho na mwili  
Uwele hususani, kioneka. nzuvu hitishi mwili.

- a) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili. (alama 4)
- b) Fafanua mbinu **nne** za lugha zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 8)
- c) Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)
- d) Ni nani anayezungumziwa na nafsineni katika shairi hili? (alama 1)
- e) Eleza bahari ya shairi hili kwa kurejelea vipande. (alama 2)
- f) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha ya nathari. (alama 3)

**SEHEMU YA E:**

**FASIHI SIMULIZI**

8. a) Eleza maana ya maigizo katika fasihi simulizi. (alama 2)  
b) Tofautisha aina mbili kuu za maigizo. (alama 4)  
c) Kwa kutoa hoja sita, eleza umuhimu wa maigizo katika jamii. (alama 6)  
d) Kwa kutoa mifano mitatu, onyesha jinsi misimu huzuka. (alama 3)

## **KIGUMO**

**101/1**

### **KARATASI YA 1**

#### **INSHA**

##### **1. Lazima**

- Wewe ni katibu mkuu wa wizara ya kilimo. Mmefanya mkutano wa kuzungumzia mikakati ya kupambana na baa la njaa nchini. Katika mkutano wenu, katibu mkuu wa chama cha msalaba mwekundu amealikwa. Andika kumbukumbu za mkutano huo.
2. Kugatuliwa kwa huduma za matibabu kutoka serikali kuu kumeleta maumivu kuliko tiba kwa wananchi. Jadili
  3. Tunga kisa kinachobainisha maana ya methali: Mbazi ukikosa kuzaa husingizia juu.
  4. Nilikuwa natazama Runinga ya Tupashe Habari, mara nikaona picha ya mtu ambaye nilimfahamu... Endeleta

## **KIGUMO**

### **KIDATO CHA NNE**

#### **MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA PILI**

##### **SEHEMU YA A : UFAHAMU (Alama 15)**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Nchi nyingi duniani zimetia sahihi mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu haki za watoto. Haki hizi ni pamoja na uhai, lishe bora inayotosha na makazi bora yaliyo salama. Hali kadhalika, kila mtoto ana haki ya kupata elimu. Elimu inastahili kutolewa bure, iwe inayofaa na inayopatikana kwa urahisi. Isitoshe, mtoto hastahili kupigwa, kudunishwa, wala kubaguliwa kwa namna yoyote ile; iwe kitabaka, kirangi, kijinsia au vinginevyo. Mtoto hapaswi kufanya kazi za kiutumwa, nzito na za kushurutishwa. Vilevile, mtoto ana haki ya kutunzwa na kulindwa dhidi ya hali yoyote inayoweza kumhatarisha. Fauka ya haya, mtoto anastahili kushirikishwa katika kufanya maamuzi yanayoweza kumwathiri maishani. Pia mtoto ana haki ya kupata huduma za afya, mahitaji maalum na habari kuhusu masuala mbalimbali. Pamoja na hayo, mtoto anastahili kupendwa na kuhestimiwa kimawazo na kihisia.

Haki za wtoto zinatakiwa kulindwa na kila mwanajamii, serikali na wazazi wakiwa katika mstari wa mbele. Hii ndiyo sababuserikali za mataifa mengi zimeshiikisha haki hizi katika katiba na sheria za nchi husika. Yeyote anayezikiuka anapaswa kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria. Walakini, haki hizi bado zinakiukwa. Watoto wengi kote duniani bado wananyimwa haki zao. Kuna watoto ambao hawajawahi hata kupata kibanda cha kuweka ubavu. Wengi hawa

wamejipata wakiselelea kwenye mitaa na hata majaa ya mijji na vijiji ambako hulazimika kupitisha usiku hata katika majira ya kipupwe na masika! Wengine hawapati chakula; licha ya kuwa wanatakiwa kupata chakula chenye lishe bora. Kwao kutarajia mlo awamu tatu kwa siku ni njozi; kwani hata awamu moja ni adimu kupata! La kusikitisha ni kwamaba wale wanaotarajia kuwa vigogo wa kuzilinda haki hizi ndio wanaongoza katika kupalilia ukiukaji wazo. Kila siku tunaskia na kushuhudia visa vya watoto kupigwa, kushinikizwa kufanya kazi za sulubu kipunda, kunyanyaswa kijinsia, kuishi katika mazingira hatari na hata kuuawa. Baadhi ya wanaohusika na vitendo hivi hasi huwa wazazi au jamaa wa karibu kama vile wajomba, shangazi au wahudumu wa nyumbani.

Madhila yanayowapata watoto hayaonekani tu katika mazingira ya nyumbani. Mateso huvuka mipaka na kufikia ngazi ya kimataifa. Watoto wengi katika mataifa yenyе fujo na ghasia hutekwa na kutumikishwa vitani. Linalokata maini ni kwamba baadhi ya viongozi katika mataifa haya hawafanyi lolote kuwanusuru. Lao huwa kuwatazama watoto wanaotakiwa kuwalinda wakigeuzwa kuwa mababe na kuua na kuuana. Watoto hawa huvishwa magwanda amabay mili yao miinyonge haiwezi kuyahimili. Pia hulazimika kuva mabuti ya kijeshi ambayo huwa nanga kwao kubeba, licha ya bunduki zinazokaribia kuwazidi uzani.

Mojawapo ya mambo ambayo viongozi nchini humu walilenga shabaha kuyafikia baada ya kujinyakulia uhuru ni elimu kwa wote. Hata hivyo, hii imekuwa kama ndoto isiyotabirika katika baadhi ya janibu. Ni kweli kwamba sera ya elimu bila malipo katika shule za msingi nchini humu inaendelea kutekelezwa. Hata hivyo, asilimia ya watoto na hata watu wazima wasiojua kusoma na kuandika ingali kubwa. Jukwaa la vijiji nchini humu na hata katika mataifa mengine ya ulimwengu wa tatu limesheheni idadi kubwa ya watoto wasioenda shulen. Kichocheo kikuu cha hali hii ni kwamba wazazi na walezi wamejipata katika lindi la ufukara uliokithiri. Hata wanapo jita hidi kujinyanya na kujikuna

wajipatapo kuyakidhi mahitaji ya kielimu ya wanao, wao hujipata wakitapatapa katika kinamasu hicho hicho cha ulitima. Matokeo ni kwamba watoto wa matajiri wanaendelea kuelimka huku wa maskini wakibakia kwenye kiza cha ujinga. Wanaongangania kuwepo kwa elimu bila malipo ni kama kwamba ni waota ndoto mchana.

Hali ilivyo sasa hivi inadai kuwa mimi na wewe tufanye hima tuungane mikono na kutafuta suluhisho la kudumu kuhusu utekelezaji wa haki za watoto. Twapaswa kuhimiza serikali zetu kufanya kila ziwezavyo kuhakikisha kuwa watoto wote wako shulen. Nasi tushirikiane kutoa huduma kwa watoto na kukomesha dhuluma, mateso na dhiki kwao. Haitoshi kupeleka miswada bungeni kuhusu haki za watoto na kupitisha kuwa sheria. Twastahili kubadilisha misimamo yetu kuhusu haki hizi na kuzilinda kwa dhati.

### **MASWALI**

- (a) Huku ukitoa mifano minne, eleza hali ya kinyume inayojitokeleza katika aya ya pili. (al 4)
- (b) Eleza namna hali ya usalama inavyoathiri utekelezaji wa haki za watoto kwa mujibu wa kifungu. (al 3)
- (c) Kwa kurejelea aya ya nne , onyesha mchangwa serikali katika kuwajibikia haki za watoto. (al 3)
- (d) "wanaong'ang'ania kuwepo kwa elimu bila malipo ni kana kwamba ni waota ndoto mchana," thibitisha kauli hii kwa kurejelea kifungu. (al 2)
- (e) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika taarifa. (al 3)
- (i) vigogo
- (ii) huwa nanga kwao
- (iii) kujikuna wajipatapo

### **SEHEMU YA B: UFUPISHO (Alama 15)**

Kwa kawaida , binadamu huishi kwa kutangamana na binadamu wenzake. Katika kutangamana huku, watu huathiriwa kitabia, kifikira,kimavazi na kimaisha kwa jumla. Watu wote katika jamii wana uwezo wa kuathiri na kuathiriwa na wenzao wa umri mmoja. Hata hivyo, walio katika hatari ya kuathiriwa Zaidi na mahirimu wao ni vijana. Hali hii ya kuathiriana huitwa shinikizo-rika au shinikizo-marika. Vijana huaminiana na kuthaminiana sana. Kwa sababu hiyo, ni rahisi sana kuingizwa katika mitego na wenzao. Isiaminiwe kuwa vijana pekee ndio wanaoathiriwa na shinikizo-rika. La hasha! Watu wazima pia huwafuata wenzao mithili ya bendera kufuata upopo. Mwenzake akinunua gari, yeye pia hukimbilia mkopo kununua gari la sampuli iyo hiyo bila kuwazia kima cha kibindo chake.

Wataalamu wa saikolojia husema kuwa kukabiliana na tatizo la shinikizo-rika si rahisi kwa sababu shinikizo-rika huleta mtarafaku wa kinafsi akilini mwa anayeathiriwa. Nafsi moja humshawishi kufuata wenzake huku nyingine ikimnashi kuandamana na upekee au ubinafsi wake.Shinikizo-rika huathiri sana mahitaji ya kisingi ya binadamu. Ikumbukwe kuwa mahitaji haya ya kimsingi ni ya kila mwanadamu, nayo ni kama vile kupata lishe, hewa safi, kupenda na kupendwa mionganii mwa mengine. Kila mtu hutaka kujihusisha na kundi la watu ambao watamfanya kuhisi kuthaminiwa na kukubalika. Kutokana na haja ya kutaka kukubalika, anayetaka kutambuliwa huridhia matakwa ya wenzake bila hata kuyawazia.

Shinikizo-rika hujitokeza kwa sura nyingi. Mathalani, vijana huwafanya wenzao kuona kuwa wana hatia wasipoafiki kutekeleza kama wanavyoshinikizwa. Kauli kama vile tulifikiri wewe ni mmoja wetu<sup>4</sup> au usiposhirikiana nasi utakuwa umetuvunja moyo<sup>5</sup> hutamalaki. Wanaokataa kushinikizwa hubezwa na kufanyiwa stihizai na wenzao na hata kutengwa. Vitisho hutolewa, wakati mwengine, na anayeshinikizwa akidinda ,mabavu hutumika.

Ni muhimu kwa watu, hasa vijana, kufahamu kuwa shinikizo-rika lipo na wanapokabiliwa na tatizo hilo, watambue kuwa wana haki ya kusimama kidete kutetea msimamo wao dhidi ya wenzao. Kumbuka, baridi huwazizima kondoo kwa namna tofauti.

Kama njia moja ya kukabiliana na shinikizo-rika, wanasaikolojia wanapendekeza watu kujiamini na kuelewa kwamba wana haki ya kuwa na upekee wao. Mtu anapojamini na kushikilia msimamo wake, anaweza kujiepusha na madhara yatokanayo na shinikizo-rika. Asiyejiamini huwa mwepesi sana wa kuingizwa katika lindi la mashaka na wenzake.

### **MASWALI**

- (a) Bila kupoteza maana, fupisha aya ya kwanza na ya pili kwa maneno (40) (alama 8,1 ya utiririko)
- (b) Fupisha mambo muhimu ambayo mwandishi amezingatia katika aya tatu za mwisho.  
(maneno 30) (alama 7, 1 ya mtiririko)

## **MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

- a) Toa mifano miwili miwili ya (al.2)  
i) Sauti ghuna ambazo ni vipasuo .....  
ii) Sauti sighuna ambazo ni vikwamizo .....
- b) Onyehsa mofimu katika neno **Aliyemcha** (al.2)
- c) Andika sentensi yenyе muundo ufuatao (al.2)  
KN(W+V) + KT (t +RH)
- d) Tumia neno shirika kama nomino na kama kielezi katika kutunga sentensi moja (al.2)
- e) Kwa kutunga sentensi yumisha nomino nguruwe kwa kivumishi cha idadi bainifu. (al.1)
- f) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya kutendewa (al.1)  
Mtoto wa waziri amekufa
- g) Yakinisha sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu wingi (al.2)  
Msomi hakutuzwa siku hiyo
- h) Tunga sentensi moja inayobainisha maana mbili tofauti za neno chuma (al.2)
- i) Tambua kiima na aina za yambwa katika sentensi ifuatayo. (al.4)  
Mwalimu mkuu hupigwa nguo pasi na Maria
- j) Kwa kutumia mifano mwafaka fafanua miundo yoyote miwili ya kirai nomino (al.2)
- k) Andika sentensi ifuatayo kwa wingi (al.2)  
Mgeni huyo na mwingine walikula wali kwa uma
- l) Andika neno lenye silabi funge yenyе muundo wa konsonanti moja (al.1)
- m) Badilisha sentensi ifuatayo iwe katika udogo wingi (al.2)  
Ng'ombe wangu ana ndama mdogo
- n) Tunga sentensi zenyе mipangilio ifuatayo; (al.4)  
i) Kishazi tegemezi na kishazi huru  
ii) Kishazi tegemezi na kishazi tegemezi
- o) Eleza matumizi ya ki katika sentensi ifuatayo: (al.3)  
Nyamunga na kitoto wamekuwa wakila, wakiimba kikasuku
- p) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mchoro wa matawi. (al.4)  
Mtoto wa mjomba alikuja kwetu nyumbani jana
- q) Andika kwa msemo wa taarifa. (al.2)  
Yafaa tumwendee mama mkubwa ili atushauri juu ya jambo hili, 'Amina alipendekeza.
- r) Andika kinyume cha: (al.1)  
Chakula hiki kitamu nitakimeza
- s) Tunga sentensi ukitumia viwakilishi vifuatavyo. (al.2)  
i) Kiwakilishi nafsi huru  
ii) Kiwakilishi nafsi kiambata

## **ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

- (a) Eleza sababu tano zilizochangia katika maenezi ya Kiswahili katika Afrika Mashariki kabla ya Uhuru. (al.5)  
(b) Eleza hatua tano ambazo zimesaidia kuikuzalugha ya Kiswahili baada ya Uhuru nchini Kenya. (al.5)

**SEHEMU YA A: USHAIRI**

1. Mbiu naipulizia, kwa wa hapa na wa ng‘ambo,  
Kwani ngoja mesikia, inaumiza matumbo,  
Kwa upole sitafyoa, hata kama kwa kimo mbo,  
Yafaa jihadharia, maisha yas,ende kambo;
2. Maisha yas‘ende kombo, kututoa yetu ari,  
Zingatia haya mambo, wetu walezi mukiri,  
Kuwa wana kwa viambo, huwa Baraka na kheri  
Watunzeni na maumbo, msijezusha hatari
3. Msijezusha hatari, na nyingi hizi zahana,  
Wazazi haya si siri, mawi mnayoandama  
Twaeleza kwa uzuri, matendoyo yatumua.  
Watoto tunayo mori, mi lini mtajakoma?
4. Ni nani mtajakoma, na pombe ziso halali?  
Sio baba sio mama, mbona ny‘hamtujali  
Mwafa ja nzi twasema, mwatuacha bila hali  
Hangaiko acha nyuma, kwani hamuoni hili?
5. Kwani hamuoni hili, kila mwapigana  
Nyumbanizo hatulali, jehanamu tumeona  
Mwatusumbua akili, twaumia tena sana  
Achene na ukatili, kwani upendo hamna,
6. Kwani upendo hamna, Kama mbwa mwatuchapa  
Mwatuchoma sisi wana, mioyeru yatupapa  
Pa kujificha hatuna, tumebaki tikitara  
Maisha hamu hayana, timevunjwa na mifupa.
7. Tumevunjwa na mifupa, hata leo uke wetu,  
Mwatubaka na kuapa, kutung‘ata nyi‘ majitu,  
Maisha hatujakopa, fahamu mkosa utu,  
Hayo makeke na pupa, mtakoma utukutu,
8. Mtakoma utukutu, na kutumia mikiki,  
Na tabia zenye kutu, tumechoka nay chuki,  
Hatutakubali katu, kutendewa yenya siki,  
Serikali fanya kitu, kwani nasi tuna haki.

**Maswali**

- |    |  |           |
|----|--|-----------|
| a) | Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili   | (alama 2) |
| b) | Fafanua tamathali nne za usemi zilizotumiwa katika shairi hili.                            | (alama 4) |
| c) | Taja nafsi neni katika shairi hili.  | (alama 1) |
| d) | Eleza bahari nne zinazowakilishwa katika shairi hili.                                      | (alama 4) |
| e) | Andika ubeti wa nne kwa lugha nathari.   | (alama 4) |
| f) | Eleza maudhui matatu yanayojitokeza katika shairi hili.                                    | (alama 3) |
| g) | Huku ukitoa mfano taja mfano mmoja wa uhuru wa mshairi ambao umetumiwa katika shairi hili. | (alama 2) |

## **SEHEMU YA B:**

### **RIWAYA KIDAGAA KIMEMWOZEA K. WALIBORA**

#### **Jibu swalii la 2 au la 3**

2. —Dunia imepasuka ufa mkubwa usiozibika alaa kulihali”  
 a) Eleza mbinu mbili za lugha zilizotumika.  
 b) Thibitisha ukweli kuwa dunia imepasuka ufa mkubwa usiozibika kwa kumulika matukio riwayani. (alama 12)  
 3. Uchochole umekithiri katika jamii anayotuchorea mwandishi. Thibitisha kauli hii kisha utambue chanzo chake. (Alama 20)

## **SEHEMU YA C: TAMTHILIA KIGOGO PAULINE KEA**

#### **Jibu swalii la 4 au la 5**

4. —Oooh bbi, miaka yaenda mbio sana, nayo sura yako inachujuka.....”  
 a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)  
 b) Mhusika anayehusishwa na wimbo huu ana msimano gani wa kimapinduzi? (alama 8)  
 c) Taja sifa zozote nane za muhusika huyu (alama 8)  
 5. Tamthilia ya Kigogo ni kioo cha uhalisia wa maisha ya jamii nyingi za kiafrika. Thibitisha. (alama 20)

## **SEHEMU YA D: HADITHI FUPI TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINEZO**

#### **Jibu swalii la 6 au la 7**

6. —Rista twambie bwana!”  
 a) Weka dondo katika muktadha (ala 4)  
 b) Taja mbinu zilizotumiwa na mwandishi katika dondoo hili (ala 2)  
 c) Ni kwa vipi mzungumziwa anamchukulia mwalimu mkuu kama hambe? (alama 4)  
 d) Je, mtihani wa maisha ni amwani faafu ya hadithi hii. (alama 10 )  
 7. Jadili mashaka ya Mashaka katika hadithi ya Ndoto ya Mashaka” (alama 20)

## **SEHEMU YA E: FASIHI SIMJULIZI**

#### **8.**

- a) Fafanua mambo yanayochangia kubadilika kwa fasihi simulizi. (alama 10)  
 b) Eleza maana ya lakabu. (alama 2)  
 c) Sifa za lakabu ni zipi? (alama 4)  
 d) Kwa nini lakabu ni muhimu katika jamii. (alama 4)

<b>Previous Score:</b>	<b>Examiner Marks:</b>
_____	—

Husemwa kisirisiri au wazivazi  
Huwa neno moja au fungu la maneno

- Huonyesha majigambo ya mhusika
- Ni jina la kijazanda / kiistiari (Simba mwenda pole)
- Hupendelewa hasa na wasanii zozote  $4 \times 1 = 4$ )

- d) Umuhimu wa lakabu
- Hubainisha sifa ya mtu
  - Hutumiwa kulinda hadhi ya mtu
  - Humtambulisha mtu
  - Hufcsha jina la mtu
  - Huoyesha ubunifu
  - Hudhihirisha weledi katika lugha husika.
  - Hudhihaki hali Fulani.
  - Hufikirisha
  - Huhamasisha wengine kubuni lakabu zao.
  - Hatambulisha kazi ya msanii.

zozote  $4 \times 1 = 4$

## MURANGA SOUTH

**102/1**

### KISWAHILI

#### KARATASI 1

##### INSHA

1. Wewe ni katibu wa Chama cha Mazingira katika kaunti yako. Mwandikie Waziri wa Mazingira mdahilishi/ barua pepe ukimwelezea madhara ya mafuriko na jinsi ya kutafuta suluhisho.
2. —Ehnu bila malipo inafaida na hasara.” Jadili.
3. Tunga kisa kitakacho bainisha maana ya methali:  
Ajizi ni nyumba ya njaa.
4. Andika kisa kitakachomalizika kwa maneno yafuatayo:  
.....Niliachwa kinywa wazi.  
Haikuwahi kunipitia akilini kuwa binadamu anaweza kumtendea binadamu mwenzake jambo kama hilo.

## MURANGA SOUTH

### KISWAHILI

#### KARATASI YA 2

### SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

#### 1. UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma Kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali yanayofuata.

Ripoti ya hivi punde iliyotolewa na taasisi ya Kitaifa kuhusu Takwimu (KNBS) kuhusu uharibifu wa chakula nchini ni ya kutamausha na kila hatua inapasa kuchukuliwa kukabiliana na hali hiyo. Kwa mujibu wa shirika hilo, chakula cha thamani ya shs 150 bilioni kiliharibika mwaka uliopita. Chakula hicho kiliharibika huku maelfu ya Wakenya wakikeketwa na makali ya njaa kutokana na kiangazi cha muda mrefu.

Tani 1.9 milioni za mahindi, ambacho ndicho chakula msingi cha Wakenya wengi, ziliozeana huku wadudu wakivamia takribani magunia milioni sita ya mahindi.

Kwa kweli hizi ni takwimu za kuhofisha au kutamausha. Kwamba, chakula kingi kiasi kinawezu kupotea kutokana na utepetevu wa idara za serikali zinazohusika na uhifadhi wa chakula ni uhalifu wa hali ya juu.

Kuna wale wanaohisi hali hii, ambapo chakula kinavunwa kasha kuachwa kuoza kutokana na ukosefu wa masoko au vifaa nya kutosha nya kuhifadhi chakula ni hujuma ya baadhi ya maafisa na viongozi kutaka kunufaika na masaibu ya raia maskini. Hii ni kwa sababu katika kipindi hicho hicho ambapo kulikuzwa chakula kingi, shs 42 bilioni zilitumika kuagiza chakula, hasa mahindi kutoka nchi za nje. Hali haikuwa tofauti kwa vyakula vingine kama vile matoke na viazi. Kutokana na ukosefu wa maghala ya kutosha na yafaayo, wadudu hatari wa vifukusi huparamia chakula hicho na kuwaacha Wakenya maskini wakikabiliana na makali ya njaa wasijue la kufanya.

Wakati umewadia kwa Wizara ya Kilimo, na hasa, shirika la Kitaifa la Uhifadhi wa nafaka na mazao(KCPB) kuweka mikakati kuhakikisha chakula kinachoalishwa nchini kinahifadhiwa ipasavyo ili kuepusha hali ya sasa ambapo kwa upande mmoja wakulima wanahangaika kutafutia mazao yao masoko kutokana na ukosefu wa maghala ya kutosha, na upande mwingine, wafanyibiashara walaghai wanaruhusiwa kuagiza chakula kutoka nje ilhali mahindi na vyakula vingine vinaoza mashambani.

Mbali na hali ya sasa ya vyakula kuharibikia mashambani, kuna mawakala walaghai ambaa huwapunja wakulima. Mbali na wakulima, wavuvi pia wamehanganyaika pakubwa kutokana na ukosefu wa majokovu ya kutosha. Kutokana na hilo, wavuvi hulazimika kuuza samaki wao kwa bei ya chini mno. Hii ndio hali inayowakumba wakulima na wafugaji nchini na kila juhudhi zinapasa kuchukuliwa kuwanusuru wasiendelee kupunjwa na mawakala.

### **Maswali**

1. Kipe kifungu anwani mwafaka. (al. 2)
2. Uhaba wa chakula unasababishwa na nini? (al. 3)
3. Onyesha kinaya kinachopatikana katika kifungu. (al. 2)
4. Chakula hypotea kutokana na utepetevu wa idara za serikali. Utetevu huu unadhihirishwa vipi? (al. 2)
5. Shirika la Kitaifa la nafaka linaweza kuwafaa vipi wakulima? (al. 2)
6. Wavuvi wana changamoto zipi? (al. 2)
7. Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika kifungu.
  - (i) Wakikeketwa
  - (ii) Utetevu (al. 2)

### **SEHEMU B; UFUPISHO (ALAMA 15)**

Kufufua na kuendeleza uchumi wa nchi ni jambo linalotegemea bidii na ambalo huchukua muda mrefu. Ili kufufua na kuendeleza uchumi wan chi, mbinu zifuatazo zinapaswa kutumiwa.

Kwanza, ni bora kutegemea **rasilimali** iliyomo nchini kwani suruali ya kuazima haisitiri matakao. Ni lazima tukome kutegemea misaada kutoka ng'ambo. Wahenga hawakuwa wenda wazimu waliposema kuwa mtegemea cha nduguye hufa maskini.

Bidhaa zinazonunuliwa kutoka ng'ambo huigharimu serikali kiasi kikubwa sana cha fedha. Tukiyatosheleza mahitaji yetu kwa kutumia bidhaa zinazotayarishiwa humu nchini, uchumi wetu utaimarika. Rasilimali ya nchi hutokana na ardhi. Ardhi yetu ina rotuba katika sehemu nyingi. Tuna mito, maziwa, misitu na madini mbalimbali kama vile dhahabu na aina zingine ambazo hata hazijavumbuliwa bado.

Wakenya wengi hawaithamini kazi ya ukulima. Ukuzaaji wa vyakula kwao ni kama kazi ya **kijungu jikoambayo** huachiwa wasio na tegemeo linguine maishani. Mwelekeo huu ukibadilishwa na tuwe na wakulima wathaminio ukulima, uchumi wa nchi utaboreshwu kwa kiwango kikubwa. Badala ya kukopa pesa nyingi ambazo mara nyingi huwa vigumu kulipa, nchi yetu inafaa iombe misaada. Jambo hili likitokea, wahisani wetu katika nchi za kigeni wataelewa kwani sisi tumo katika taifa ambalo halijastawi kiuchumi. Jambo la kudai malipo kwa kutoza riba kubwa hudhoofisha mno hali ya uchumi wa mataifa yanayoendelea. Riba hutatiza mataifa yanayokopa jinsi kupe afanyakyo anapofyonza damu ya ndama bila huruma wala karaha.

Kuwahimiza wananchi kujitegemea kwa kila njia jambo linaloweza kuifaidi nchi yetu. Si lazima kila mtu aajiriwe ili apate riziki. Sekta ya juu kali ni mfano mzuri wa kuigwa ili wananchi wajitegemee. Hali hii itahakikisha kuwa serikali haitataabika ikijaribu kuwaajiri watu kazi ambazo hazipatikani kwa urahisi.

Hatua nyingine ni utulivu nchini. Nchi yoyote yenye rabsharabsha mionganoni mwa wananchi wake haiwezi kupiga hatua mbele kiuchumi. Utulivu huwapa wananchi nafasi ya kushughulikia wajibu wao na ujenzi wa taifa. Michafuko ikiwepo, serikali hutumia pesa kununua zana za kivita kama vile bunduki za kutolea hewa ya kutoa machozi ili kukabiliana na sokomoko kila mara itokeapo.

Viongozi ni lazima wawe mfano mzuri katika harakati za kuboresha uchumi. Mti ukifa shinale na tanzuze hukauka. Viongozi wenye nyadhifa mbalimbali nchini huwa si mifano mizuri. Wengi wao hujiingiza katika lindi la ujisadi ili kujinufaisha binafsi. Jambo hili huwavunja miyo akina yahe ambaao hawana nafasi za kuwafisidi wenzao. Uchumi wan chi hauwezi kuendelezwa kwa njia hii.

Kazi za viwango vya juu kama vile uhandisi, urubani, unahodha na uanasheria nyakati nyingi hufanywa na wageni kutoka ng'ambo. Watu hawa hupata malipo ya hali ya juu sana. Ni bora serikali igeuze hali hii ili wenyeji wachukue nyadhifa hizi za kiasi cha mishahara kipunguzwe kidogo – na hapo nchi yetu ifaidike kiuchumi.

Kwa kununua hisa za makampuni ya nje, serikali itauendelea uchumi kwa vile itakuwa na kibali cha kufaidika kutokana na faida zinazopatikana kwa makampuni kama hayo.

#### Maswali

- (a) Eleza mabo yanayosaidia kuinua na kuendeleza uchumi.  
(b) Kwa kutejelea kifungu eleza mambo yanayokwamiza uchumi wan chi.

(Maneno 60 – 70) (al. 7)  
(maneno 60) (al. 6)

### **SEHEMU C : SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

1. Eleza tofauti moja kati ya sauti zifuatazo. (al. 2)  
(a) /b/ na /d/  
(b) /z/ na /s/
2. Andika nomino katika sentensi hii. Kuzembea kwake kulimsababishia ukata (al. 2)
3. Mofimu zifuatazo ni za aina gani? (al. 2)  
i) alitufia  
ii) lakini
4. Kwa kutumia mifano eleza matumizi ya alama ifuatayo ya uakifishaji. Paradesi (al. 2)
5. Tunga sentensi zenyе vivumishi vya pekee vya kuonyesha dhana zifuatazo. (al. 2)  
(i) Umilikisho  
(ii) Kutobagua
6. Bainisha virai viwili katika sentensi hii. Mashamba mengi yataandaliwa tena msimu ujao. (al. 2)
7. Changanua kwa kutumia jedwali. Nitakapofika shulen i kaka atakuwa ameondoka. (al. 4)
8. Eleza matumizi matatu ya kiambishi ji. (al. 3)
9. Andika katika usemi halisi. Nilimwambia rafiki yangu kuwa siku hiyo ningejithidi hadi nikamilishe kazi hiyo. (al. 3)
10. Fuata maagizo kwenye mabano kuandika upya sentensi hii. Mama alimkaripia mtoto mtoro. (anza: kwa kitondo .... ) (al. 1)
11. Tunga sentensi itakayodhihirisha kihuishi cha wakati. (al. 1)
12. Eleza matumizi ya kwa na na katika sentensi hizi. (al. 2)  
a) Nyumbani kwao ni karibu kutoka hapa.  
b) Tutatembeleana leo jioni.
13. Huku ukitimia mfano, eleza dhana ya kauli ya kutendata. (al. 2)
14. Bainisha vishazi katika sentensi hii. Mhazili ambaye ni mzembe atapigwa kalamu. (al. 2)
15. Tambua aina za vitenzi katika sentensi ifuatayo. Yule aliyekuwa hapa sio mgeni wetu. (al. 2)
16. Tumia neno **hoi** kama chagizo katika sentensi. (al. 1)
17. Andika katika ukubwa. Mwanaume aliyekamatwa jana alikouwa gaidi. (al. 2)
18. Unda nomino kutohana na kivumishi **mfariji**. (al. 1)
19. Kanusha:  
Utatuimbia nyimbo tamutamu.
20. Eleza maana mbili za neno changa. (al. 2)
21. Neno mbuyu liko katika ngeli gani? (al. 1)

### **SEHEMU D: ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

- MHUSIKA I: Nidhamu , Mheshimiwa Sudi. Hili ni onyo dhidi ya tabia hiyo.  
MHUSIKA II: Nisamehe Bwana.....  
MHUSIKA I: sasa ninakaribisha swali la tatu. Mheshimiwa Mambo, uliza swali lako.  
MHUSIKA III: Ninaomba kufahamishwa ni kwa nini Waziri wa Maji ameshindwa kusambaza  
huduma za maji katika kijiji cha Walalahoi.

Maswali

1. Bainisha sajili ya makala haya. (al. 2)
2. Fafanua sifa za sajili hii. (al. 8)

## **MURANGA SOUTH**

**102/3**

### **KISWAHILI**

### **KARATASI YA 3**

### **FASIH**

#### **SEHEMU I: SHAIRI - LAZIMA.**

#### **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Mwanadamu mambo yake, kueleweka muhali  
Ubavuni umuweke, umtowekule mbali  
Maskanini afike, umtindie fahali Utamu anufaik, sima, bada au wali  
Hatimaye ateuke, kwa viliwa nya samli  
Mwanadamu simuamini, afadhali nyama lumbwi.

Mwanadamu umjenge, awe mwenye kutajika  
Mambo yake uyapange, ukawa wahangaika  
Uwashe wake muwenge, uhakikishe wawaka  
Nao mkono umuunge, vyake viwe vyauungika  
Dhorubani umkinge, asipate kudhurika  
Mara atakusahau, wema wako kafukia.

Mwanadamu mpe cheo, kuwa akutumikie  
Amani yako umpeo, fanaka uirajue  
Kwake iwe kimbilio, wamini akukwamue  
Mwisho takuwa kilio, shika sikio ujue  
Ndio wake mwelekeo, yuauma avuvie  
Mwanadamu mgeuze, pande zote umtizame.

Mwanadamu mfadhili, kwa kila lililo jema  
Pasiwe hata dalili, ya kwake kukosa wema  
Viteko siwe akali, kumbizo zilaterema  
Binadamu takudhili, dhili zako kazitema  
Licha ya zote jamili, mwanadamu si muema.  
Mwanadamu ni mtu, lakini nusu mnyama.

#### **Maswali**

1. Andika anwani mwafaka ya shairi hili. (al. 1)
2. Fafanua dhamira ya mshairi (al. 2)
3. Huku ukitolea mfano onyesha tamathali moja ya usemi iliyotumiwa. (al. 2)
4. Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari. (al. 4)
5. Dondoa mifano miwili ya idhini ya mshairi iliyotumiwa katika shairi. (al. 4)
6. Eleza toni ya mshairi. (al. 1)
7. Fafanua umbo la shairi. (al. 4)
8. Eleza maana ya msamiati ufuatao.
  - (i) Mfadhili
  - (ii) Muhali

## **SEHEMU II: TAMTHLIA - KIGOGO – PAULINE KEA**

### **Jibu swalii la 2 au la 3**

2. — Nini ni mtu wa vitendo, si wa vishindo.”
- (a) Weka dondo hili katika muktadha wake. (al. 4)
  - (b) Kwa kurejelea dondo eleza sifa mbili za mnenaji (al. 4)
  - (c) Thibitisha ukweli wa kauli ya mnenaji. (al. 12)
3. Ukiukaji haki na uvunjaji sheria ni mambo yaliyokithiri katika jimbo la Sagamoyo. Thibitisha. (al. 20)

## **SEHEMU III: RIWAYA – KIDAGAA KIMEMWOZEA – KEN WALIBORA.**

### **Jibu swalii la 4 au la 5**

4. —LoSijawahi kulia kama nilivyolia juzi usiku kaka aliponipiga pambaja na kuniaga akisema hatutadiriki kuonana tena.”
- (a) Eleza muktadha wa dondo hili. (al. 4)
  - (b) Taja na utoe mifano miwili ya mbinu za lugha zilizotumika katika dondo hili. (al. 4)
  - (c) Taja na ueleze sifa nne za msemaji wa dondo hili. (al. 8)
  - (d) Eleza umuhimu wa mhusika huyu. (al. 4)
5. Jadili matumizi ya mbinu zifuatazo za lugha katika riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (al. 20)
- (i) Kisengere nyuma. (ii) Uzungumzi nafsia.

## **SEHEMU IV: HADITHI FUPI;**

### **Tumbo Lisilosiba na hadithi Nyingine.**

6. Kwa kurejelea hadithi ya Tumbo Lisilosiba na ya Mapenzi ya Kifaurongo, fafanua maudhui ya utabaka. (al. 20)

## **SEHEMU V: FASIHII SIMULIZI**

- 7 (i) (a) Misimu/simo ni nini? (al. 2)  
 (b) Eleza sifa bainifu zinazojitokeza katika misimu. (al. 5)  
 (c) Misimu ina umuhimu gani katika jamii? (al. 8)
- (ii) (a) Eleza maana ya ngomezi. (al. 1)  
 (b) Ni wajibu gani ambao huteklezwa na ngomezi. (al. 4)

**KURIA EAST**  
**102/1**  
**KISWAHILI**

**1. LAZIMA**

- Umeteuliwa kuwa mionganoni mwa watakaohutubia wananchi kuhusu hali ya usalama nchini Kenya. Andika hotuba utakayowasilisha siku hiyo kuhusu visababishi vya ukosefu wa usalama na upendekeze hatua zinazofaa kuchukuliwa ili kukabiliana na hali hii.
2. Katiba mpya nchini Kenya haijabadilisha maisha ya wananchi. Jadili
3. Ukioma cha mwenzako kikinyolewa na chako tia maji.
4. Andika insha itakayomalizikia kwa maneno haya:  
.....nilitamani ardhi ipasuke na nitumbukie humo nisionekane tena.

**KURIA EAST**  
**102/2**  
**KISWAHILI Karatasi ya 2**  
**LUGHA**

**1. UFAHAMU:** (Alama 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Kamusi ya Kiswahili Sanifu inafasili neno "dawa" kama "kitu kinachopewa mtu ili apone ugonjwa alio nao". Neno "dawa" pia hutumiwa kumaanisha kitu kinachopumbaza au kutia sumu au kuzua tumbuizo kwa kuduwaaza akili. Kwa mfano, wataalamu wamefikia tamuza kuwa pombe, kwa mazoea, hutuliza ubongo wenye uchovu ilihali bangi hutuliza maumivu na kusababisha kusinzia; nayo majani ya mti unaotumiwa kutengeneza kokeini, hufisha ganzi na kumwezesha mtu kuvumilia uchungu au uchovu.

Na, je, uraibu ni nini? Uraibu in hali ya kujizoeza au kutumia kitu mara kwa mara hadi kutegemea hicho ambacho mtu amekizoea. Kwa hivyo, uraibu ni mazoea ambayo mtumizi ameshindwa kuyaacha. Hali hiyo ya uraibu huanza kwa kitendo ambacho huonekana kana kwamba hakiwezi kamwe kumdhuru anayetumia dawa. Lakini, baada ya muda, fikira zake huanza kuzoea hivi kwamba, hata kabla ya mwili kuanza kutegemea dawa hiyo, akili huitarajia. Hii ni kwa sababu, punde baada ya matumizi, mtu huhisi hali ya utulivu ambao, kwa kweli, si wa hakika bali ni kama uliotiwa chumvi kwani hasa, hauna mashiko.

Kuna aina tofauti za dawa ambazo hutumiwa vibaya na watu. Baadhi ya dawa hizo huzua hisia za kumtia mtu chonjo isiyo ya kawaida. Zingine husababisha ulegevu ambapo mtumizi huhisi usingizi au "ufu" baada ya uti wa mgongo kuathiriwa kisha mtu akakumbwa na hali ya usahaulifu halafu asiweze kufuatiliza fikira kwa mantiki kama kawaida ya binadamu mwenye akili razini hadi kufikia kupoteza fahamu.

Matokeo ya matumizi ya dawa zisizofaa huwa ni mtu kukumbwa na hali hiyo ambapo anajihisi "akiwa juu" na hutamani mno kuendeleza hisia hizo hadi anapokuwa hajiwezi wala kujimudu ndiposa watu huanza kumsema mtu kama huyo — kwamba amehusudu kupindukia hali hiyo ambapo, uraibu huwa umetimia.

Dawa za kulevyia zinaweza kulinganishwa na kisu kinachotumiwa jikoni. Kisu hicho kina kazi maalumu. Kazi yake ni kukata mboga kama kabeji, karoti, nyanya, vitunguu na vyakula kama mikate na vinginevyo. Lakini kisu chicho hicho kinaweza kutumiwa kumkata shingo binadamu! Basi hapo kitakuwa kimenajisiwa — yaani kutumiwa kwa njia isiyofaa.

Kila mara mtu anapomeza tembe au dawa yoyote yenye uwezo wa kusisimua sehemu ya mbele ya ubongo. mtu huyo huhisi msisimko.

Bangi, miraa, pombe (kama chang'aa, busaa, muratina, kwete, kaluvu na zinginezo) na sigara zina mnato ambao humzuzua mtumizi hadi asiweze kujizuia na hata akapuza mambo mengine muhimu angalau apate hisia hizo za kusisimua. Mtu kama huyo, ingawa anatambua kuwa anatumia dawa hizo, hatambui kamwe jinsi zinavyoathiri ubongo wake, na jinsi zitakavyomdhuru siku za usoni.

Baadhi ya wanaouza dawa hizo kwa vijana huwa wanahoji: "Iwapo vijana hawa ni wajinga kufikia kiwango cha kujiruhusu kukubali kuharibiwa miili yao hivyo, basi nami nitakuwa mjinga kama wao iwapo nami sitatumia ujinga huo wao kujipatia faida."

Kwa nduli mwenye maoni kama hayo, wasia ambao tunaweza kumpa ni huu: iwapo haja yako kuu maishani ni kujipatia faida, basi tambua kwamba hucheka kovu asiyefikwa na jeraha. Na iwapo w ewe ni mmoja wa wanaotumia dawa za kulevyia na unaishi kwa mwelekeo wa kujistarehesha kwazo, basi umo kwenye hatari kubwa ya kuwa mtumwa wa hao wanaotafuta faida. Je, unafikiri umo duniani kwa haja ya kujitumbuiza huku ukijidhuru mwenyewe? Matumizi mabaya ya dawa za kulevyia huathiri mwili. akili na roho. Kila mtu anapaswa kujali maslahi ya wenzake katika jumuiya anamoishi na kwa hivyo ni wajibu wa kila mtu kudumisha desturi yenyenye maadili na kuepuka kutumia dawa zinazovuruga akili na kudhoofisha mwili. Kwa kifupi, matumizi ya dawa za kulevyia ni upumbavu mtupu.

Baadhi ya matokeo ya matumizi mabaya ya dawa ni hisia za pumbao la mawazo, kutojali mambo hatari, hamu ya kula kupindukia, ulegevu, vitendo vya kihuni, wasiwasi usio na sababu na hata wazimu. Matokeo mengine hasa ya dawa kama bangi, changaa, pombe na nyingine zinapotumiwa kwa wingi ni kwamba humfanya mtu asiweze kupumua vyema, awe chonjo kuzidi kawaida, mkakamavu kuliko anavyopaswa, mwenye wasiwasi, anayesinzia kila mara, anayehisi kutapika, anayetetemeka viungo, anayeshuku watu kuwa wanamuia kumdhuru, anayetenda vitendo hatari kwake mwenyewe na kwa wenzake na hatimaye husababisha kupoteza fahamu na hata kufariki.

Mtu anapokolewa na dawa mwilini, tabia zake hudhihirisha kuchanganyikiwa akili, kutotambua baina ya hali halisi na hali inaytokana na fikira potofu, kutotambua wakati na kutojali lolote.

### **MASWALI**

- a) Teua Anwani mwafaka kwa taarifa hii. (alama 2)
- b) Taja matokeo ya matumizi mabaya ya dawa za kulevyia kwa mujibu wa kifungu hiki. (alama 4)
- c) Eleza vile walanguzi wa dawa za kulevyia wanavyohalalisha vitendo vyao. (alama 2)
- d) Taja dalili za kuthibitisha kuwa mtumiaji wa dawa za kulevyia amezidiwa na kiwango cha dawa mwilini. (alama 3)
- e) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika kifungu. (alama 4)
  - i) Duwaza.....
  - (ii) Fishaa ganzi
  - (iii) Razini.....
  - (iv) Mnato.....

### **2. UFUPISHO:** (Alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Usasa na mabadiliko katika mitindo ya maisha ni mionganini mwa mambo yanayochangia kuongezeka kwa idadi ya wasichana wadogo kipata mimba. Katika jamii ya zamani ya Kenya, msichana ambaye hajaolewa alipata mimba kwa tukizi sana. Lakini maadili ya kungani yamedidimia sana siku hizi na hivyo kujenga mazingira mwafaka ya wasichana kubeba mimba wakiwa bado wadogo. Imekuwa hali ya watoto kuzaa watoto wenzao. Sambamba ni ongezeko la wasichana wadogo wanaoshika mimba kuondolewa shulenii kwa fedheha inayoambatana na mimba nje ya ndoa.

Usasa umesambaratisha mfumo wa kitamaduni uliohakikisha kwamba akina nyanya wanawafunza wasichana mambo ya kiutuuzima. Vivyo hivyo usasa umewatenganisha wavulana na babu zao waliokuwa chanzo cha hekima ya mambo ya kiutuuzima. Wasichana chungu nzima wanazaliwa na kulelewa katika majiji na miji — mbali na nyanya zao, Vijana wengine — wavulana kwa wasichana, wameachwa kutapatapa katika bahari ya maisha bila mwelekezo kwa vile wazazi wao wenye haya wanashindwa kuwakabili na kusema nao kuhusu mambo ya ngono. Wanabaki kuokotaokota porojo na hekaya za marika zao, majarida ya kutilika shaka, wavuti na sinema zisizoaminika. Vyano hivi vya maelezo kuhusu ngono vinachochea harara katika miili ya vijana hao wanaopitia mabadiliko ya kubalehe.

Utukuzaji wa ngono unatilia shadda na kugeuza ngono kuwa bidhaa ya kibiashara. Hili huchangia dhana potofu kwamba ngono si tu chanzo cha ureda bali chanzo cha kipato. Baadhi ya wasichana wanalazimika kuchuuza miili yao ili kusaidia uzumbuaji wa riziki kwa familia zao. Mara nyingine tokeo ni kupachikwa mimba. Kuenea kwa ufukara kunawasukumiza wasichana wengine kuzika aibu zao na kutumia miili yao kama bidhaa ya kuuza.

Jamii ya leo inayopenda raha ina wanaume wenye ashiki za kinyama wanaowadandia wasichana wadogo na

kuwabaka. Wakati mwengine huwaambukiza magonjwa ya zinaaa sikhambii kuwapachika mimba.

Mimba nyingine za wasichana wadogo hutokana na matumizi ya mihadarati. Wasichana wanaotumia dawa za kulevyta hawawezi kujidhibiti Wanapoteza uhalisia wao na mtazamo wao wa kimaadili. Kwa hivyo, sio mno wao kuhusika katika utovu wa nidhamu ya kingono. Wanaweza kuijingiza katika maisha yanayowaweka katika hatari ya kupata himila. Vivyo hivyo wavulana na wanaume wanaotumia dawa za kulevyta wanaweza kuwashawishi au kuwashurutisha wasichana kufanya mapenzi ya kiholela.

Kwa kweli dunia imebadilika sana siku hizi. Siku hizi kuna wasichana wengi wanaopachikwa mimba kabla ya ndoa kuliko enzi ya kabla uhuru. Athari ya himila hizo za mapema ni nyingi. Wasichana wadogo hujipata wamekuwa wazazi wa watoto ingawa wenyewe wangali watoto. Jukumu la kulea vitoto vyao huwa gumu. Hali huwa mbaya zaidi wavulana au wanaume waliowapachika mimba wanapodinda kuhusika au kukataa kusaidia gharama ya malezi. Ndipo kukawepo watoto wengi wanaolelewa na mzazi mmoja – ambapo mara nyingi mzazi huyo mmoja tu ni mama. Baba anakuwa fumbo na tena mkimbizi mkubwa. Wakati mwengine msichana anapopata mimba hukataliwa na wazazi wake au kukatisha masomo yake. Aidha, anaweza akaaadhirika kiafya kwa kubebeshwa mimba ilihali mwili wake haujakomaa vya kutosha. Maisha humgeukia kuwa sawa na kukwea mlima Kilimanjaro.

- a) Ni kwa sababu gani idadi ya wasichana wadogo wanaopachikwa mimba imeongezeka. (Maneno 100)  
(Alama 9, 1 utiririko)
- b) Fupisha aya ya mwisho. (Maneno 40)  
(Alama 6, 1 utiririko)
3. **MATUMIZI YA LUGHA:** (Alama 40)
- a) Eleza sifa mbili mbili za sauti hizi.  
/i/.....  
/ch/.....  
(alama 2)
- b) Huku ukitoa mifano tofautisha ala sogezi na ala tuli.  
(alama 2)
- c) **Yakinisha.**  
Mamlaka makubwa ya Rais hayakwazi juhudhi za upinzani.  
(alama 1)
- d) Huku ukitoa mifano, tofautisha silabi fungo na silabi wazi.  
(alama 2)
- e) Tia shadda katika neno lifuatato ili litoe maana mbili tofauti.  
Walakini  
(alama 2)
- f) **Andika katika usemi wa taarifa.**  
—Ntawafuta kazi wafanyakazi wote wanaozembea kazini.” Waziri aliwaonya.  
(alama 2)
- g) Tunga sentensi moja ukitumia nomino katika ngeli ya U - YA.  
(alama 2)
- h) Tumia kitenzi –fa katika sentensi sahihi kuonyesha kauli ya kutendesha.  
(alama 1)
- i) Tambua kiima na yambwa katika sentensi hii.  
Mwanafunzi alipewa zawadi na mwali muu.  
(alama 2)
- j) Tambua na ueleze hali na nyakati katika sentensi hii.  
Sehemu hii yampendeza mtu ambaye anapenda kitalii.  
(alama 2)
- k) Changanya kwa njia ya jedwali.  
Wanafunzi wengi waliosoma kwa bidii hawakuathirika na udanganyifu wa mitihani.  
(alama 3)
- l) Bainisha maana mbili zinazotokana na sentensi hii.  
Wanafunzi walosomeana barua.  
(alama 2)
- m) Tumia chagizo ya idadi badala ya uliyopewa katika sentensi ifuatayo.  
Tulimtembelea nyanya Jumamosi iliyopita.  
(alama 2)
- n) Bainisha matumizi ya kiambishi KU katika sentensi hii.  
Mkurugenzi hakukusaidia ulipoenda kule Mombasa anakofanya kazi.  
(alama 3)
- o) Andika Methali inayojumuisha ujumbe ufuatao.  
Hata mtaalamu huhitaji kutafuta msaada wa wataalamu wenzake.  
(alama 2)
- p) Bumba ni kwa nyuki ..... ni kwa samaki na ..... ni kwa siafu.  
(alama 2)
- q) Tunga sentensi moja kutofautisha kimaana jozi lifuatato.  
Pure.....  
Bure.....  
(alama 2)
- r) Tunga sentensi moja kuonyesha maana mbili za neno: Mradi.  
(alama 2)
- s) Taja dhana zinazowakilishwa na Mofimu zilizopigiwa mstari.  
(alama 2)
- i) Someni.....

- t) ii) Ukuta ..... (alama 2)  
Unda majina mawili kutohana na neno **dhuru**.
4. **ISIMUJAMII** (Alama 10)
- a) i) Eleza dhana ya misimu. (alama 1)  
ii) Taja sifa nne za misimu. (alama 4)  
(i) Eleza maana ya lakabu. (alama 1)  
(ii) Eleza dhima ya lakabu katika jamii. (alama 4)

for free past papers, visit: [www.freekcsepastpapers.com](http://www.freekcsepastpapers.com)

**SWALI LA LAZIMA****KIGOGO**

1. .... Hivi vishahada vyao wanavyovipata siku hizi vinawavimbisha kichwa! Mtu anaitwa daktari na hata kazi ya maana hana....  
 a. Weka dondo hili hili katika muktadha wake (Alama 4)  
 b. Fafanua mbinu mbili za sanaa alizozitumia mwandishi (Alama 4)  
 c. Ukirejelea tamthilia ya Kigogo, dhihirisha kuwa mtu anaitwa daktari na hata kazi ya maana hana. (Alama 12)

**SEHEMU YA B: RIWAYA:****KIDAGAA KIMEMWOZEA – KEN WALIBORA****Jibu swali la 2 au 3**

2. Ujenzi wa jamii mpya ni wajibu wa vijana. Thibitisha ukweli wa kauli hii ukirejelea riwaya ya Kidagaa Kimemwozea.  
 AU (alama 20)
3. —Lowela tunapendana mno na ni msiri wangu wala hakuogopa kuniambia yaliyojiri.  
 (a) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)  
 (b) Fafanua yaliyojiri kwa mujibu wa msemaji. (alama 8)  
 (c) Lowela ni kielelezo kibaya cha msichana wa kisasa. Thibitisha. (alama 8)

**SEHEMU C: HADITHI FUPI: TUMBO LISILOSHIBA****Jibu swali la 4 au 5**

4. —Hatchukua muda mrefu, akili zao zilipowaamsha kuwapeleka kwenye maana hasa ya kile kilichokuwa kikitokea ...”  
 a. Eleza muktadha wa dondo hili (Alama 4)  
 b. Fafanua tamathali ya usemi aliyoitumia mwandishi katika dondo hili (Alama 2)  
 c. Fafanua kile kilichokuwa kikitokea (Alama 2)  
 d. Eleza juhudzi zilizofanywa kuzuia kilichokuwa kikitokea kisitokee (Alama 12)
5. a. Ulezi umewapa wazazi wengi changamoto nyingi. Ukirejelea hadithi ya shogake, dada ana ndevu dhihirisha ukweli wa kauli hii (Alama 10)  
 b. Fafanua changamoto zinazokabili asasi ya ndoa ukirejelea hadithi ya Masharti ya kisasa (Alama 10)

**SEHEMU YA D: USHAIRI****Jibu swali la 6 au 7****6. Soma shairi hili kasha ujibu maswali yanayofuata:**

Jukwani naingia, huku hapa pasokota,  
 Kwa uchungu ninalia, hii tumbo nitaikata,  
 Msiba mejiletea, nimekila kiso takata,  
 We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

Wazee hata vijana, wote umewasubua,  
 Huruma nao hauna, heshima kawakosea,  
 Ukambani na Sagana, hata mbwa wararua,  
 We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

Wahasibu ofisini, kibwebwe mejifunga,  
 Miaka mingi vitabuni, ili wasikose unga,  
 Nadhari wanadhamini, hesabu wanazirenga,

We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

Wapenzi wa kiholela, pia wanakuogopa,  
Baada yao kulala, wana wao wanatupa,  
Wakihitaji chakula, wanachokora mapipa,  
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

Wafugaji hata nao, kama dawa wakwamini,  
Hawajali jiranio, wamesusia amani,  
Wanaiba ng'ombe wao, na kuzua kisirani,  
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

Nayo mizozo ya maji, kaonekana kwa mara,  
Hiyo nayo ni dibaji, sababu sio harara,  
Njaa wahepe wenyeji, huo ndio mkarara,  
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

Ningeweza kukuza, ingekuwa siku njema,  
Tena kwa bei ya meza, sokoni nimesimama,  
Wala tena singewaza, kuhusu wali na sima,  
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?  
Hatima umefikika, naenda zangu nikale,  
Mate yanidondoka, kwa mnukio wa wale,  
Naomba kwenda kukaa, wala sio nikalale,  
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

### **Maswali**

- (i) Lipe anwani mwafaka shairi hili. (alamu 2)
- (ii) Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu. (alamu 2)
- (iii) Huku ukitolea mifano mwafaka, taja arudhi zilizotumiwa katika ubeti wa tatu. (alamu 4)
- (iv) Andika ubeti wa nne kwa lugha nathari. (alamu 4)
- (v) Thibitisha kuwepo kwa idhini ya ushairi. (alamu 2)
- (vi) Taja madhila anayoelezea mtunzi wa shairi hili yaletwayo na tumbo. (alamu 4)
- (vii) Elezea maana ya maneno yafuatayo.
  - (a) Dibaji
  - (b) Harara(alamu 2)

AU

### **7. FASIHI SIMULIZI.**

- i) Eleza maana ya misimu. (alamu 2)
- ii) Eleza dhima ya misimu. (alamu 4)
- iii) Taja aina **nne** za ngomezi za kisasa. (alamu 4)
- iv) Eleza sifa **nne** za maapizo. (alamu 4)
- v) Eleza kikwazo **vitatu** vinavyokumba Fasihi simulizi. (alamu 6)